ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 07Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kuwasilisha mezani kauli ya Serikali kuhusiana na Skuli ya Darajani na Vikokotoni katika uendelezaji wa Ukanda wa Darajani *(Darajani corridor).* Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na yeye aje aweke mezani.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ili nae aje aweke hati mezani. Kwa niaba yake Mhe. Ussi Yahya Haji.

Mhe. Ussi Yahya Haji (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa niaba ya

Mwenyekiti naomba kuweka hati mezani Hotuba ya maoni ya kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Katibu kwa shughuli inayofuata.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 115

Matumizi ya Uwanja wa Mpira Tibirinzi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Mji wa Chake Chake ambao ni Mji Mkuu nambari mbili Zanzibar umekuwa na msongamano wa watu pamoja na magari kutokana na ufinyu wa maeneo. Pamoja na ufinyu huo wa nafasi, uwanja wa Mpira wa Tibirinzi baadhi ya wakati hutumika kwa mikutano ya kisiasa na kusababisha hatari ya kukosa amani na utulivu kwa watumiaji wa Mji huo, wafanyabiashara na hata vikosi vya ulinzi kukosa udhibiti wa usalama wa watu na mali zao.

(a) Je, uwanja huo unamilikiwa na taasisi gani ya Serikali.

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kutumia uwanja huo kwa mikutano na shughuli za kisiasa ni hatari.

(c) Kama ni hatari kutokana na kukosekana kwa usalama, ni lini Serikali itapiga marufuku kutumika uwanja huo kwa mikutano na shughuli za kisiasa na kuendelea na matumizi ya michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 115 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika**,** naomba nikiri kwamba Mji wa Chake Chake umekuwa na msongamano wa watu pamoja na magari kutokana na ufinyu wa nafasi hususana katika eneo la mji huo. Mhe. Spika, Matumizi ya Uwanja wa Mpira wa Tibirinzi kwa mikutano ya kisiasa ni jambo linaloeleweka,ingawa hadi sasa hatujapata taarifa rasmi katika vyombo vya Ulinzi na Usalama kuwa mikutano hiyo ya kisiasa inahatarisha amani na utulivu kwa watumiaji wa mji huo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Uwanja wa Mpira wa Tibirinzi unamilikiwa na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo pamoja na taasisi za Ulinzi na Usalama italifanyia kazi wazo la Mhe. Mjumbe na ikibainika kuwepo kwa kasoro hizo tutashauriana Serikali juu ya hatua zinazostahiki kuchukuliwa.

(c) Mhe. Spika, kama nilivyojibu hapo awali ni kwamba maamuzi ya matumizi ya Uwanja huo yanategemea uamuzi wa Serikali baada ya kufanyika uchunguzi juu ya kasoro zilizoelezwa na Mhe. Mwakilishi. Nakushukuru.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa sababu amekubali kutokana na msongamano pamoja na matatizo ambayo yanajitokeza katika maeneo hayo, na wakati Tibirinzi ni eneo la Ikulu na ndio njia ya Ikulu. Mimi nililozungumza hasa katika mikutano ya kisiasa.

(a) Je, waziri yuko tayari kupiga marufuku mikutano ya kisisa katika mji wa Chake Chake.

(b) Ana uhakika kwamba uwanja wa Tibirinzi una waraka wa Wizara ya Habari.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mahitaji wa uwanja unapofika wakati wa kipindi cha kampeni na kipindi cha uchaguzi yanakuwa ni makubwa mno. Na dhamira ya Tume ya Uchaguzi ni kutafuta maeneo ambayo yanaweza yakutumia viwanja vile kwa kipindi kifupi. Ndio maana sote tunajua katika kipindi chote cha mikutano taasisi zetu za Ulinzi na Usalama zinakuwa *alert* kuhakikisha mikutano ile inafanyika katika hali nzuri na yenye usalama mkubwa.

Sasa si jambo jema kwa serikali kupiga marufuku mikutano ya kisiasa katika viwanja hivi kwa sababu wakati mwengine sisi tunaotokana na Vyama vya siasa ndio ambao tunakuwa na mahitaji wa viwanja hivi. Lakini pale ambapo tutapata taarifa za kutosha kutoka katika taasisi zetu na Idara zetu za Ulinzi na Usalama hatutochelea kupiga marufuku. Lakini kwa sasa kama ambavyo tumemjibu katika

jibu letu hatujapata taarifa ya kina kutoka katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama ndio maana bado hatujapiga marufuku. Ikitokea kufanya hivyo basi hatutochelea.

(b) Uhakika kwamba uwanja huu una hati ya Wizara ya Wizara ya Habari. Kama ambavyo nimezungumza awali kiwanja hiki kinamlikiwa na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Hivyo suala la hati hususan itakuwepo katika taasisi husika na kama bado watakuwa hawajautafutia hati taasisi husika itakuwa na wajibu wa kufata taratibu ili kuweza kupata hati iseje ikatokezea watu wengine wakajimilikisha viwanja hivyo. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 14

Utaratibu unaotumika katika kufuatilia Mashamba ya Mikarafuu

Mhe. Maryam Thani Juma (kny) Mhe. Khadija Omar Kibano - Aliuliza**:**

Miongoni mwa lengo kuu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuweza kuondosha malalamiko makubwa yanayojitokeza siku hadi siku kwa baadhi ya wakulima wetu hususan wale waliopewa mashamba ya eka tatu ya Mikarafuu. Hata hivyo, inapofikia wakati wa chumo la zao hilo hujitokeza baadhi ya watendaji wa Serikali kupita katika mashamba hayo yaliyokodishwa bila ya kutoa taarifa yoyote kwa wamiliki wa mashamba hayo wakodishaji.

(a) Je, watendaji hao huwa wanatumia vigezo gani mpaka kufanya hivyo bila ya kutoa taarifa kwa wamiliki.

(b) Je, ni utaratibu upi uliowekwa kisheria kwa watendaji wa Serikali wanapopitia mashamba yote yaliyokodishwa kwa wananchi kutoka Serikalini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye kifungu (a) na (b). Kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kazi ya ukodishaji wa mashamba ya mikarafuu watendaji hutoa matangazo kwenye redio ikiwemo *ZBC*, *Zenji Fm*, radio jamii na Radio Istiqama. Pia maofisa hufika kwa Wakuu wa Wilaya husika kueleza azma hiyo ya ukodishaji mashamba ya Serikali. Aidha kopi za matangazo hayo huwekwa kwenye mikusanyiko ya watu kama vile sokoni, migahawani na maeneo mengine.

Mhe. Spika, Sasa naomba kujibu swala a na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi huandaa ratiba na orodha kwa kila Shehia na kopi yake hupatiwa masheha husika kwa ajili ya kuwajuilisha wanaosimamia mashamba hayo pamoja na wananchi wanaotaka kukodi. Aidha, sio mashamba yote ya eka huwa yanakodishwa na Wizara hii ni yale tu ambayo hayana mikataba ya umiliki.

(b) Mhe. Spika, Kazi zote za serikali huendeshwa kwa mujibu wa katiba, sheria na kanuni za nchi. Kwa msingi huo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeagizwa na serikali kuyatafuta na kuyakodisha mashamba yote ya serikali ambayo hayana mikataba ya umiliki. Hivyo, mikataba ya umiliki wa mashamba ya eka tatu inawapa uwezo maofisa

wanaohusika na usimamizi wa mashamba ya serikali kupitia na kuona maendeleo ya mashamba hayo. Hadi sasa Wizara imeshayatambua mashamba 5,822 kati ya mashamba 8,215 tuliyokabidhiwa kutoka Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Mashamba 2,324 yaliyotambuliwa yapo Mkoani, 1,417 yapo Chake Chake, 831 yapo Micheweni na 1,250 yapo Wete. Hata hivyo, kazi ya kuyatambua mashamba yaliyobaki bado inaendelea.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni mapato kiasi gani yamepatikana kwa kukodisha mashamba hayo katika kipindi cha 2016/2017.

(b) Ni wahusika gani huyashughulikia mashamba hayo kuyasafisha ili kuona kwamba uzazi wake unaongezeka.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naomba kwa idhini yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kuhusu takwimu za mapato naomba nitamletea kwa maandishi sina takwim hapa sasa hivi. Lakini kuhusu kushughulikiwa fedha inayopatikana kwa yale mashamba yanayo mikataba na wale watu ambao tumewakabidhi kwa mtakataba kuna asilimia fulani tunawakabidhi asilimia 30 ambayo inasaidia kusafisha mashamba.

Lakini nataka nikiri ni kweli kuna mashamba mengi kutokana na uchache wa wafanyakazi na fedha chache inayopatikana yamekuwa bado hayajawezwa kusafishwa yote kikamilifu. Sasa hivi serikali inaanza kuangalia utaratibu mpya wa kuweza kuyakabidhi mashamba haya na kuhakikisha yako safi mpaka

wakati huu itakapomaliza serikali itatoa kauli rasmi utaratibu gani wa kuweza kuyatunza mashamba haya tutautangazia rasmi wananchi na wakodishaji kwa jumla.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini pia napenda nimuulize swala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri ijapokuwa mashamba haya watendaji huwa wanafatilia kwa kuyasafisha ili mazao yawe mazuri zaidi. Lakini je, ni taratibu gani wanazozichukua endapo wanapokodisha wale watu na kipindi ambacho wanachuma ni taratibu gani ambazo wanazifuatilia kwa hawa wachumaji wa karafuu ili wasiharibu hii mikarafuu na iweze kuzaa zaidi kila kipindi kinachofata.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane kwamba wakati mwingi watu wanakodisha mikarafuu huona zaidi wanashughulikia kuchuma karafuu na wakati mwengine hata kukataa matawi katika mikarafuu. Kwa jambo hilo sasa serikali inakuja na utaratibu mpya wa kukodisha mikarafuu ili tuhakikishe tunaempa mikarafuu tunampa na jukumu la kuweza kuitunza na pale ambapo atavunja utaratibu basi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, tutakuwa na mikataba maalum hatutokwenda kama hivi tunavyokwenda hivi sasa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri mimi nina swali moja (a) na (b).

(a) Kuna utaratibu gani wa kumkodisha yule ambaye analishughulikia shamba au kumpokonya yule na kumpa yule

ambaye kwa wizara imeona ni wa kumpa ili, maana yake kuna utaratibu gani wa kumpokonya shamba yule mshughulikiaji wa shamba baadae ukampa mtu mwengine lile shamba au ukamkodisha mtu wengine.

(b) Ni *percentage* ngapi baada ya kulikodisha yule anayelihudumia anapata katika pato lile.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu ni kwamba yule ambaye analishughulikia shamba hupewa nafasi ya kwanza kabisa katika kukodi anaposhindwa kutokana na ile thamani ambayo imefanywa ndio tena hupewa mtu mwengine. Lakini kwa nafasi ya kwanza hujapata yeye sasa *privilege* anayoipata yeye ni kwamba nafasi ya kwanza kwamba huyu shamba linakodishwa kiasi fulani baada ya kamati inayofanya tathmini kupita na kujua kiwango cha kukodisha, basi yeye hupewa *priority number one* kwamba wewe thamani ya kukodi hii je, unaweza kukodi au huwezi. Kama hauwezi ndio anapewa mtu mwengine akiweza anakodishwa. Huu ndio utaratibu ambao tunautumia.

(b) Vile vile kuna asilimia ndogo huachiwa kwa ajili ya kulisafisha lile shamba kwa sababu yeye ndie analishughulikia lile shamba. Kwa hiyo, pia hupata *facility* ya pili hiyo ni ya kupewa *percent* fulani ya kuweza kushughulikia shamba.

Kuhusu suala la pili la samahani Mhe. Spika, sikulisikia vizuri lile suala.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Suala la pili umeshalijibu lakini *percent* hukuitaja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: *Percentege* kwa kweli mara nyingi ni asilimia isiyozidi 30 ndio asilima ambayo tunamwachia mtu katika wale wanaosafisha mashamba.

Nam. 134

Kuiwezesha *ZRB* Kibajeti ili Ifikie Malengo ya Makusanyo

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa kipindi cha Bajeti ya mwaka 2016/2017 Bodi ya Mapato Zanzibar ilikadiriwa kupatiwa jumla Tsh. Billioni 12 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kukusudia kufikia lengo la kukusanya Tsh. 272.64 Billioni kutoka katika vyanzo vyake vya kodi na Tsh. 35.20 Billioni kutoka vyanzo visivyokuwa vya kodi.

(a) Je, Mfuko Mkuu wa Serikali umetoa kiasi gani cha fedha kuwapa *ZRB* kwa lengo la kuongeza nguvu ili kujiimarisha katika kusimamia vyema ukusanyaji wa kodi.

(b) Je, *ZRB* wamekusanya kiasi gani cha kodi hadi kufikia mwezi Februari, 2017, kwenye lengo la ukusanyaji kodi la 272.64 Billioni .

(c) Je, ni lini *ZRB* itaanza mpango wa lazima wa kuwasajili na kutoa namba za usajili walipa kodi kwa wafanyabiashara wote ambao hawajasajiliwa na kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara ili waweze kujisajili na kulipa kodi zao zinazostahiki kulipwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 (a), (b) na (c) lakini kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kipindi cha miezi tisa cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Mfuko Mkuu umetoa TZS 9.02 bilioni kwa *ZRB* sawa na asilimia 75 ya lengo.

(b) Mhe. Spika, Hadi kufikia mwezi wa Febuari, 2017 *ZRB* imekusanya TZS 197.34 bilioni ambalo ni sawa na asilimia 71.3 ya lengo la TZS 272.64 bilioni na sawa na asilimia 106.19 ya lengo lililowekwa la TZS. 194.43 bilioni.

(c) Bodi Mapato Zanzibar kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi, nambari 7 ya mwaka 2009 tayari inatoa namba za usajili kwa wafanyabiashara wote kutegemea na Kodi anayohusika nayo. Sheria inataka mtu yeyote kujisajili *ZRB* kabla ya kuanza biashara yake.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na muelekeo mzuri wa *ZRB* kwa kutuongezea makusanyo, mimi nawapongeza sana kwa kufikia lengo hilo. Lakini je, *ZRB* haioni kwamba sasa ipo haja ya kuwafuata wafanyabiashara hao na kuwapatia *tin number* baada ya yao kuwasubiri afisini ili wafanya biashara wale wende wakajiandikishe na wanachukuwa muda na jambo hili wafanyabiashara saa nyengine wanaliona ni usumbufu na hatimae kuacha kwenda kujisajili na wakakosa hiyo *tin number* na ikawa idadi halisi ya wafanyabishara kutokutambulika. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, hicho alichokisema Mheshimiwa Mwakilishi ndicho kinachofanywa na Bodi yetu ya Mapato na hivi sasa kuna utaratibu wa kuweka *block* na nasema kwamba ni *block management* kila eneo na wameshaanza *plot* katika eneo la Mlandege na wanaendelea sasa hivi eneo la Kwahajitumbo, kwamba katika maeneo hayo wanaangaliwa wafanyabiashara wote waliopo katika eneo hilo na wale wanaostahiki kusajiliwa wanasajiliwa. Sasa hatua hiyo tayari imeshaanza na itakwenda kwenye maeneo yote na kinachohitajika ni kwamba wale wote wanaostahiki kusajiliwa kama walipa kodi wasajiliwe na wapewe *tin number* zao.

Mhe. Mwinyihaji Makame: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na azma nzuri waliyonayo *ZRB* ya kutukusanyia mapato na kwa kweli wanastahili pongezi sana. Naomba sasa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, najua serikali imeshaanza utaratibu wa kuwataka wafanyabiashara watowe risiti kwa kila wanachokiuza, lakini ukweli hawafanyi hivyo.

Je, *ZRB* itasimamia vipi zoezi hili ilituone kwamba mapato ya serikali yanazidi kuimarika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza ni kiri kuwa ni kweli kuna wafanyabiashara ambao hadi sasa wanaendelea kutotoa risiti. Lakini vile vile nikiri kwamba wako wananchi ambao nao hawadai kupatiwa risiti hizo. Kwa hivyo, hapa ni suala la taaluma ziendelee na *ZRB* inafanyakazi hiyo, ina vipindi mbali

mbali ambavyo vinarushwa kwenye *ZBC* kutoa taaluma, lakini pia kukaa na wafanyabiashara hawa, hivi karibuni tuliwakusanya wafanyabiashara na kuwaelezea umuhimu wa wao kulipa kodi zao, lakini na wananchi pia kudai risiti wakati wanapofanya manunuzi ya mahitajio yao mbali mbali ambayo yanastahiki kutolewa risiti.

Mhe. Spika, sasa hilo moja la taaluma tutaiendeleza. Lakini la pili kuna huu utaratibu wa kuanzisha matumizi ya (*EFD)* yaani *Electronic Feasible Defined* ambayo tunataka ndani ya mwaka wa fedha 2017/2018 basi tuwe tumaanza kutumia *EFD*, ambayo tunahisi nayo hiyo itatusaidia sana katika ukusanyaji wa mapato ya serikali. Kwa hivyo, suala la *EFD* lakini vile vile suala la kuhakikisha kwamba tunatoa taaluma, lakini jengine zaidi ni ufuatiliaji. Kazi hiyo imeshaanza na itaendelezwa kuhakikisha wale wote wanaokwepa kutoa risiti kwa maana ya kukwepa sasa ulipaji wa kodi nao tutawatia hatiani kwa mujibu wa sheria zilizopo katika nchi hii.

Nam. 86

Ubovu wa Nyumba ya Mwalimu wa Jambiani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, sasa hivi niko tayari kusubiri swali ambalo nimelileta ndani kama mtumishi au mtumwa wa wananchi wa Jimbo la Paje ambalo limekuwa kero kwa muda mrefu na waziri kuniahidi katika bajeti hii niko tayari wananchi wamenunua redio mpya kusikiliza kauli ya serikali.

Nyumba ya Skuli ya Jambiani kwa muda mrefu imekuwa katika hali mbaya, inavujiwa na hata mwalimu anayeishi mule anahangaika uhamisho ili apate sehemu ya kujisitiri. Pamoja na Waziri kuahidi kulishughulikia suala hili kwa maandishi lakini bado hakuna hatua zilizochukuliwa.

Je, ni lini suala hili litachukuliwa hatua kulitatuwa kama waziri alivyoahidi kwa barua kuwa atalipatia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Waziria wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli tunafahamu ubovu wa nyumba ya skuli ya Jambiani kwa muda mrefu imekuwa katika hali mbaya. Wizara imeanza kulifanyia kazi suala hili kwa kupeleka waandisi wake kwa ajili ya kuikagua na kutathmini gharama za ukarabati wa nyumba hiyo. Nyumba hiyo inahitaji ukarabati wa paa kwa vile nyumba yote inavuja, plasta, sakafu na rangi. Makisio ya kazi hiyo yote imeshafanywa, ambayo ni kiasi cha shilingi milioni 10,721,185. Kazi hii ya ukarabati tutaizingatia katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 hali itakaporuhusu. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kukiri na kusema kweli, ndio hayo niliyosema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kakiri skuli hiyo inahitaji shilingi milioni 10, lakini hii ni bajeti ya pili Hansard zipo Mhe. Naibu Waziri, waziri kama yupo mwenyewe aliniahidi hapa nikiachie kifungu tutakwenda, nafikiri safari yenyewe ndio tunatambaa mpaka leo hatufiki.

Mhe. Spika, shilingi milioni 10,700,000 Mhe. Naibu Waziri kweli ni suala la kukaa mkafikiria hili. Unajua kuwa mwalimu anayekaa nyumba ile keshahamishwa na kwenda skuli nyengine, unalijua hilo. Nimpongeze Naibu Katibu Mkuu wa wizara yako Maalim Abdalla kwa jitihada aliyofanya katika sekta hiii.

Mhe. Spika: Swali lako Mhe. Jaku Hashim.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, shilingi milioni 10,700,000 mko tayari kwenda kukopeshwa mpaka mtakapozipata mkifika bajeti yenu ili kwenda kuijenga skuli ile ili kuiokoa hali ile.

Mhe. Naibu Waziria wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake kama ifuatavyo. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haiko tayari kukopeshwa kiasi hicho, kwa sababu ina uwezo wa kufanya.

Lakini pia naelewa kwamba mwalimu huyo amehamishiwa skuli ya Miwani Makunduchi, Mwalimu Abdu Haji wa Haji tunamuelewa mpaka jina lake ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa katika swali alililoulizwa. Lakini napenda nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba mwalimu yule sasa hivi pale keshaondoka kaelekea sehemu nyengine.

Je, hatuoni kwamba kuondoka kwa mwalimu yule kunarudisha nyuma ile juhudi au lile lengo ambalo alipelekewa pale kuhusiana na suala zima la uhaba wa walimu.

Mhe. Naibu Waziria wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika uhamisho ambao tumefanya tumezingatia kwamba skuli ya Jambiani pamoja na kumuhamisha mwalimu huyo haitaathirika katika usomeshaji. Kwa hivyo, usomeshaji utakwenda kama kawaida katika skuli hiyo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo anaonesha matumaini ya uendelezaji wa mikakati ya elimu nchini.

Mhe. Spika, pamoja na majibu hayo ukiwacha skuli ya Jambiani kuna nyumba nyingi za skuli zina hali mbaya sana ya majengo kwenye nyumba hizi za walimu. Naomba nikuulize swali kama hivi ifuatavyo. Ni nyumba ngapi na katika skuli gani za Unguja na Pemba ambazo wizara yako imezitengea bajeti katika kuzitengeneza katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, ahsante.

Mhe. Naibu Waziria wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe, swali lake kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nimueleweshe kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inamiliki nyumba 172, kati ya hizo nyumba 135 zinakalika na nyumba 37 ni mbovu ikiwemo pamoja na hiyo ya Jambiani. Sasa kwa mwaka huu tumepanga kuikarabati skuli ya Jambiani.

Nam. 130

Ulipaji wa Fidia kwa Waathirika wa Ajali Kazini

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kwa kuwa programu ya uratibu wa huduma za hifadhi ya jamii ilipanga kwa mwaka 2016/2017 kulipa fidia kwa watu 14 walioathirika kwa kupata ajali kazini.

(a) Je, Wizara imeweza kukamilisha ahadi ya kuwalipa waathirika hao na kama imeweza kulipa fidia hiyo, Unguja imelipa watu wangapi na Pemba wangapi.

(b) Je, katika waathirika wa ajali kazini, wanawake ni wangapi, Taasisi au Kampuni ambazo wakifanyia kazi na baada ya ajali hizo wana uwezo wa kufanya kazi sehemu nyengine kutokana na athari walizozipata.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha za fidia ambacho kimetolewa kwa waathirika hao wa ajali kazini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza naomba nianze kwa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye na yeye anaendelea kunipa pumzi zake na asubuhi hii nikaweza kusimama katika Baraza lako tukufu nikiwa katika afya njema.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu na kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, niweze kuwatakia Saumu njema Waislamu wote duniani, hususan wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba. Namuomba Mwenyezi Mungu atutakabalie Saumu zetu, tupendane na atupe riziki za halali.

Vile vile Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara na ampe afya njema na maisha marefu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nichukuwe nafasi hii kutoa mkono wa pole kwa familia ya Mzee Mkadara, mzee wetu wa chama ambaye leo hii ametangulia mbele ya haki. Nawaomba familia wawe na subra katika kipindi hiki kizito.

Baada ya salamu hizo Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 130 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, malipo ya fidia kwa waathirika yanafanywa kwa kutumia Sheria ya Namba 5 ya Mwaka 2005 ya Fidia. Malipo hayo yanawahusu Watumishi wa Umma waliopata ajali kazini.

(a) Mhe. Spika, ndiyo wizara imeweza kukamilisha ahadi ya kuwalipa waathirika hao. Jumla ya waathirika 22 wa ajali kazini waliweza kulipwa fidia zao. Kati ya hao Unguja waathirika Sita (6) na Pemba waathirika kumi na sita (16).

(b) Kati ya waathirika 22 waajali kazini niliyowataja katika jibu (a), wanawake ni saba (7). Taasisi au Kampuni ambazo wakifanyia kazi ni Wizara ya Afya; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Mahakama Kuu. Waathirika hao walipatiwa huduma za matibabu na wana uwezo wa kufanya kazi na wanaendelea kufanyakazi katika sehemu zao za kazi.

(c) Jumla ya Shilingi milioni 18,650,057 zilitumika kulipia fidia kwa waathirika hao wa ajali kazini. Unguja shilingi milioni 8,698,910/- na Pemba milioni 9,951,147/-. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali moja dogo dada Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri sana na ninampongeza kwa majibu yake yamenifurahisha nashukuru sana.

Lakini Mhe. Spika, kidogo niliona kwamba hapa zilizotajwa zimetajwa taasisi za serikali tu, sijaona kampuni za watu binafsi kutajwa kama nazo zililipa fidia.

a) Je, kwa kipindi hiki hizi kampuni hakuna taarifa yoyote kwamba kuna waathirika wa ajali kazi kwenye hizo sekta binafsi, hizo kampuni binafsi ambazo wafanyakazi wao wamepata hizo ajali.

b) Je, kwa sasa wizara ina mpango gani wa kuyafuatilia yale makampuni au haioni kwamba iko haja ya kuyafuatilia yale makampuni ya watu binafsi ili kuhakikisha kwamba wale watumishi wao au wafanyakazi wanaopata ajali kwenye makampuni yao wanawalipia fidia, ili na wao wapate kujisikia kidogo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kwa mataasisi ambayo wafanyakazi wake wamepata ajali kazini tunazo. Hivi sasa namwambia Mhe. Mwakilishi anistahamilie nitamjibu kwa maandishi idadi ile ya waathirika wa taasisi binafsi.

b) Kuhusu kufuatilia waathirika wa kazini katika taasisi binafsi, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu iko karibu sana na taasisi hii, na linapotokea suala hili basi wizara yangu inasimamia na kuhakikisha kwamba wale wote waliopata athari ile wanalipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri kwenye jibu mama alieleza kuwa, umewalipa waathirika 22 kwa Unguja na Pemba.

Je, mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 wizara yako imejipanga vipi ili kuweza kuwalipa waathirika hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwa mwaka 2017/2018 wizara yangu mpaka hivi sasa haijajua italipa fidia kwa waathirika wangapi, kwa sababu wizara yangu inapokea maombi kutoka taasisi mbali mbali za serikali, kwa hivyo sasa hivi ni mapema sana kuweza kujua kwa mwaka huu tutaweza kulipa waathirika wangapi.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kutokana na ugumu wa maisha unaopanda kila uchao. Je, Wizara yako haioni kuna haja ya kurekebisha sheria hii ya mwaka 2005, ili waathirika hawa kuweza kupata fidia iliyo nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza naomba nikiri kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli sheria hii imepitwa na wakati, iko haja ya kubadilisha sheria hii ili kulingana na wakati na matakwa yanavyokwenda. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 53

Kuchakaa Kwa Tangi la Maji la Unguja Ukuu

Mhe. Suleiman Sarahan Said: (Kny: Mhe. Simai Mohamed Said) - Aliuliza:-

Tangi la Maji la Unguja Ukuu ambalo limekuwa likitoa huduma kwa wananchi wa Uzi, Unguja Ukuu Kaepwani, Tindini, Kaebona pamoja na Kikungwi limechakaa na limeanza kuvuja.

Je Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha tangi hilo ambalo limeshapitwa na muda.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Tangi la Maji la Unguja Ukuu ni tangi la aina ya sandarusi ambalo ni miongoni mwa matangi ya muda mrefu ambayo kwa sasa yamechakaa na yanayovuja, wizara yangu inalifahamu vizuri jambo hilo na pia imejipangia utaratibu wa kuyafanyia matengenezo na kuyabadilisha kwa yale ambayo yameathirika sana.

Mhe. Spika, hivyo wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itaendelea na mpango wa kulifanyia matengenezo tangi hilo kwa kadiri ya hali itakavyoruhusu, kwa lengo la kuimarisha upatikanaji mzuri wa huduma za maji kwa wananchi wa Uzi, Unguja Ukuu Kae Pwani, Tindini, Kaebona pamoja na Kikungwi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba wakati ana mpango wa kuyafanyia matengenezo matangi hayo,

a) Je, haoni umuhimu wa pale kuweka tangi jipya ili isiwe usumbufu wa kuharibika siku hadi siku. Hilo ni swali (a)

b) Je, ni lini kutokana na kadhia inayowafika wananchi wale atalifanyia matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, serikali inaona umuhimu na kama nilivyokuwa nimesema kwamba kwa yale ambayo yanatengenezeka tunatengeneza, na yale ambayo yamechakaa na kuharibika sana tunafanya mapya, na tunafanya kwa awamu. Tulifanya pia Makunduchi, Nungwi na sehemu nyengine mapya. Kwa hivyo, kadiri hali itakavyokuwa inaruhusu basi tunakuwa tunabadilisha.

b) Kuhusu ni lini kwamba tutafanya hivi, ni kutokana na upatikanaji wa fedha. Kwa hivyo, hali itakapokuwa inaruhusu tunafanya kwa sababu ni kazi endelevu. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa (Kwaza): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Lakini nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ya wizara yake. Mhe. Spika, yapo matangi ambayo serikali imejenga katika maeneo tofauti, ikiwemo ndani ya Jimbo la Chumbuni pia lipo tangi ambalo mpaka sasa halijaungwa na kutoa huduma kwa wananchi.

Je, ni lini serikali itakamilisha uungaji wa matangi haya ili huduma ya maji iwe endelevu namaanisha kwa masaa 24 hasa katika Jimbo la Chumbuni na tangi ambalo nimekuwekea mfano.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishai na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Chumbuni lipo tangi hilo na ni matangi sita ambayo yalifadhiliwa na Ras al Khaimah mpango wake ni sambamba na uendelezaji wa vile visima vilivyochimbwa na Ras al Khaimah na zaidi upatikanaji wa fedha ndio unaotuelekea lini lifanyike, lakni tuna

dhamira ya dhati kumaliza visima vile pamoja na yale matangi kutumika.

Nam. 10

Ujenzi wa Barabara ya Wete – Konde na Wete – Gando Kupitia Mkopo wa *BADEA* na *Saudi Fund:*

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa katika muhtasari wa matumizi ya 2015/16 imeelezwa kwamba Serikali ilipata mkopo kutoka *Saudi Fund* na *BADEA* kwa jumla ya Tshs. 400 Bilioni na fedha za ndani 2.4 zilitengwa ni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Konde - Wete na Wete – Gando na kwa sababu barabara hizo zilishakamilika kwa kiwango kizuri sana na kwa sasa zinatumika, na kwa kuwa kuna taarifa kwamba Mjenzi wa barabara hizo bado hajakamilishiwa malipo yake ya mwisho.

(a) Je, ni kweli kwamba mjenzi huyo (*Kampuni ya MECCO*) hajamaliziwa malipo yake ya mwisho.

(b) Je, mkopo huo kutoka *BADEA* na *Saud Fund* utalipwa kwa muda gani.

(c) Kama mjenzi huyo hajakamilishiwa malipo yake ya mwisho ni lini Serikali itamalizia malipo ya awamu ya mwisho ili apewe kazi ya ujenzi wa barabara nyengine.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa *Kampuni ya MECCO* ambayo ndio mjenzi wa barabara hiyo bado hatujaweza kummalizia malipo yake ya mwisho kutokana na uhaba wa fedha unaotukabili.

(b) Mhe. Spika, mkopo wa deni hili unatakiwa kuanza kulipwa kuanzia mwaka 2013 na kukamilika mwaka 2037 na malipo hayo yatafanywa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ya *SMT*.

(c) Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar inalifatilia kwa karibu deni hilo ili kuhakikisha kwamba linalipwa.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kuuliza suali moja la nyongea.

Lakini Mhe. Spika, kabla ya kuuliza suali hili kwa ruhusa yako kwa faida ya wanamichezo naomba kuwapongeza sana vijana wetu wa *Jang'ombe Boys* kwa kushiriki katika mashindano ya *Sport Pesa* ingawa wametolewa katika mashindano haya kwa hivyo nawapa pole, lakini vile vile niwape pole Klabu yako ya Simba kwa kutolewa katika mashindano haya na nichukue fursa hii kuwapongeza wale wa kimataifa kwa kuendelea katika mashindano haya.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuuliza suali moja kama ifutavyo, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naipongeza sana Serikali kwa kuweza kuijenga barabara ile ya Wete/Konde na Wete/Gando kwa kiwango kikubwa na nichukue fursa hii kuipongeza sana kampuni ya *MECCO* kwa ujenzi mzuri wa barabara ile.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba *MECCO* wanadai na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Muungano wanaendelea kulifuatilia ili kulipa deni hili, na kwa kuwa kampuni ya *MECCO* wako tayari kuendelea na ujenzi wa barabara ya Wete/Chake-Chake kwa njia ya mkopo. Je, Waziri huoni kwamba ipo haja ya kuendelea kuwapa Kampuni hii ya *MECCO* kuijenga barabara ya Wete/Chake-Chake pia japo kwa njia ya mkopo ambayo tayari wamekubali.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, katika majibu ya suala hili ningependa kueleza tu kwamba unapotoa kazi za kujenga njia tuna utaratibu wetu na utaratibu huo ni kutoa zabuni. Sasa ikiwa kunatoka ushauri hapa kwamba ikiwa mkandarasi ameshajenga njia halafu tumuachie aendelee kujenga njia nyengine kwa mkopo itakuwa haina maana, itabidi tukiuke utaratibu na hatutaki kukiuka utaratibu wa kutoa zabuni, natumai hapo suala lako Mheshiiwa nimelijibu.

Lakini pia nilitaka nijibu hili swali lako la awali la kuhusu huu mkopo na mimi pia nitoe jibu la nyongeza kwamba katika kudai na kudaiana mwenye kujua anajua anachodai, lakini mwenye kudaiwa anawajibika kuangalia na kufanya uhakiki tujue tunadaiwa kiasi gani. Mpaka sasa hivi hatujakubaliana hasa na mkandarasi huyu kuhusu kiasi gani anatudai, yeye anadai fedha nyingi zaidi kuliko zile sisi ambao tunakiri na ni wajibu wetu kwenda kufanya uchunguzi na kuangalia hasa ni kiasi gani anachotudai nikishapata habari hiyo ambayo nimeshaagiza uchambuzi huo ufanywe. Nikishapata habari hiyo basi nitaishauri Serikali itoe kibali kipitie kwenye Wizara ya Fedha tuweze kuwalipa deni lao.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri pamoja na malipo ya mwisho kutokumlipa Mkandarasi huyu ama kampuni hii ya *MECCO*. Je, Wizara ina mpango gani wa kumlipa Mkandarasi huyu kufidia ukarabati na uharibifu uliojitokeza katika barabara ya Wete/Gando kabla ya kumalia malipo yake.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ningependa kumjibu Mhe. Muwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba tunapojenga njia tunapotoa mikataba ya kujenga njia tunamtaka mjengaji njia yaani mkandarasi aweke asilimia 5% ya gharama zote za ujenzi wa ile njia kama ni *bond* ya kuhakikisha kwamba baada ya kukabishi hii njia tunakuwa tunaiangalia kwa muda wa mwaka mmoja, kuangalia kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja hakuna tatizo na likitokea tatizo katika kipidi hicho cha mwakammoja basi tunakwenda tunamwita mkandarasi tunamwambia afanye matengenezo yanayostahili na tunatumia zile fedha asilimia 5% kwa mia kwa kulipia hizo gharama.

Kwenye hiiyo barabara ambayo ameitaja Mhe. Muwakilishi inasikitisha kuona kwamba kile kipindi cha mwaka mmoja kilipindukia, kwa hivyo ni vigumu sana kurejea tena kwa mkandarasi na kumwambia kwamba aende akatengeneze njia kwa sababu baada ya mwaka mmoja tulimrejeshea fedha zake na kwa sasa hivi kama kuna matengenezo yanayotakiwa kufanywa itabidi tufanye mkataba wa ziada ili aende akafanye hayo matengenezo. Wizara bado inafanya uchunguzi kuangalia kutokana na matatizo yaliyotokezea baada ya mvua hizi za masika tutaangalia baadae ni

kazi gani ambayo tunatakiwa kuifanya basi hapo ndio tutafanya maamuzi ya kuwaita hawa wakandarasi angalau tufanye mazungumzo nao na tuwakumbushe tu kwamba kazi waliyoifanya hawakuifanya kwa kile kiwango ambacho tulitegemea, basi tutawaomba na wao wachangie katika kufanya marekebisho.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena kwa kumuuliza Mhe. Waziri suala moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

Kwanza Mhe. Waziri katika majibu yako umekiri kuwa lipo deni ambalo mnalifanyia uhakiki katika utaratibu wa kutengeneza malipo, kwanza naishukuru Serikali kwa hatua hiyo. Lakini mara zote kwenye mikataba kuna sehemu ya makubaliano ya malipo na ukicherwa kulipa ndani yake kuna *interest.*

(a) Je, mkataba huu ambao haujalipwa mpaka sasa hivi kuna intrest ndani yake.

(b) Lakini kama ipo ni kiasi gani sasa kwa muda tuliochukua tutakabiliwa kulipa na *interest* hiyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Sikumbuki kwamba katika mikataba tunakuwa tunakubaliana kwamba tukichelewa kumlipa mkandarasi basi huwa tunamlipa pamoja na riba, hilo nitakwenda kulichunguza lakini kwa uelewa wangu mpaka hivi sasa ni kwamba ni kweli kama tunachelewa kumlipa inabidi tumlipe deni lake, lakini suala la riba halipo kwa sababu kama lipo suala la riba itabidi mkubaliane kile kiwango cha riba, kwa hivyo mimi silikumbuki lakini nakumbuka tu

kwamba kuna wakandarasi ambao walidai hawakulipwa kwa wakati muafaka kwa hivyo wanadai kwamba walipwe deni lao pamoja na riba.

Mimi hilo kama ni Waziri wa Wizara hii nililikataa na nina sababu zangu sababu zangu ni kwamba lazima tukubaliane tangu mwanzo kwamba ikiwa tunalipa deni pamoja na riba basi tuijue na hiyo riba ni ya kiwango gani na pia nikupe pia jibu la nyngeza la kwamba wapo wakandarasi waliokuwa wanafanya hizi kazi halafu wamechelewa kulipwa walitoka wenyewe wakenda kwenye mabenki wakachukua mikopo wakajilipa wenyewe zile fedha, halafu wakatuletea sisi deni la kusema kwamba tulikuwa tunakudaini shilingi 100 sisi tumekwenda kuzikopa kule mtulipe 112 kwa sababu hizi kumi na mbili ni riba, hilo nimelikataa kwa sababu utaratibu hauruhusu hilo.

KAULI YA SERIKALI

Kauli ya Serikali kuhusiana na Skuli ya Vikokotoni na Darajani katika Uendelezaji wa Ukanda wa Darajani *(Darajani Corridor)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais(Kny. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe.Spika: Mheshimiwa naomba uendelee kutoa kauli, Mhe. Jaku sijakuruhusu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais) Mhe. Spika, kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kutoa kauli ya Serikali

kuhusu hatima ya skuli ya Vikokotoni na Darajani katika uendelezaji wa ukanda wa Darajani *(Darajani Corridor).*

Mhe. Spika, wakati wa kujadili bajeti na kupitisha vifungu vya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar kulitokeza hoja za kuiomba Serikali kufikiria kubadilisha maamuzi ya kuivunja Skuli ya Vikokotoni wakati utakapoanza ujenzi wa uendelezaji ukanda wa Darajani *(Darajani Corridor)* ili kutunza historia ya majengo hayo. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume ambaye ni Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wakati akijibu hoja hizo aliahidi Baraza lako tukufu kuwa atalifikisha suala hili Serikalini kwa mashauriano zaidi.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa mashauriano haya yamefanyika Serikalini na maoni yaliyotolewa hapa yameonekana uzito wake, lakini ukilinganisha na faida ambayo itapatikana kutokana na mpango huo ambao ulipitishwa na Serikali na sasa unasubiri utekelezaji tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ni vyema kuendelea na maamuzi ambayo hapo awali yalishaamuliwa ambayo ni kuivunja Skuli ya Vikokotoni na kujenga majengo makubwa ya kibiashara. Skuli ya Darajani ambayo ndio ya kihistoria haitovunjwa bali itabadilishwa matumizi kuendana na mpango mpya wa matumizi ya eneo hilo. Wanafunzi wanaosoma katika skuli hizo watajengewa skuli mpya ya kisasa katika eneo la Rahaleo ambao ujenzi wa skuli hizo fedha zake zinapatikana kupitia mkopo wa *OPEC*.

Mhe. Spika, Serikali ina jukumu na kuwapatia watoto wetu sehemu ya kusomea ili wapate elimu kwani elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani, ndio maana Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Zanzibar anapata fursa ya kusoma katika mazingira mazuri na kuwapatia skuli bora na zenye

madarasa ya kutosha, madawati, vitabu na walimu waliohamasika kuwafundisha vijana wetu. Aidha, tangu Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 Sarikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Chama cha *Afro Shirazi Party* na sasa CCM moja katika vipaumbele vyake ni elimu. Kwa misingi hiyo ndio maana Serikali inajiandaa kuwapatia wanafunzi wa skuli hizo majengo mapya na ya kisasa ili waendelee na masomo kwa utulivu tofauti na eneo la Darajani ambako kuna vurumai za watu na kelele ambazo zinawaondolea wanafunzi na walimu utulivu wanaohitaji katika mazingira ya kujifunza.

Mhe. Spika, natumai suala hili limeeleka vyema na ni matumaini ya Serikali kuwa halitoibuka tena na nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tuunge mkono mipango ya Serikali ktika kubadili mji wetu wa Zanzibar ili uwe wa haiba nzuri na wa kuvutia, ili sisi wenyewe na wageni tuone fahari ya kuwa na mji wenye mpangilio bora wa majengo na shughuli zinazofanyika kwa utaratibu mzuri na kukuza biashara.

Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa Kanuni ya 43 kauli za Serikali na nitaisoma,

> 43(1) "Kiongozi wa shughuli za Serikali au Waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo Serikali inawajibika, na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anawez kutoa nafasi ya kutoa maoni ya kamati juu ya kauli hiyo".

(2) Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika, katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli ambao umewekwa na Kanuni ya 27.

(3) Hakutokuwepo na majadiliano yoyote kuhusu kauli yoyote inayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii, lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo kwa madhumuni ya kueleweshwa zaidi juu ya maelezo ya kauli hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe nimeona nikisome hiki lakini nina msisitizo hasa uko kwenye hii 43(3) kwa sababu nilipata ombi la mtu mmoja ambaye alitaka kuichangia hii kauli, lakini nisisitize kamba haichangiwi isipokuwa namruhusu aulize kwa ajili ya kupata ufafanuzi Mhe. Jaku sasa naomba nisikie kauli yako. Naam! Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa kutumia Kanuni hiyo hiyo 43(1) kama ulivyokwisha kuisoma labda niinukuu na mimi inasema:-

43(1) "Kiongozi wa Shughuli za Serikali au Waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo Serikali itawajibika, na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati anayehusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati juu kauli hiyo".

Mhe. Spika, Mwenyekiti wa Kamati ndio mimi na kamati inayohusika ni Kamati ya Mawasiliano na Ujezi ya Baraza la Wawakilishi kwa bahati mbaya sana inaonesha labda pengine Serikali ilipitikiwa haikuwahi kuleta hii hoja kwenye kamati ili na

sisi tukapata kuijadili, kwa sababu kamati inapojadili ndio inapunguza hiyo michango au majadiliano mengine. Sasa kanuni ya 43(1) imekiukwa.

Kwa hivyo nakuomba Mhe. Spika, kauli hii ya Serikali sasa hivi usiiruhusu kujibiwa au kuulizwa masuali ake mpaka iende kwenye kamati husika ijadiliwe halafu ili mwenyekiti au mjumbe yoyote atakayemruhusu kwa niaba ya kamati aje atoe maoni ya kamati halafu uwape ruhusa Wajumbe waweze kuuliza maswali. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na kuunga mkono kabisa kwa sababu ndio naunga mkono Kanuni tuziheshimu ilikuwa tuzifuate Kanuni na nilitegemea kauli hii ingekuwa imepita kwenye Kamati ili Kamati itoe maoni.

Sasa mimi nitakachoweza kufanya ni kumruhusu Mhe. Hamza kama una maoni yoyote kuhusiana na jambo hili kwa sababu najua unalielewa, kwa sababu mshalifanyia kazi kwenye Serikali naomba mtuache kidogo. Ni kama Mhe. Hamza unahisi una nafasi ya ili tuendelee kwa sababu tusirudishe ishakuja hii nikupe nafasi sasa kama Mwenyekiti wa Kamati ili uzungumze chochote kuhusiana na hii kauli baadae nitampa Mhe. Jaku aulize lile swali ninahusika. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, hoja niliyoizungumza sio hoja yangu ni hoja ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi na Mhe. Spika utaratibu huu sio mgeni na Kanuni hii sio iliyorekebishwa hivi karibuni ni Kanuni ambayo ipo muda mrefu tumeshaitumia muda mrefu kauli za Serikali zinakuja tunakwenda kuzijadili kwenye Kamati.

Mhe. Spika, ukisema mimi nichangie kwa niaba ya Kamati nitakuwa nachangia maoni yangu sio maoni ya Kamati. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba sana turuhusu Waheshimiwa Wajumbe tusimamie kanuni ambazo tulizozipitisha na Baraza hili linaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni, tukianza kuzigeuka Kanuni tutakuwa hatuendeshi Baraza la Wawakilishi, tutakuwa tunaendesha shughuli zetu za kawaida. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba ukae nimekuelewa pamoja na Kanuni hizi bado Spika ana *discretion* yake kwenye jambo hili, na nisingelipenda kulifanya liwe jambo kubwa kwa sababu jambo lenyewe ni dogo tu ni kosa lililofanyika awali, wakati wa uwasilishaji wa Bajeti limefanywa na Serikali na wenyewe wamekuja wamelirekebisha, tunakubaliana kwamba hawakufuata utaratibu wa Kanuni kwa kutokuja kuileta hiyo kwenye Kamati mimi sikuwa na fahamu hilo. Kwa fahamu yangu mie nipo hapa ni kwamba taratibu zote kwa mujibu wa Kanuni zimefatwa, kwa sababu sote ndio tunaotekeleza hizi Kanuni. Lakini lishakuja lishawasilishwa na wananchi wachalisikia na ni jambo ambalo linafahamika kabla mimi ningeshauri kama Spika tusiliendeleze hili. *(Makofi)*

Sasa hii hoja hasa mwenyewe iliyokuwa imemgusa zaidi ni ya Kamati lakini naibeba kama Spika, ili nimpe Mhe. Jaku aulize swali, sio achangie aulize swali ili Mhe. Waziri aweze kujibu kama Mhe. Jaku hana swali kwa sababu alileta kuomba kuchangia. Mimi naomba hili suala liishie hapa ili tuweze kuendelea na shughuli nyengine.

Mwanasheria Mkuu naomba kukusikiliza.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika nashukuru na sisi kutupa nafasi nimemsikia Mhe. Hamza nadhani Mhe. Hamza na yeye anataka kuila pilipili isomuwasha, maana hii si ya kwake Mhe.

Spika, hoja hii imetolewa mwanzo iliulizwa kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na tukajibu maswali hapa.

Na Ofisi hii inasimamiwa na Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali ambaye Mwenyekiti wake ni Mhe. Seif Omar Abeid wala sio Mhe. Hamza sasa kama kupewa nafasi apewe Mhe. Seif Omar Abeid wala sio Mhe. Hamza Hassan Juma kwa sababu hii sio Kamati yake, hii ni Kamati ya inayotoka kauli ya Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili Rais na aliyetoa kauli hiyo ni Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais. Makamo wa Pili wa Rais anasimamiwa na Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa ili kuondosha huu mzozo, mimi naomba kauli hii iyoondolewe irudi ifuate utaratibu, halafu ije tena baada kutekeleza masharti. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi Maji, Nishati na Mazingira kwa Mwaka wa 2017/2018

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji nilionao wako sita waliobaki kwenye hoja hii lakini tunakusudia hoja hii kuitimisha leo sasa mimi naomba, kwa wale ambao wameomba kuchangia washangie kwa maandishi kama wakati wanao wa kufanya hivyo, lakini sasa nitawapa nitawapa watu wawili nitampa kwanza Mhe. Mwanasheria Mkuu baada ya hapo nitampa Mhe. Naibu Waziri ili waanze kupihisha hii hoja. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Naam! Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika naomba kidogo na kubaliana na uwamuzi wako lakini kwa kuweka *hansard* sawa na kuweka taarifa ili Baraza lako Tukufu lielewe na wananchi watusikie ni kwamba utaratibu tumeufuata Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu anaelewa, kuhusu kauli yetu ya Serikali na yeye alikuwa tayari kutoa taarifa yoyote ambao kama angeweza kuitwa na Spika, kwa msingi huo nakubaliana na maamuzi yako lakini Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali kupitia kwa Mwenyekiti anayo taarifa ya kutosha. Ahsante sana Mhe. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa pendekezo la kwamba iende kwenye Kamati ya Mhe. Omar Seif Abeid imetolewa na Mwanasheria Mkuu na ndio maana nikasema kwa kuwa taratibu hazikutimika. Mimi naiondoa ili ikafute huo utaratibu, mimi nadhani hili tulimalize irudi kule ifuate utaratibu ni jambo lenyewe ni dogo miye wala sikuona haya ya kuwa na mvutano huu naomba mheshimu kiti kikitoa maamuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kusema machache juu ya hoja ambayo iko mezani ya Wizara ya Ardhi, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wetu Mtukufu kwa kutujaalia afya, uhai na mpaka siku ya leo tunaendelea vizuri tukiwa na afya ya katika kutimiza ibada yetu ya saumu ya kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Lakini ya pili nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa dada yangu Mhe. Waziri wa Ardhi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya yeye na Naibu wake Waziri pamoja na watendaji wake wote katika kusimamia sekta hii muhimu ambayo imesheheni mambo yote, imesheheni ardhi, imesheheni madini, imesheheni mazingira, imesheheni maji yote yale ambayo tunayahitaji yako kwenye sekta hii. Kwa hiyo, nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na niombe aendelee kuifanya kazi hiyo kwa kasi na nguvu zaidi, na tunamuahidi sisi wenziwe tutashirikiana naye kila wakati ambapo atahitaji ushirikiano wetu. Nichukue fursa hii kuzungumzia suala ambalo wengi wamelizungumzia suala la ardhi.

Kama ambavyo tunajua Mhe. Spika tarehe18 Mei, 1965 Baraza la Mapinduzi kupitia Sheria Nam.13 ya mwaka 1965 ilitangaza kuwa ardhi yote ya Zanzibar itakuwa ni Ardhi ya Serikali pamoja na kwamba Sheria hiyo ilikuwa ya mwaka 1965, lakini matumizi ya Sheria hiyo kwa mujibu wa Sheria ile yalianza tarehe 8 Machi, 1964. Kwa hivyo, miezi mitatu tu mara tu baada ya Mapinduzi Serikali ili-*declare* kwamba ardhi yote ya Zanzibar itakuwa ni Ardhi ya Serikali tokea tarehe 8 Machi, 1964.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Sheria hii ya mwaka 1965 ilifutwa na Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 ambayo inajulikana kwa jina la Sheria ya Matumizi ya Ardhi lakini dhamira na masharti yale yale ambayo yalikuwepo kwenye Sheria Nam. 13 ya mwaka 1965 bado yaliendelezwa kwenye Sheria Nam.12 ya mwaka 1992. Mhe. Spika, ukisoma Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 kuanzia kifungu cha 3 kinaelezea kwamba ardhi bado ni Ardhi mali ya Serikali, na msimamizi wa ardhi hiyo ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yeye kwa mujibu wa masharti haya ya vifungu vya tatu vya Sheria ndo amepewa Mamlaka na Sheria ya kusimamia ardhi ya Zanzibar kwa niaba ya wananchi.

Lakini Mhe. Spika, ukisoma kifungu hicho hicho cha tatu cha Sheria hiyo, Sheria imetoa Mamlaka kwa Rais kukasimu madaraka yake kwa Waziri mwenye dhamana ya ardhi na kwa sasa hivi dhamana hio amepewa dada yetu Bi. Salama ndio yeye anafanya kazi hiyo ya kusimamia ardhi kwa niaba ya Mhe. Rais sasa nimuombe sana sana sana kwamba ana dhamana ya Mhe. Rais ya kusimamia ardhi ya Zanzibar. Aisimamie bila ya woga asiogope kusimamia ardhi ambayo yeye amekasimiwa na Mhe. Rais kusimamia ardhi. Isimamie wala usiogope na utangaze vita kwa wale wote ambao wamekuwa madalali ndani ya ofisi yako na nje ya ofisi yako, uwatangazie vita kama sasa utaishughulikia ardhi ya Zanzibar na utaisimamia kwa mujibu wa Masharti ya Sheria.*(Makofi)*

Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 ndio awe rafiki yako huna haja ya rafiki mwengine rafiki yako ni Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992 ushakuwa naye huyo haya mengine yote ambayo wameyasema waheshimiwa wajumbe yote yatakupungia kwa sababu wewe utakuwa unafuata masharti yaliyoelezwa na Sheria, mengine yote haya yaliyosemwa yote yatapungua, lakini kwa sababu tumeacha kufuata masharti ya Sheria ndio maana haya mengine yote yanazungumzwa na waheshimiwa wajumbe.

Sasa nikuombe sana kama hii kwenye mkoba wako humo iwe ndiyo unatembea nayo, kila siku ukipata fursa unatizama na Sheria hii ndo imekupa mamlaka ya kutoa haki ya matumizi ya ardhi kwa mzanzibari na imekupa fursa ya kutoa *lease* kwa wageni pamoja na hayo yote lakini Sheria hii pia ndo imekupa, ukisoma kifungu cha 48 na ukisoma kifungu cha 55 imekupa pia uwezo wa kufuta hiyo *lease* na pia imekupa uwezo wa kufuta haki ya matumizi ya ardhi sasa usifute kwa sababu tu waheshimiwa wajumbe wamepiga kelele humu ndani, ufute kwa kufuata Sheria inavyosema. *(Makofi)*

Ufuate masharti ya Sheria, ukishafuata masharti ya Sheria huna tena ugomvi na mtu. Sasa nikuombe kwenye hili, Mhe. Waziri mengi haya yaliyosemwa yatakupungukia malalamiko mengi tu ili ufuate masharti ya Sheria hii. Sote tunajua Sheria imeeleza kama wale ambao wanatakiwa wapewe *ratio* na Serikali, Sheria imewapa wapewe ardhi mbili lakini Sheria haikumkataza mtu kununua mazao huko na akaja baadae akaomba apewe haki na matumizi ya ardhi. Sheria imeweka masharti kwamba kila Mzanzibari ana haki ya kupewa ardhi ya kilimo ya eka tatu, na ardhi mbili za ujenzi kupitia Serikalini, lakini haikumkataza mtu kupata maeneo mengine kama na yeye atafuata utaratibu.

Sasa nikuombe sana na katika kukusaidia hilo Baraza pia limekutungia Sheria ya Kamisheni ya Ardhi ambayo nayo ilifutwa na Sheria Nam. 12 ya mwaka 1992. Sasa Sheria hii ya Kamisheni ya Ardhi nayo pia ni msaidizi wako wale ambao wameteuliwa kuongoza Kamisheni hii Katibu Mtendaji na Bodi yote ya Kamisheni ya Ardhi nayo pia uwenayo karibu.

Lakini na wao lazima uwaambie kama wafate masharti ya Sheria. Mhe. Spika, si jambo la ajabu kama leo ardhi yetu sisi tunakaa tunasema ardhi mali ya Serikali lakini ukifungua kwenye *internet* unaona ardhi ya Zanzibar inauzwa tena kwa bei ya juu dola milioni mbili, dola milioni tatu ardhi hiyo hiyo ambayo mtu wake amepewa *lease* na Serikali halafu na sisi tumekaa bado tunapiga debe kama ardhi mali ya Serikali. Hatuwezi ikawa bado wanatoka watu nje kwa kivuli cha kwamba wanataka kuja kuwekeza kumbe wao wenyewe ni wababaishaji, wameshaona kama Zanzibar kuna ardhi ya bure, ukishapewa ardhi basi wewe ukishaitia kwenye *internet* baada ya muda wewe utapata fedha zako na ziada hayo yameshapitwa na wakati hatuko huko tena, lazima watu wajue kama hatuwakimbizi wawekezaji lakini pia hatukaribishi wababaishaji. *(Makofi)*

Hatuwezi tukakaribisha wababaishaji kwenye ardhi yetu ambayo tukiipima hata *square meter* elfu tatu haifiki ardhi hiyo hiyo tuzikane, ardhi hiyo hiyo tuchimbe mchanga, ardhi hiyo hiyo tuchimbe mawe lazima tuisimamie vizuri na usimamizi wake ni kupitia masharti ya Sheria. Sasa mimi nikuombe sana sana Mhe. Waziri kama baada ya waheshimiwa wajumbe na nawaomba wakupitishie bajeti hii yako lakini ukishakumaliza basi, uanze sasa kusimamia masharti ya Sheria wala huna haja ya kumuonea mtu. Katika Sheria katika jambo ambalo limewekewa Sheria nyingi Mhe. Spika ni eneo hili la ardhi. *(Makofi)*

Ardhi peke yake ya Zanzibar inasheria karibu nane ardhi tu, na imewekewa pia Mahkama yake *Land Tribunal* sasa hakuna wala sioni sababu kwa nini bado tunamizozo ya ardhi kwenye jambo ambalo usimamizi wake ni wakisheria. Sasa niwaombe sana Waheshimiwa wajumbe najua wengi wamezungumza, lakini yale yote ni katika kumsaidia Mhe. Waziri ili asimamie vizuri masharti ya Sheria, sasa niwaombe wale wote waliokuwa na dhamira ya kutunga ya kuuza Kamati Teule niwaombe sana wamuachie wampitishie Bajeti Mhe. Waziri ili akatekeleze masharti ya Katiba na masharti ya Sheria ili aweze kusimamia uzuri ardhi ya nchi yetu.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na niwaombe sana Waheshimiwa wote wamuunge mkono Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu sasa naomba nimwite Mhe. Juma Makungu Juma - Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ili akatoe mchango wake. Karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi asubuhi ya leo kutoa mchango wangu ikiwa ni sehemu ya kutoa ufafanuzi baadhi ya hoja za Wajumbe wako wa Baraza lako Tukufu juu ya Hotuba ya Wizara wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Naomba uniruhusu nianze kwa upande wa Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA).* Nianze na Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi alishauri Mradi wa Uimarishaji wa Miundo Mbinu ya Maji mjini unaofadhiliwa na India utekelezwe kwa wakati, lakini pia alisema visima vilivyochimbwa na Mradi wa Ras al Khaimah viendelezwe na kutoa huduma kwa wananchi, lakini kuwe na ulinzi wa vianzio vya maji kwa mshirikiano na Serikali za mitaa na pia kashauri kuharakisha mradi wa ubadilishaji wa miundo mbinu unaofadhiliwa na *ADF 12*, tuseme ushauri umepokelewa Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji tutaifanyia kazi yote yaliyoshauriwa ili kutoa huduma bora na endelevu ya maji safi na salama.

Pia alikuwepo Mhe. Masoud Abrahman Masoud alisema kwamba wananchi wa shehia ya Kizimbani hawafaidiki na huduma ya maji ni njia ya kuwa na visima vingi vya miradi mikubwa wa maji imechimbwa katika eneo hilo. Mhe. Spika ni kweli kuna mradi mkubwa wa maji ambao umechimbwa, umechimba visima katika eneo la Kizimbani kwa lengo la kupeleka maji katika matangi ya Welezo ambayo utatoa huduma kwa maeneo ya mjini hususan Mjimkongwe. Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba kila mradi una dhamira kuu kwa maeneo mahususi. Hivi kwa kuwa kizimbani ni eneo salama la maji imeonekana ni busara kuchimba kisima hata hivyo Mamlaka ya Maji imeibua mradi unaofadhiliwa na Serikali ya watu wa China ambao wanajenga miundombinu yake Miwani ambayo itaweza kuwapatia huduma wananchi wa Kizimbani. Hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi

kuwa na subra hadi mradi utakapomalizika unaotarajiwa kukamilika mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Abdalla Maulid Diwani alizungumzia kuhusu tatizo la maji bado lipo na hakubaliani kabisa na utapatikanaji wa kutumia maji uliyopo. Niseme kwamba huduma ya maji Zanzibar imeimarika kwa kiasi kikubwa ambapo serikali inaendelea kuchukua jitihada kupitia miradi mbali mbali ukiwemo mradi wa ufadhili wa *ADB*, India, *JICA*, kukamilika kwa miradi hii kuwasaidia kupunguza tatizo hilo.

Pia akataka kujua visima vingapi vya Ras al Khaimah vinafanya kazi. Tunamwambia kwamba visima 24 mpaka sasa tayari vinafanya kazi ikiwa 10 kwa upande wa Unguja na 14 kwa upande wa Pemba. Akataka kujua visima vingapi vya mradi wa China vinafanya kazi, mradi bado unaendelea na haujakamilika kwa kutoa huduma.

Mhe. Ali Suleiman Ali alizungumzia uendelezaji wa visima vya Ras al Khaimah vilivyokuwepo Tomondo, Magirisi na Kijitoupele. Nimwambie kupitia bajeti ya serikali ya mwaka 2017/18 visima hivyo tayari vimeshatengewa fedha za kuviendeleza.

Pia akasema kupatiwa wafanyakazi wa huduma atakaeshughulikia tatizo la maji katika Wilaya ya Madharibi 'A' na 'B'. Kwa heshima tunapenda kumjuilisha kwamba kuwa hivi sasa *ZAWA* tayari tumeshaweka Maafisa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba ikiwemo Wilaya ya Magharibi 'A' na 'B' ambao wahusika wanayafuatilia masuala ya maji kiujumla kwa wakati wote.

Lakini pia akaendelea kusema kwamba wananchi waliofungiwa mita za maji wanalalamikia utowaji wa bili za maji zenye madeni makubwa. Niwaambie kwamba *ZAWA* inaendelea na utaratibu wa

ufungaji na usomaji wa mita katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba. Sambamba na kufanyia marekebisho mita hizo katika maeneo ambayo huduma inapatikana vizuri.

Aidha katika kuweka utaratibu mzuri wa malipo kwa wateja. *ZAWA* inatumia bei maalum ambapo mteja aliyefungiwa mita analipia kwa mujibu wa matumizi yake tofauti na malipo yaliyokuwa yakilipiwa kwa mwezi kabla ya kufungiwa mita. Hivyo basi, Mamlaka ya Maji inawaomba wananchi kutumia maji kwa uwangalifu zaidi ili kupungufu upotevu usiowalazima ambao hupelekea ongezeko kubwa la bili za maji.

Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na Mhe. Ussi Yahya Haji walitaka kujua ukarabati wa matangi, tangi la Kama. Nimwambie kwamba Mamlaka ya Maji bado inaendelea na ukarabati wa tangi hilo na *inshaallah* ifikapo Septemba mwaka huu tunatarajia itakuwa limekamilika.

Mhe. Spika, wakataka kujua Ras al Khaimah ufanisi wake ni mdogo. Katika kuendeleza visima vya Ras al Khaimah serikali imepanga utaratibu maalum wa kuviendeleza ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzi bajeti ya 2017/18. Lakini wametushauri suala la maji ligatuliwe kwenda kwa wananchi. Niseme kwamba dhana ya ugatuzi ni suala la Kisera ambalo serikali limeanza kulifanyia kazi hatua kwa hatua na kwa upande wa maji serikali italizingatia na italifanyia kazi.

Likaja suala la kwamba ni kiasi gani za miradi zilizotumika katika Sekta ya Maji kuanzia mwaka 200 - 2017. Niseme jumla ya bilioni mia moja sabini na nane, milioni mia mbili hamsini na moja na laki nne (178,251,400,000) zimetumika kwa miradi ya maendeleo kwa maji safi na salama nchini ambako bilioni mia moja na sitini, milioni sita tisini na nane na laki nne (160,698,400,000) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na

bilioni kumi na saba, milioni mia tano na hamsini na tatu (17,553,000) ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mussa Foum alielezea matatizo ya maji Chole na Shehia ya Mtangani. Namwambia kwamba upungufu wa huduma ya maji katika kijiji cha Chole kinatokana na kisima wanachokitegemea cha Kengeja Skuli kuwa na watumiaji wengi. Hata hivyo, mamlaka ya maji imechimba kisima chengine katika maeneo ya matangi makongwe Kengeja, lakini bado hakijaungwa ili kukabiliana na upungufu huo. Kwa upande wa Mtangani kupitia mfuko wa Jimbo uchimbaji wa kisima unaendelea katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Mohamed Mgaza Jecha alitaka kujua hatua aliyofikia Wizara kupitia Mamlaka ya Maji juu ya ukarabati wa Tangi la Mtambile. Nimwambie kwamba ukarabati wa tangi hilo upo katika mpango wa fedha wa mwaka 2017/18.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Nassor Salim Ali, ambapo kwa ujumla walipongeza Mamlaka ya Maji kwa kupeleka maji Vijijini kupitia mradi wa Rasil-Hema na China na Mradi wa *ADF12* lakini pia walishauri kudhibiti mabomba ili kudhibiti cholera na wametunasihi au wamenasihi wananchi kulipia maji ili huduma iwe endelevu. Kwa ujumla niseme pongezi, ushauri na nasaha zimepokelewa serikali itazingatia na imeliingiza eneo hilo katika mradi wa *JICA*.

Mhe. Spika, pia walisema kwamba jitihada ndogo za ufungaji wa mita. *ZAWA* inaendelea na utaratibu wake wa kawaida wa ufungaji wa mita, aidha katika kuendeleza jitihada hizo imejiwekea siku ya Jumanne na Alkhamis kuwa ni siku maalum hadi sasa jumla ya mita elfu kumi zimeshafungwa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Rashid Makame Shamsi alielezea kuharibika kwa pampu ya kisima cha Binti Hamrani. Niseme kwamba ni kweli pampu na mota ya kisima cha Binti Hamrani imeharibika na Mamlaka imefanya jitihada za awali za kutengeneza pampu hiyo lakini pia imeagiza mota nyengine mpya ambayo tayari imeshafika na mafundi wanaifanyia majaribio mara tu baada ya kukamilika kwa majaribio hao pampu hiyo itarejeshwa na wananchi watapata huduma kama kawaida.

Mhe. Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kujua tatizo la maji Michamvi litakwisha lini. Jitihada mbali mbali imechukua katika suala la utatuzi na upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuanzia tayari visima vya Ras al Khaimah vimechimbwa na ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji tayari umekamilika. Hivyo, kukamilisha mradi huu tathmini imefanyika na jumla ya shilingi bilioni1.8 za Kitanzania zinahitajika. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imo katika hatua ya utafutaji wa fedha hizo kupitia vyanzo tofauti wakiwemo wahisani. Aidha, kwa kulitambua hilo serikali imeingiza katika mpango wa uendelezaji wa visima vya Ras al Khaimah ambao unatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed alitoa ushauri kuhusu uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme kwa mji mpya wa Tunguu. Ushauri umepokelewa. Lakini pia akapongeza kuhusu ugatuzi wa madaraka mikoani. Niseme ugatuzi kwa wizara yetu bali ni katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa vilivyo lakini pia pongezi tumezipokea.

Mhe. Mwantatu Mohammed Ussi, alipongeza sekta ya maji kwa kuwafanya kazi na kuakikisha wananchi wanapata maji yaliyosafi na salama. Nitoe pongezi kwamba zimepokelewa. Pia akashauri jitihada zifanyike za kuwapatia wananchi maji ziendelee. Niseme kwamba ushauri tunauchukua.

Mhe. Spika, kwa upande wa *ZAWA* nimalizie na Mhe. Ussi Yahya Haji, aliyesema kwamba kisima cha Moga kipatiwe umeme ili huduma ya maji safi ipatikane. Lakini pia na Kijiji cha Mlilile kilichopo katika Shehiya ya Matemwe Kusini ifaidike na huduma hii ya maji. Niseme kwamba kwa upande wa Mlilile kijiji hicho kitapatiwa maji kupitia miundombinu uliojengwa na mradi wa Matemwe ADB.

Mhe. Spika, niendelee kwa Shirika la Umeme la Zanzibar *(ZECO)* wa kwanza Mhe. Hamza Hassan Juma aliyesema kwamba Wizara ya Fedha ishauriwe kulipia moja kwa moja kwa Shirika la Umeme ankara za kila mwezi za taasisi za serikali ambazo hazitumii mita za TUKUZA. Lakini pia naomba niseme Wizara yangu imeupokea ushauri wa Kamati na itakaa pamoja na Wizara ya Fedha ili kurahisisa utekelezaji wa malipo ya ankara za taasisi hizo moja kwa moja kwa Shirika la Umeme badala ya fedha hizo kuingizwa katika *OC* za taasisi hizo.

Lakini pia alisema uongozi wa Shirika la Umeme uwe makini zaidi katika masuala ya manunuzi ili kudhibiti matumizi ya shirika. Tuseme ushauri wa Kamati tumeupokea na uongozi wa shirika utazidisha umakini katika manunuzi yote yanayofanyika pamoja na kuhakikisha kuwa vifaa vinavyonunuliwa kupitia manunuzi hayo vinakuwa na ubora unaokubalika.

Mhe. Spika, Mhe. Masoud Abrahman Masoud aliomba kupatiwa ufafanuzi wa deni la taasisi za serikali. Naomba nimwambie kwamba hadi kufikia mwezi wa April, 2017 taasisi za serikali zinadaiwa na Shirika la Umeme jumla ya Shilingi bilioni 25.35 ambapo deni la taasisi za SMZ ni shilingi bilioni 23.40 na taasisi za SMT ni shilingi bilioni 1.95.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani alisema kwamba Shirika limetumia gharama ya Tanzania milioni 140 kununua gari ambapo unununzi

huo haukufuata utaratibu za kisheria. Naomba nimwambie kwamba ununuzi wa gari hilo ulifanywa kwa kufuata taratibu zote kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma kupitia Zabuni Nam. ZECO/G/2015 -2016/11 iliyotangazwa katika gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 29/1/ 2016 na ufunguzi wake kufanyika tarehe 2/3/2016. Aidha, gharama ya gari hiyo ilikuwa ni shilingi milioni 105 na siyo milioni 140 kama alivyoainisha Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Spika, pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Mohamed Said Dimwa, alielezea wakatazi wa Tunguu anapoomba huduma ya umeme huwa wanashurutishwa kulipa gharama za shilingi laki tano (sh. 500,000) kama malipo ya shirika. Niseme katika kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia wananchi waliyopo katika maeneo ya makaazi mapya, shirika inajenga miundombinu ya umeme katika maeneo hayo kwa gharama zake. Hatua hiyo imeratibiwa kwa nia nzuri ya kuwaondoshea mzigo wa gharama wananchi hao ambapo wangelazimika kugharamia nguzo na vifaa vyengine ili huduma hiyoiwafikie hivyo kuna umuhimu wa kila mwananchi wa maeneo hayo kuchangia huduma ya kuungiwa umeme kwa viwango vilivyowekwa na Shirika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliendelea kusema kuna taarifa kuwa *ZECO* imenunua *transformer* nyingi kuliko mahitaji. Kadhia hiyo imepelekea *transformer* nyingi kubakia ghalani. Manunuzi yote ya vifaa vya umeme zikiwemo transformer yanafanywa kulingana na mahitaji ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Hivyo, *transformer* zilizopo ghalani zote zimepangwa kwa ajili ya kusambazia umeme maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na hoja ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Abdalla Ali Kombo ya kwamba kuna mafuta ya *IDO* yamekubaliwa kuuzwa kwa milioni 600 na badala yake yameuzwa kwa milioni 200. Napenda niseme kwamba mafuta ya

IDO yaliuzwa kwa mara ya kwanza kwa mnada wa hadhara ambapo mshindi aliyebarikiwa alishindwa kulipa fedha alizotaja. Hivyo, Shirika lililazimika kuitisha tena mnada kwa mara ya pili siku ya jumamosi ya tarehe 10/12/2016, kufuatia mnada huo wa mara ya pili mwananchi aliyebarikiwa alitakiwa kulipa shilingi milioni 244.96 ambapo fedha hizi zimeshalipwa.

Pia Mhe. Abdalla Maulid Diwani alielezea kwamba kuna mfanyakazi aliyetumikia shirika kwa kipindi cha miaka 25 lakini wakati wa kulipwa mafao yake alilipwa shilingi milioni mbili tu.

Mhe. Spika, mhusika ambaye anazungumziwa ni Mbarakati Hafidh aliajiriwa na Shirika la Umeme mnamo tarehe 1/10/1996 kipindi baina ya ajira yake na kuanza kazi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mwaka 1998, ndicho kipindi kinachoingia katika hesabu ya kiinua mgongo kinachopaswa kulipwa na Shirika la Umeme. Aidha, sehemu iliyobakia ya kiinua mgongo chake yamelipwa na *ZSSF* kutokana na michango iliyowasilishwa katika Mfuko huo hadi alipostaafu kazi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani aliendelea na kutaka kujua kwamba deni la *TANESCO* lilianza upya mnamo 2016 baada ya malipo yaliyofanyika kufuta deni lote lililokuwepo kwa wakati huo. Niseme kwamba malipo ya deni la *TANESCO* lililokuwepo hapo kabla lilipwa hadi kubakia shilingi bilioni 1.8 mnamo mwaka 2006. Hali hii ya deni lililokuwepo hivi sasa limetokana na deni ndogo ya kuzuia umeme inayotumiwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya *TANESCO* sambamba na taasisi za serikali kulipa ankara zake za matumizi ya umeme kwa *ZECO* kwa wakati.

Mhe. Ali Suleiman Ali alimuomba Mhe. Waziri afuatilie watendaji wa Shirika wasio waaminifu ambao wanasababisha usumbufu kwa wananchi.

Naomba kumjuilisha Mheshimiwa kwamba litafuatiliwa kwa kina suala hilo la watendaji na iwapo itabainika kuna watendaji wasiowaaminifu watachukuliwa hatua za kisheria kwa kushirikiana na bodi ya Wakurugenzi ya Shirika.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Machano Othman Said alishauri serikali kuanzisha wakala wa kusimamia usambazaji wa umeme vijijini kama ilivyo *REA* kwa upande wa Tanzania Bara. Niseme ushauri huo ni mzuri na umepokelewa na utafanyiwa kazi. Akaendelea kusema kwamba kujenga kituo cha kuuzia umeme katika maeneo ya Chuini kitakachohudumiwa wananchi wa maeneo ya Karibu ya Wilaya ya Magharibi 'A'.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kumwambia kwamba hivi sasa Shirika la Umeme tayari limeshampata wakala wa uuzaji umeme katika maeneo tofauti nchi nzima ambae ni *Max Malipo* inayotarajiwa kuanza kazi mwezi wa Agosti mwaka huu 2017. Hivyo, hakutokuwa na haja ya kuingia gharama za uwekaji wa vituo vya kuuzia umeme.

Nije kwa Mhe. Mussa Foum Mussa, alizungumzia baadhi ya vijiji vya jimbo la Kiwani vimo katika ahadi ya Mhe. Rais na kupatiwa umeme vijiji hivyo ni Mtondooni, Mtandafu na Mshamba. Niseme utarabu wa kuvifikishia umeme vijiji hivyo upo kama ulivyopangwa. Namuomba Mhe. Mwakilishi avute subra ndani ya mwaka wa fedha 2017/18 *inshaallah* vijiji hivyo vitafikishiwa umeme.

Mhe. Mohamed Said Mohamed alisema serikali haijapeleka umeme katika vijiji vya Tunguu/Uwandani na Kikungwi/Uwandani. Niseme awamu ya mwanzo ya upelekaji

umeme katika Kijiji cha Tunguu/Uwandani imekamilika na awamu ya pili inatarajia kuanza ndani ya mwezi wa Julai 2017. Aidha, kijiji cha Kikungwi uwandani kimo katika mpango wa upelekaji umeme kwa mwaka 2017/18....

Mhe. Spika naomba nimalizie kwa upande wa *ZECO* na badala yake nije nimwachie Mhe. Waziri aendelee na kilichobakia.

Mhe. Miraji Khamis Mussa alishauri *ZECO* kuongeza kasi ya kubadilisha mita zote za kawaida na kufunga Tukuza Shirika linaaendelea na mpango wake wa miaka miwili na kuziondoa mita zote za kawaida na kufunga Tukuza, jumla ya mita 122,515 zimeshafungwa na zilizobaki ni mita 35,161.

Kwa upande wa Mhe. Said Omar Said anasema kuna vijiji katika Jimbo la Wingwi bado havijapatiwa huduma ya umeme vijiji hivyo ni Mnazimmoja, Miyai na Chaguwani, niseme kwamba utaratibu wa kufikisha umeme katika vijiji hivyo upo kama ulivyopangwa na kama alivyoahidi Mhe. Waziri kwenye ziara.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi aliuliza kwa nini *ZECO* haikufikia lengo la ukusanyaji wa mapato ambapo makusanyo yamefikia asilimia 71 tu. Tumwambie kwamba makusanyo hayo yalikuwa ni ya kipindi cha miezi tisa tu ukilinganisha na makadirio yaliyoainishwa kwa mwaka mzima. Vile vile makadirio yamekusanywa hayajazingatia mabadiliko ya bei ambayo yakichelewa hadi mwezi wa Novemba, 2016 ilipoanza kutumika.

Lakini Mhe. Yussuf Hassan Iddi alisema kijiji cha Fuoni birikani kwa muda mrefu kimekosa umeme akauliza je, lini Shirika la Umeme linapeleka umeme katika kijiji hicho. Nimwambie kwamba Shirika la Umeme lina nia ya kusambaza umeme katika vijiji na maeneo yote ya Unguja na Pemba ikiwemo Fuoni

birikani. Hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi awe na subira wakati Shirika linaendelea na mpango wake huo.

Na mwisho ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu anasema kwamba Mhe. Waziri hivi sasa kuna madalali wa kupata umeme kwenye Shirika lako, ili wapate umeme kwa urahisi lazima wawaone madalali hao. Yeye anataka kujua Mhe. Waziri unalijua hilo. Niseme kwamba Wizara yangu haina taarifa za kuwepo za watu wa aina hiyo tena tunatoa wito kwa mtu yeyote mwenye taarifa za watu hao atuwasilishie ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao kwa vile suala la udalali wa umeme halikubaliki. Vile vile natoa wito kwa wananchi waende kwenye vituo vya kutoa huduma za kuungiwa umeme.

Mhe. Spika, baada ya hayo nikushukuru kwa kunipa nafasi kusema ambayo nimeyasema na naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Juma Makungu Juma, Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite mtoa hoja ili aweze sasa kuhitimisha hoja yake kwa kuja kutoa majumuisho. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira una muda usiozidi saa moja. Muda wako si zaidi ya saa moja Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa mara nyengine tena naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho ya hoja, michango na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakati wa kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ambayo imekuwa ikishirikiana nasi muda wote tangu tulipoanza matayarisho hadi kuwasilishwa kwa hotuba hii. Shukrani za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Wananchi jimbo la Shauri Moyo ambaye katika hotuba yake aliyoiwasilisha kwa ufasaha, ustadi, umahiri na umakini mkubwa. Napenda kuwahakikishia wajumbe wote wa Baraza hili na wananchi kwa ujumla kwamba michango na maoni waliyoitoa wajumbe wa Kamati na iliyochangiwa kwa pamoja tumeipokea, tunaithamini na Serikali kupitia Wizara yangu tunaahidi tutaifanyia kazi ipasavyo kwa mujibu wa Sheria, taratibu na miongozo tunayoipata kupitia Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, nawashukuru wajumbe wote waliochangia hotuba yangu moja kwa moja, kwa maandishi na wale wote waliokuwa hawakuchangia. Wajumbe wote mnaonekana kuifahamu vyema na kwa umakini hotuba yangu niliyowasilisha kwenu.

Mhe. Spika, mimi pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya watendaji wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira tunazipokea pongezi za dhati zilizotolewa takriban na Waheshimiwa wote waliochangia hotuba hii. Aidha, ushauri, maelekezo, miongozo, maswali na mapendekezo yote kwa pamoja yaliyotolewa tunaahidi kuyafanyia kazi ili kuongeza kasi ya kuwaletea wananchi maendeleo waliyoyatarajia.

Mhe. Spika, jumla ya Waheshimiwa 38 wa Baraza lako tukufu hili walichangia hotuba yangu. Waheshimiwa 23 walichangia moja kwa moja na 15 walichangia kwa maandishi. Kabla ya kutoa ufafanuzi wa hoja zilizowasilishwa, naomba nitumie fursa hii kuwatambua kwanza wajumbe wa Kamati ya Ardhi na

Mawasiliano, waliotoa msukumo mkubwa kwa michango yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe.Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Mjumbe
6. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
7. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu ambaye tunamshukuru sana kwa miongozo yake mbali mbali aliyokuwa akiitoa kwa Wajumbe.

Mhe. Spika, aidha, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa waliochangia moja kwa moja na kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Wajumbe waliochangia moja kwa moja ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano
2. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Machano Othman Said
6. Mhe. Mussa Foum Mussa
7. Mhe. Simai Mohammed Said
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Mohammed Said Mohammed
10. Mhe. Ali Khamis Bakari
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Abdalla Ali Kombo
13. Mhe. Rashid Bakari Shamsi
14. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu

15. Mhe. Miraji Khamis Mussa
16. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
17. Mhe. Said Omar Said
18. Mhe. Suleiman Sarahan Said
19. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
20. Mhe. Nassor Salim Ali
21. Mhe. Suleiman Makame Ali
22. Mhe. Mwanasheria Mkuu
23. Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Wajumbe waliochangia kwa maaandishi ni hawa wafuatao:-

1. Mhe Maudline Cyrus Castico
2. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
3. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
4. Mhe. Machano Othman Said
5. Mhe. Shaib Said Ali
6. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
7. Mhe. Ussi Yahya Haji
8. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
9. Mhe Abdalla Maulid Diwani
10. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
11. Mhe. Rashid Ali Juma
12. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo
13. Mhe. Dk. Makame Ali Ussi
14. Mhe. Omar Seif Abeid
15. Mhe. Shehe Hamad Mattar

Mhe. Spika, hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wakati wa kutoa michango yao ilijikita katika maeneo mbali mbali kama ilivyoainisha Kamati ya Ardhi na Mawasiliano yakiwemo maeneo makuu yafuatayo:-

1. Sekta ya Ardhi
2. Mamlaka ya Maji *(ZAWA)*

3. Shirika la Umeme *(ZECO)*
4. Mamlaka ya Udhibiti *(ZURA)*
5. Sekta ya Nishati
6. Sekta ya Mazingira

Mhe. Spika, Wizara yangu itaendelea kufanyakazi kwa mashirikiano ya pamoja na kamati mahiri ya Ardhi na Mawasiliano ambayo imetoa muongozo wa kutekeleza na kusimamia majukumu yetu ambayo imeonesha hakuna haja ya kuwepo kwa kamati teule ya Wajumbe wa Baraza hili. Kwa vile kazi hiyo itafanikishwa na kutekelezwa na wataalamu wenye uzalendo wa dhati tutakaowaidhinisha ili kuleta mabadiliko ya Wizara kwa muongozo, naomba niendelee kufanya kazi na Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na Wajumbe wa Baraza hili kuwa makini na ninamini kamati hii haijashindwa kufanya kazi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru kwa namna ya kipekee Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wa mzuri alioutoa ndani ya Baraza lako Tukufu kuhusu Utaratibu na Sheria za Ardhi zinazotuongoza naomba kumshukuru sana.

Mhe. Spika, naomba sasa kutoa ufafanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza nianze pia kumshukuru Naibu Waziri ambaye ameweza kutowa hoja kwa asilimia kubwa katika Mamlaka ya Maji na katika Sekta ya Umeme naomba niongeze kwa ujumla tu labda niseme dhamira ya Serikali katika kuwapatia wananchi wake huduma bora, huduma safi na salama ya maji safi na maji salama na pia kuwapatia huduma za umeme.

Dhamira ya Serikali ina nia njema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ana nia ya kuwahudumia wananchi wake ipasavyo na kila mmoja wetu anaona juhudi ambazo Mhe. Rais anazichukua katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata huduma bora ya maji safi na salama.

Vile vile Mheshimiwa naomba nizungumzie kidogo tu katika Sekta ya Ardhi ambayo wengi walichangia jumla ya watu 14 ambao ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma kwa niaba ya Kamati
2. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
5. Mhe. Simai Mohammed Said
6. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
7. Mhe. Mohamed Said Mohammed
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Abdalla Ali Kombo
10. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
11. Mhe. Suleiman Sarahan Said
12. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
13. Mhe. Shaib Said Ali
14. Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini

Niliamua niwataje kwa sababu nitatoa ufafanuzi kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa kuanza ufafanuzi Mwanasheria Mkuu aliutoa kwa kina sina haja ya kurejea yale ambayo yalikuwa yameshatolewa ufafanuzi ambayo kanuni na sheria zinatuongoza na sasa hivi tunahitaji kuzitelekeza. Lakini naomba tu niseme kidogo kwa kweli kuna maeneo ambayo baadhi ya watu wamepewa kweli maeneo makubwa naomba nikiri hili na kadhia

hii imetokea baina ya miaka minane na miaka kumi nyuma iliyopita kama vile hotuba ya Mwenyekiti alivyokuwa akizungumza kwamba Mawaziri kwa Mawaziri waliopita hotuba hii vilitokea vitu hivi kwa muda mrefu.

Lakini naomba Baraza lako Tukufu na wananchi wanaotusikiliza watuamini kwamba tunaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu taratibu zilizopo ili kadhia hizi ndogo ndogo zilizokuwepo basi tuziondoe. Vile vile naomba nikiri kwamba lile jengo la Mahkama ya Ardhi ni bovu lakini halipo katika hali nzuri hata kidogo, lakini Serikali kupitia Wizara yangu imeshalifanyia tathmini jengo hilo na hivi sasa inatafuta fedha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo makubwa.

Wizara yangu pia ilifanya kazi eneo la Dole Ndunduke ambapo kulikuwa na mgogoro wa wakulima katika eneo la Serikali na kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais utatuzi ulipatikana na wakulima hao walitambuliwa na kupewa vitambulisho maalum vya kuwakabidhi hati ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo. Vile vile naomba nitoe taarifa za ardhi kuwa zinabadilika kila baada ya miaka kumi na kwa sasa Wizara inaendelea na mradi wa kupiga picha za anga ambapo tutapata taarifa sahihi na kiraia ambazo tutazitumia katika kuandaa ramani mpya. Tunakubali kwamba kubadilika kwa maumbile ya ramani ya Visiwa vya Zanzibar na ndio maana kazi hii inafanyika.

Mhe. Spika, pia napenda kuwafahamisha Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na wananchi kwa jumla kuwa Bodi ya Uhaulishaji kawaida haitoi hati za ardhi isipokuwa huidhinisha uhaulishaji kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine. Tangu kuanzishwa Bodi ya Uhalishaji jumla ya vyeti vya uhaulishaji 4,123 vimetolewa na naomba niseme kwamba wizara yangu inachukua juhudi mbali mbali katika kuhakikisha kwamba yale

maeneo muhimu yote yaliyopimwa basi zile huduma za lazima zinafika kwa maana huduma ya maji na huduma ya umeme na hili tutaendelea kulifanya kila uwezo unapopatikana.

Lakini vile vile ni kweli ilikuja hoja kwamba kuna upimaji wa viwanja katika eneo la Vumawimbi Makangale naomba niseme ni kweli. Eneo la Vumawimbi Makangale tumelipima na kutokana na uzito wa kazi hiyo ilibidi tupige kambi na kufanya shughuli za upimaji kuanzia tarehe 20 mpaka 23 eneo hili lilipimwa kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa11:00 jioni. Upimaji huo ulifanyika baada ya kutolewa taarifa za kutosha kwa mamlaka za Serikali ikiwemo Shehia, Wilaya, Mkoa pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Pemba.

Naomba niliseme hili lilitokea baada ya mgogoro uliotokea huko nyuma na katika kutatua mgogoro na ziara niliyoifanya Pemba kwa wale tuliokuwa nao tarehe 6/3/2016 mwaka jana, mwaka huu tulikwenda Pemba tukafanya ziara ya pamoja tukimshirikisha Mshauri wa Rais Dkt. Mauwa Abeid Daftari, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Watendaji na Maafisa wa Wilaya, Watendaji na Maafisa Ardhi, Watendaji wa *ZIPA* na Watendaji wa Wizara ya Fedha. Tulikaa pamoja na kuangalia mgogoro ule tutautatuaje na mgogoro ule hautaweza kutatuka kama kwa pamoja hatutaweza kupima eneo lile na kukaa pamoja juu ya meza tukaweza kutatua ule mgogoro wakati tutakuwa na vipimo halali na vipimo halisi kufuatia amri ya mahkama iliyotolewa.

Vile vile kulikuwa na suala la ucheleweshwaji wa utolewaji wa hati naomba niseme sababu za ucheleweshaji wa kutoa hati ni ubadilishaji wa hati zilizopo. Wizara yangu ilifanya mapitio ya kina ya hali halisi ya utayarishaji wa utoaji, ubadilishaji, umiliki na usalama wa hati. Wizara ililazimika kufanya marekebisho hayo kwa lengo la kuwa na hati mpya ambazo zitakuwa vigumu

kughushiwa na wajanja, lazima tukubali hati tulizokuwa nazo sasa hivi wajanja wengi wanazighushi na migogoro mingi inatokea.

Zoezi hili la utoaji wa hati mpya litasaidia sana kuondoa migogoro ya ardhi na utapeli ulikuwa unafanywa na baadhi ya wananchi wetu na naomba niseme kwamba suala la ukodishaji wa ardhi na kwa nini wanalipishwa viwango vikubwa. Sheria ya Matumizi ya Ardhi inataka kuwa kila mwekezaji anakodishwa na kulipa kodi ya ardhi malipo ya kodi ya ardhi inategemea ukubwa wa eneo, sehemu husika na matumizi yaliyokusudiwa, ili kushajihisha wawekezaji wazalendo Serikali pia imewapa upendeleo maalum kuwawekea kiwango tofauti na wageni.

Mhe. Spika, katika suala zima la kujiimarisha katika ukusanyaji wa kodi Wizara iliendelea kufanya mapitio ya mfumo wa taratibu za ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Mapato Zanzibar ili viwango vya zamani vya kodi ya ardhi vinafanyiwa marekebisho ili viende sambamba na wakati uliopo. Aidha, kwa kushirikiana na wakala wetu *ZRB* tumeanzisha zoezi maalum la kuwabaini wawekezaji wote wasiolipa kodi.

Kuhusu eneo la Saateni kwa kushirikiana na Manispaa ya mjini Idara ya Mipango Mji imelipanga upya eneo la Saateni chini ya uratibu wa Manispaa ya Mjini utaratibu mzuri umepangwa na kutumika kuwahamasisha wafanyabiashara wote waliokodishwa katika eneo la Michenzani kwenda Saateni. Hata hivyo, jukumu la ugawaji wa maeneo kwa wafanyabiashara hao linaratibiwa na Manispaa ya Mjini.

Suala la kutayarisha Kituo cha Mabasi Kijangwani baada ya kufanya utafiti wa kina mpango wa matumizi ya Kituo cha Mabasi tayari umekamilika na kukabidhiwa Manispaa ya Mjini na hii lazima niseme tunafanya kazi kwa mashirikiano Wizara yangu na Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Eneo jipya la biashara lililotajwa katika ukurasa wa 21 para. "V" ni lipi ndani mpango mpya dani ya Mpango Mpya wa Kitovu cha Mji "**Ng'ambo Tuitakayo"** eneo lote la barabara kutoka Mkunazini mpaka Kariakoo litajengwa upya na viwanja 102 vilivyoainishwa katika jaduweli namba 1 ni viwanja vilivyopimwa na Serikali, bali ni viwanja vya wananchi walioomba kupimiwa maeneo yao sio viwanja vya kupewa vile ambavyo vinapimwa na taasisi yangu ya Kamisheni na kupewa watu. Na viwanja 54 vya huduma ni viwanja vile ambavyo maeneo ya maskuli ambayo yamepimwa na maeneo ya hospitali.

Kulikuwa na swali kwamba kuna mkakati gani wa kuweza kuendeleza Zoezi la Utambuzi na Usajili. Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi inaendelea na zoezi hili kwa mikakati miwili kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Sasa hivi tuna MKURABITA ambao watoa pesa kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo lakini pia tunatumia fedha za Serikali ili kuiweza kuongeza kasi ya zoezi la utambuzi na usajili.

Sitorejea maswali ambayo tayari tushayajibu lakini pia kulikuwa na swali ya ujenzi kiholela ambayo ndugu yangu wakwezi na wakulima Mhe. Hassan Khamis Hafidh alilizungumza tuchukuwe maamuzi magumu, nakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi juu ya hali ya ujenzi holela nataka nimuhakikishe kuwa Serikali kupitia Wizara yangu tayari limeshachukua hatua swali hili.

Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara Tawala la Mikoa tumeunda Kamati Usimamizi na Udhibiti Ujenzi *(DCU)* ambayo imeshaanza kuthibiti suala la ujenzi holela. Kwa hivi sasa watu wanashajihishwa kwenda kukata vibali na kupekeka michoro na wale wasiofanya hatua za kisheria zinachukiliwa.

Lakini hili naomba niombe sana kupitia Baraza lako Tukufu Mhe. Spika na naomba Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane kwa pamoja na wananchi wanaotusikiliza waweze kusikia kwamba waheshimiwa mara nyingi tunapochukua maamuzi magumu, basi Waheshimiwa mnakuwa wakali.

Niwaombe sana katika hili, kwa sababu Mhe. Mkuu wa Mkoa alifanya kazi kwa dhamira njema katika Mkoa wa Mjini kwa sababu hivyo hivyo ya kufanya maamuzi magumu na kukabiliana na changamoto ambazo zilizopo. Sote tulishuhudia kila mmoja alikuwepo, na katika hili naomba pia niseme kwamba kama tunaona kuna uvunjifu wa sheria na taratibu za ujenzi katika maeneo, tunaomba sisi ndio wananchi lakini sisi ndio tumo ndani ya mitaa yetu na maeneo yetu, basi tunaomba sana tuweze kutoa taarifa mapema. Naomba nitoe wito kwa wananchi, lakini naomba pia nitoe wito kwa viongozi kama tunaona kuna jambo linaharibika katika maeneo yetu, tunaomba tusibiri mpaka lishafikia kiwango kikubwa tuanze kulitatua mapema zaidi.

Mhe. Spika, katika kuwasaidia wakaazi kwenye fukwe serikali kupitia wizara yangu imeanza mchakato wa kupitia mpango wa utalii wa mwaka1995. Kazi ya awali inafanywa katika shehia sita kuanzia Marumbi mpaka Mbuyutende, ndani ya eneo hili la kilomita 40 utafanywa mpango mpya ambao utatoa kipaumbele kwa wakaazi, huduma na biashara. Mapungufu yote yaliyojitokeza katika mpango wa 1995 yatarekebishwa na ripoti ya awali ya kazi hii itapatikana katika robo ya pili ya bajeti ya mwaka huu wa 2017/2018.

Mhe. Spika, lakini vile vile kazi hii itafanywa katika eneo la Pemba kwenye fukwe ya Makangale na Wambaa.

Halafu kulikuwa kuna suali la kufutwa *lease* za Tibirinzi. Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa eneo hilo kwa

sasa linapangwa kwa matumizi ya ujenzi wa ofisi za serikali kama vile *ZURA* na *ZECO* na halijatolewa *lease* kwa mtu yeyote. Aidha, wizara yangu tayari imeshaanza mchakato wa utengenezaji wa *Master Plan* ya Mji wa Chake-Chake. Matunda ya mpango huu ni kuyatenga upya maeneo yote ya wazi, maeneo ya michezo na maeneo ya kupumzikia. Sambamba na Pemba eneo la Chake-Chake naomba pia kuzungumzia maeneo ya kupumzikia katika maeneo ya Ng'ambu ambayo sasa hivi kwa Unguja tuna eneo moja tu la Forodhani.

Wizara yangu imeupokea ushauri mzuri wa Mhe Mwakilishi juu ya umuhimu wa kupanga maeneo ya kupumzikia lakini kwa sasa hivi kwa Unguja tayari kazi hii ishaanzwa kuna maeneo makubwa matatu. Kuna eneo la Kiembesamaki, eneo la Kibanda Maiti na eneo la Daraja Bovu. Na kwa sababu wizara yangu ina nia thabiti na inataka maeneo ya kupumzikia yawe mengi, wizara yangu kupitia *DCU* tayari wametoa milioni 50,000,000 katika makusanyo yale ambayo wanayapata katika Halmashauri, Manispaa ya Magharibi "A" ili waweze kujenga eneo la Kiembesamaki. Kwa hiyo, sasa hivi tunasubiri utekelezaji kutoka Magharibi "A".

Suala la eka ngapi ambazo hadi sasa zimerejeshwa serikalini na watu kwa imani zao. Napenda kuwajulisha waheshimiwa, kwa sasa hakuna mwananchi aliyerejesha eka 3 kwa njia ya imani yake. Aidha, kwa upande wa Pemba eka zipo chini ya Wizara ya Kilimo ambayo ndio inayohusika na utaratibu wa ugawaji.

Vile vile kulikuwa kuna suali la kulijua eneo la uwekezaji la Fumba na lipi la wananchi. Naomba kusema kwamba wakati mwaka 1992, wakati linatolewa tamko la *declaration* ya *EPZ* basi jumla ya hekta 600 zilitengwa kwa ajili ya uwekezaji na eneo jengine lote lililobaki ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimalize hili la ardhi kwa hiyo nimekuwa nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano yenu ya pamoja ili tuondoshe changamoto hizi na kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo ambayo tunayo na sheria ambazo tulizozipitisha ndani ya Baraza hili naomba tushirikiane kuhakikisha kwamba kazi hii tunaifanya kwa pamoja. Changamoto hizi hatutoweza kuzisimamia kama sisi wenyewe tukiwa hatupo pamoja na hatutoweza kufanya kazi kwa pamoja. Niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi tukiwa mitaani kwetu sote tufanye kazi kwa pamoja kama Mwanasheria Mkuu alivyosema, ardhi hii ni mali ya serikali na msimamizi mkuu ni Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa hiyo, naomba tuilinde, tuihifadhi na tuweze kuitumia vizuri.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa niende moja kwa moja kutoa ufafanuzi katika Idara ya Nishati. Kuna wachangiaji ambao walichangia katika idara hii ni Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Simai Mohammed Said. Katika hili walizungumzia sana hoja za Shirika na Idara ya Nishati na Madini katika matumizi ya nishati mbadala.

Mhe. Spika, kusema kweli ushauri wao tumeupokea na kwa sasa naomba niseme taasisi hizi mbili, Shirika la Umeme na Nishati wanafanya kazi kwa mashirikiano makubwa na wafanyakazi kwa pamoja. Na sasa hivi tuna utafiti wa jua na upepo ambao unafanywa na nchi za Umoja wa Ulaya *(EU)* na inatarajiwa ripoti inayohusiana na mradi huu iwasilishe Agosti mwaka huu. Kwa hiyo, tutajua tumefikia wapi na ule uchambuzi wa zile data tutajua tunafanyaje, lakini katika taarifa yangu wakati naisoma niliisema sana hii kwamba Kampuni ya *Inter Global* ya Ujerumani ndio sasa hivi inafanyia kazi mradi huo, na unatarajiwa kumalizika kabisa mwaka 2018.

Lakini pia ilitaka kujulikana gharama za utafiti wa mradi huu. Mradi huu umepata ufadhili kutoka Jumuiya za Ulaya ambazo ni Euro milioni tatu ziliweza kutumika.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la azma ya serikali baada ya kumalizika kwa utafiti huo mapendekezo yatakayotolewa kutokana na utafiti wa mradi huo serikali itazifanyia kazi kuhakikisha kuwa Zanzibar inaneemeka katika nyanja za nishati mbadala ili kuboresha hali za wananchi wake kwa kupatikana nishati ya bei nafuu na ya uhakika kama mapitio yanayoendelea ya sera ya nishati ya 2009 yanavyoelekeza.

Mhe. Spika, katika kuendeleza hili pia kulikuwa kuna suala zima tumefikia wapi baada ya kuundwa *ZPRA*, Mamlaka ya Udhibiti na Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

Mhe. Spika, baada ya kuundwa Mamlaka ya Udhibiti na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Zanzibar, mnamo Machi mwaka huu wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mamlaka hiyo imeanza mazungumzo ya kupitia kitalu cha *Pemba-Zanzibar Basin* unaojulikana kama *Antrim PSA*. Kama ilivyotakiwa na sheria Nam. 6 ambayo tumeipitisha hapa Barazani ya 2016 ya mafuta na gesi asilia. Baada ya kumalizika mazungumzo hayo serikali itaendelea kupitia mikataba mengine iliyoko eneo la Zanzibar. Lakini vile vile Mamlaka tayari imeanza mchakato wa kutunza baadhi ya miongozo muhimu kwa ajili ya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Utungaji wa miongozo hiyo upo katika hatua nzuri.

Mhe. Spika, vile vile walitaka kujua makampuni mangapi yalikuja hapa Zanzibar yaliyojitokeza na kama yameshapewa kibali. Wako wawekezaji wengi ambao tayari wameshaanza kuonesha nia ya kuja kuekeza katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta

na gesi asilia Zanzibar. Kwa mfano, kuna *SHELL, RAKGAS* na *CNOOC* na wako wengine pia. Hata hivyo, kipaumbele cha serikali kwa sasa ni kumaliza mazungumzo *negotiation* ya mapitio ya mikataba iliyokwisha sainiwa kabla ya sheria yetu kupitishwa. Mazungumzo hayo yatakapokamilisha leseni za utafutaji zitatolewa kwa mujibu wa sheria, ama kwa wawekezaji wapya sheria ya utafutaji wa gesi asilia ya Zanzibar imeweka utaratibu wa zabuni (*tendering*) kwa makampuni hayo, na muda muafaka ukifika serikali itaweza kutangaza zabuni hizo.

Mhe. Spika, vile vile majibu ya utafiti uliofanywa na ndege *Full Tensor Gravity Survey (FTG*) bado yanaendelewa kufanyiwa tafsiri na Kampuni ya *Belgiospace* kutoka kwenye tarakimu na hatimae kuwa taarifa. Baadae taarifa hiyo zinafanyiwa uchambuzi wa pamoja baina ya Kampuni ya *Belgiospace*, *RAKGAS* na Mamlaka yetu ya *ZPRA* ili kuchagua maeneo ya kuendesha Utafiti wa Mtetemo (*Seismic Survey*). Naomba niwakumbushe Wajumbe wa Baraza hili tukufu na wananchi kwa jumla kuwa utafiti wa ndege hautoi majibu kuwa mafuta yapo wala mahali yalipo. Utafiti huwa unatuonesha maeneo ambayo miamba ya kuhifadhia mafuta inapoweza kupatikana kwa ajili ya kufanya utafiti na mitetemo.

Mhe. Spika, vile vile Mamlaka imejipanga vizuri katika kutoa uelewa kwa wananchi. *ZPRA* ilianza na programu ya kutoa walimu kwa wananchi kufanya semina mbali mbali lakini pia kutayarisha vipindi vya redio mbali mbali, lakini pia kwenda katika maskuli na kuweza kukutana katika skuli za sekondari kutoa elimu pamoja na vyuo. Na Mamlaka itaendelea na zoezi la kutoa elimu kwa Masheha, Madiwani wote wa Unguja na Pemba, Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, viongozi na wanachama kwa ujumla kwa kupitia mikutano na vyombo vya habari mbali mbali.

Ulitolewa ushauri kwamba *ZPRA* wawezeshwe kuhudhuria mikutano na mafunzo. Ushauri tumeupokea na tayari tumeshaanza kulifanyia kazi jambo hili kwa ajili ya kutafsiri tafiti zote za mafuta na gesi asilia na sio mitetemo peke yake. Kwa hiyo, sasa hivi tumelifanyia kazi na wanaweza kuhudhuria na wengine wamekwenda masomoni.

Pia suala la kuwa wawazi katika kutoa taarifa, suali hili tumelipokea na tushaanza kulifanyia kazi na tutaendelea kutoa taarifa za mafuta na gesi asilia kila pale matokeo yanapojitokeza. Hili tumelipokea naomba tushirikiane kwa pamoja tuweze kuelimisha wananchi wetu.

Vile vile kulikuwa kuna suala la kuharakisha uchimbaji wa mafuta ili wananchi wafaidike. Ushauri ule niliupokea ila ni muhimu kufahamu kuwa kabla ya shughuli za uchimbaji wa mafuta kuanza lazima kufanywe tafiti za awali, zifanywe na mafuta yagundulikane. Naomba niwafahamishe wananchi kuwa fursa za ajira zitapatikana hata katika hatua ya utafiti. Hivyo, wananchi wachangamkie fursa hizo mara tu zinapotangazwa.

Mhe. Spika, na suali la uanzishwaji wa Kampuni ya Taifa ya Mafuta na Gesi Asilia *(ZPDC)* wamefikia wapi. Serikali iko katika hatua za mwisho za usajili wa uanzishwaji wa Kampuni yetu ya Mafuta na Gesi Asilia *(ZPDC)*. Rasimu ya Uanzishwaji (*Memorandum and Articles of Association*) ya Kampuni hiyo iko katika hatua za mwisho, tunawaomba wananchi wawe na uvumilivu wakati serikali inakamilisha taratibu za uanzishwaji wake.

Pia ulitolewa ushauri wa kujengwa Kiwanda cha Kusafishia Mafuta tukianza uzalishaji. Ushauri tumeupokea na wakati ukifika hatua muafaka zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ndani ya sheria yetu, na pia kujenga chumba cha

kuhifadhia taarifa. Mamlaka tayari imeshaajiri Mkandarasi kwa ajili ya kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi ya Mamlaka liliopo Forodhani. Chumba cha kuhifadhia taarifa hizo kwa muda na chumba cha kuangalia taarifa zimeshatengwa kwa ajili ya kazi hizo na kwa sasa matengenezo ya awali yameanza kufanyika.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba pia wajumbe walichangia katika suala zima la *ZURA*. Naomba pia niseme pongezi nyingi zilitolewa na pongezi hizi tumezipokea, lakini suali la mashine nyingi kuwa hazipimi mafuta kwa ufanisi wizara kupitia *ZURA* imekuwa ikisimamia kwa karibu sana zoezi hili la kupita na kuangalia mezani na vipimo na kukagua mashine zote ili kupima ubora na utendaji wake. Zoezi hili limekamilika mwezi wa April, 2017 na ni endelevu kila inapotokea haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, pia kulikuwa suala hatua gani tumechukua ya kuliendeleza eneo la Mangapwani. Eneo la Mangapwani tayari limeshatangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali kuwa ni eneo la uwekezaji wa mafuta na gesi. Wizara yangu inaendelea na kazi ya kulipima ili kulipangilia kitaalamu na jumla ya hekta 380 tayari ziko pale, wawekezaji 6 wamejitokeza kwa nia ya kuekeza eneo hilo. Kuna Singapore, *Inter Capital* (Tanzania), *PUMA* (Tanzania), *Frontier Group* Singapore, China na Hong Kong, Njake Enterprise (Tanzania) na *ASG (Poland*).

Mhe. Spika, hatua zilizofikia kwa ujenzi wa Ofisi za *ZURA*. Wizara imeipatia Mamlaka eneo la Maisara kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo ya ofisi. Mjenzi elekezi ameshachaguliwa, kazi ya kutayarisha michoro ya ujenzi na tenda ili kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi wa jengo zinaendelea.

Mhe. Spika, lakini pia kulikuwa kuna suali hivi kwa nini bei ya mafuta ya dizeli, petrol na kerosene ziwe juu hapa Zanzibar ukilingalisha na wenzetu wa Tanzania Bara. Ni kwamba mafuta

yanayoletwa Zanzibar yanapitia bandari ya Dar es Salaam hivyo kunaongezeko la gharama ya usafirishaji kutoka Tanzania Bara yanotozwa gharama za *TBS*, gharama za kuyahifadhi, gharama za upakiaji wa Tanzania Bara na yakifika Zanzibar pia yanatozwa ushuru wa forodha hii ndio sababu kubwa ya bei za mafuta Zanzibar kuwa juu. Hata hivyo, mafuta ya taa yapo chini kulinganisha na Tanzania Bara.

Mhe. Spika, pia kulikuwa kuna suala kwamba hali ilivyo hivi sasa imesababisha suala la magendo na tunadhibiti vipi magendo.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*ZURA*) na Kamati za Ulinzi na Usalama Wilaya na Mikoa imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kupambana na mafuta ya magendo kama vile kufanya doria katika sehemu mbalimbali ambazo biashara hii inasemekana imeshamiri. Hata hivyo, katika kupambana na tatizo hilo, wizara yangu kupitia *ZURA* imetafuta kampuni ya kuyawekea alama mafuta yanayoingizwa Zanzibar kisheria ili kuweza kubaini yale yalioingizwa kimagendo. Hali ambayo tunatarajia itasaidia kwa kiasi kikubwa kuondosha kabisa tatizo hili.
Mhe. Spika, vile vile kulikuwa kuna suala kwamba bei ya mafuta ikipanda inapandishwa haraka na wamiliki wa vituo, lakini inaposhuka wanachelewa sana kuishusha.

Wizara yangu kupitia *ZURA* inahakikisha kuwa bei inaposhuka basi vituo vyote vinashusha bei kwa kufanyiwa ukaguzi, hivyo tunashauri inapotokezea kuwepo kwa kituo ambacho bei imeshuka lakini bado haikushushwa basi taarifa iletwe *ZURA* kwani hilo ni kosa kulingana na kanuni za usimamizi wa vituo vya kuuzia mafuta.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pia naomba niendelee kwenye sekta ya mazingira. Hoja zilitolewa na wajumbe Mhe. Hamza Hassan

Juma, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Shaib Said Ali. Hoja zilizotolewa walishauri sana wizara kutafuta jengo jengine kwa ajili ya jengo la mazingira.

Mhe. Spika, kusema kweli wizara inakiri kuwa Jengo la Sekta ya Mazingira ambalo linatumiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (*ZEMA*) ni dogo mno ambalo linatumiwa na Mamlaka lakini pia linatumiwa na idara kulinganisha na idadi ya wafanyakazi na majukumu ya taasisi hizi mbili. Lakinipia nakiri kwamba haipendezi baina ya mabosi wawili kukaa katika eneo moja, lakini kutokana na hali hiyo wizara yangu imeanza mazungumzo sasa hivi na Wizara ya Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili kuruhusu sehemu iliopo ofisi ya kilimo pale nyuma yake kupimwa na kupatiwa Sekta ya Mazingira ili waweze kujenga jengo lao.

Mhe. Spika, vile vile kulikuwa kuna suala la kusema nyumba 80 za wananchi wa Jimbo la Mtoni zinaingia maji ya bahari kutokana na mradi mkubwa unaoendelea katika eneo la *Mtoni Marine*.

Mimi binafsi mnamo tarehe 02/06/2017 nilikwenda katika eneo hilo na baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri tulifanya ziara ya kukagua eneo la ukanda wa Pwani ya Mtoni ili kuona hali halisi ilivyo. Aidha, tarehe 03/06/2017 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pia alifanya ziara ya eneo la Pwani ya Mtoni kusikiliza malalamiko ya wananchi wa sehemu hiyo kufuatia maji ya bahari kuvamia maeneo yao. Kufuatia ziara hiyo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameagiza taasisi zote zinazohusiana na usimamizi wa mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi ‘A’ na wananchi pamoja na Muwekezaji wa Mradi wa Hoteli ya *Mtoni Marine* kukaa pamoja ili kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo la athari ya maji ya bahari yanayolikumba eneo hilo.

Lakini vile vile naomba nitoe wito hapa mikoko pale mingi imekatwa lakini shughuli za wananchi pale zimekuwa kubwa, pia inasababisha kusogeza kwa maji kuja juu. Hivyo niombe tu wananchi washajihike katika kupanda mikoko kwenye lile hasa tukizingatia wiki hii tunayokwenda nayo ni wiki ya mazingira toka tarehe 5 tumeanza nayo. Kwa hiyo, naamini hatua hiyo ni nzuri na itatoa muelekeo mzuri wa pamoja utakaoepusha migogoro kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili ile ya muwekezaji pamoja na wananchi wa eneo la pwani ya Mtoni.

Mhe. Spika, pia kulikuwa kuna suala la mmong'onyoko wa udongo katika skuli ya Faraja kutokana na maji ya mvua. Kwa ajili ya kuangalia hatua muafaka zinazofaa kuchukuliwa kwenye eneo hilo ili kunusuru skuli hiyo, wizara yangu inaunga mkono pendekezo lililotolewa na Mhe. Mwakilishi la kwenda na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa siku ambayo Mhe. Mwakilishi ataona inafaa. Aidha, katika ziara hiyo ni vyema ikashirikisha pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kufanya mazungumzo ya pamoja juu ya mapendekezo yatakayotolewa.

Mhe. Spika, suala la kujenga ukuta katika eneo la Kilimani kulikuwa kuna swali utajengwa lini.

Naomba nitoe taarifa kwamba mkandarasi wa ujenzi wa ukuta huo ameshapatikana kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *United Nations Office for Project Service* (*UNOPS*) ambaye ni Kampuni ya *Dezo Civil Contractor Company Limited*. Kampuni hii tayari imesharipoti kwenye eneo Kilimani na hivi karibuni ujenzi utaanza na unategemea kumalizika baada ya miezi 7.

Naomba pia nipokee pongezi ya Mhe. Panya Ali Abdalla na alitaka posho kikosi kazi cha mifuko ya *plastic* ilikuwa ni kidogo na kinachelewa kutolewa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa nakiri kuwa kikosi kazi cha kusimamia marufuku ya mifuko ya *plastic* kinafanyakazi nzuri na kinahitaji kupongezwa na wizara inatambua kuwa posho linalotolewa ni kidogo. Hali hiyo inatokana na hali halisi ya fedha ilivyo.

Hata hivyo, wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwenye bajeti hii imepandisha posho hilo kutoka elfu 20 na kwenda elfu 30. Wizara yangu itaendelea kuongeza posho kadri hali ya fedha itakavyokuwa nzuri. Hapa pia naomba nitoe wito kuna wale wasiosikia bado wanaendelea kuleta mifuko ya *plastic*, naomba wananchi wakatae kutumia mifuko ya *plastic* na kuweza kulinda mazingira mazuri na haiba ya Zanzibar.

Pia kulikuwa na suala kwamba maeneo mengi yanayochimbwa mchanga na kifusi hayarejeshwi katika uhalisia wake. Nakubali lakini hili kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Sheria ya Mazingira ya 2015 imeanzisha utaratibu wa kuweka mikataba ya uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka kama vile mchanga na kifusi. Mikataba hiyo inamtaka mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji kurejesha eneo. Mfumo huo umeanza hivi karibuni ili kuhakikisha kuwa maeneo yanayochimbwa yanarejeshwa katika uhalisia wake.

Pia kufukia eneo la Qatar, Pemba. Kama inavyofahamika kuwa eneo linaloanzia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hadi Ikulu ni muhimu sana kwa kuota mikoko ambayo inaendelea kunawiri vizuri. Mikoko hiyo imekuwa ndio mhimili mkubwa wa kutoa kinga dhidi ya mawimbi ya bahari na kupunguza kasi ya upepo mkali kutoka baharini kwenda nchi kavu pamoja na mmong'onyoko wa fukwe. Hivyo, kuiondoa mikoko na kuifukia sehemu hiyo kunaweza kupelekea maji ya bahari kuvamia sehemu

nyengine na kuweza kusababisha athari kubwa za kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Tunamuomba Mhe. Mwakilishi wa Chake Chake achukue nafasi ya kulihamasisha Baraza la Mji wa Chake Chake kuliendeleza vizuri eneo lililoruhusiwa kufukiwa ili liweze kutoa tija iliyokusudiwa. Hili naomba nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi wa Chake Chake Meya Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuhakikisha wananchi wake wa Jimbo la Chake Chake wanapata eneo la kupumzikia. Kwa kweli anafanyakazi nzuri na Mwenyezi Mungu *inshaallah* atamsaidia na atafanikiwa katika lengo lake. (*Makofi*)

Lakini vile vile kulikuwa na suala la Maafisa wa Wizara yako wanaendelea kutoa vibali ovyo vya ukataji wa miti na uchimbaji wa mchanga. Lakini naomba nilijulishe Baraza hili tukufu na wananchi kwa ujumla, vibali vya ukataji miti na uchimbaji wa mchanga ni Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka.

Aidha, vibali vya ukataji miti hutolewa na idara hiyo baada ya muombaji kujaza fomu ambayo hupita kwa wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na Sheha wa eneo husika na baada ya kufanyika kwa ukaguzi ili kuona mti unaombewa kibali kuwa unastahiki kukatwa au laa. Kibali cha uchimbaji mchanga hutolewa na Idara ya Misitu vile vile baada ya kamati ya wadau inayoongozwa na Mhe. Mkuu wa Wilaya husika kupitia na kuridhika na eneo linalotaka kuchimbwa. Kutokana na utaratibu huo kwa sasa katika eneo la Micheweni lipo eneo moja tu la mchanga lilitolewa kibali ambalo ni eneo la Mamoja Shehia ya Shumba Viamboni.

Lakini vile vile kulikuwa na suala la matumizi ya misumeno ya moto. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imepiga marufuku ya matumizi ya misumeno ya moto kwa

nia ya kulinda misitu yetu. Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka imekuwa inafanya doria za mara kwa mara ili kukamata misumeno hiyo. Kutokana na doria hizo, katika kipindi cha mwaka 2013 hadi 2016, jumla ya misumeno ya moto 159 imeshakamatwa na kuchomwa moto Unguja na Pemba. Hivyo, naomba nitoe wito kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba kuendelea kuhifadhi misitu yetu na kuacha kutumia misumeno ya moto.

Lakini pia naomba niseme kulikuwa na suala ambalo ukisoma kitambatanisho E1 kimeeleza muhtasari wa matumizi kwa program kuu ndogo ya mwaka 2017/18. Miongoni mwa program zilizomo kwenye kiambatanisho hiki ni program ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ambapo kuna fedha za kawaida ni shilingi 740,698,000.0 na kazi za maendeleo.

Kwenye kazi za maendeleo mchango wa SMZ ni shilingi 50 milioni na mchango wa Wahisani ambao ni shilingi 804,733,000/=. Kwenye kiambatanisho E2 mchango wa SMZ upo sehemu ya 13 ya kiambatanisho ambapo ni 50 milioni. Aidha ushauri wa matumizi ya zero (0) badala ya *dash* (-) umepokelewa na tuaendelea kuufanyia kazi kwa mujibu wa tarakimu zinavyokaa ndani ya bajeti.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru kwa namna ya kipekee Mhe. Abdalla Maulid Diwani ambaye kwa kweli ananisaidia sana na amenisaidia sana katika kutatua na kukabiliana na changamoto ya Shirika la Umeme. Kwa kweli naomba niseme ni shujaa ni hodari na anafanyakazi kila wakati anajitahidi kunipigia simu na kunieleza mapungufu yote ambayo anayaona ndani ya Shirika la Umeme na nasema hatoi hoja tu hapa Barazani lakini hata kama hakukuwa na Baraza basi yeye wakati wowote anapoona tatizo yuko mstari wa mbele katika kunieleezea na mara nyingi nayafatilia na nampa majibu husika.

Lakini vile niombe kwa Wajumbe wengine wote tusisubiri wakati wa vikao, tusisubiri wa kati wa bajeti, wakati tumeona tatizo basi tukubali tukambizana. Lakini vile vile Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub yaani namshukuru sana na nasema namshukuru kwa sababu na yeye amekuwa mdau katika sekta sana ya maji mara nyingi ananipigia simu ukiacha mbali ya jimbo lake, lakini pia hata katika maeneo mengine lakini amekubali kujitolewa kwa hali na mali katika kuhakikisha kwamba maji katika eneo lake yanapatikana. (*Makofi*)

Naomba niseme hili na Waheshimiwa wengine wawe mfano kama wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia katika sekta ya maji. Nasema hili kwa sababu saa zote ananipigia simu yeye hajali usiku hajali mchana hajali saaa ngapi, akiona maji shida kwa watu wake basi tayari ananipigia simu. Lakini nikushukuru sana Mhe. Jaku na kama nilivyozungumza katika taarifa yangu na majibu yangu kwamba sasa hivi eneo la Michamvi linafanyiwa kazi kisima kile kitaungwa na tangi liko pale. Lakini niwashukuru sana wale wengine ambao kwa namna mmoja au nyengine wanaendelea kunipa mashirikiano, najua Mhe. Mtumwa Peya amejitolea kwa hali na mali kutoa fedha zake za mfuko pia katika kuhakikisha visima vile tutavikamilisha.

Lakini na wale wote walioweza kutoa kama kina Mhe. Suleiman Sarahan Said na wengine kina Mhe. Yussuf Hassan Iddi basi wote naomba tuendelee kushirikiana na nasema tuendelee kushirikiana kwa sababu changamoto hizi za wananchi ni nyingi na zipo ndani ya wizara. Serikali inajitahidi sana dhamira yetu kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata huduma safi. Lakini wakati mwengine tunakwazwa na fedha.

Lakini pale ambapo tunaona Mheshimiwa Mwakilishi una uwezo wa kusaidia, una mfuko wa jimbo lakini pia umepata mfadhili sehemu nyengine. Niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi tushirikiane katika hili maana yake lengo la serikali, lengo la wizara yangu ni kuwa na wananchi wanaoishi na afya njema na ili uweze kuishi na afya njema lazima upate maji, lazima uweze kuishi maisha mazuri, lazima upate umeme, lazima uishi kwa raha.

Kwa hiyo, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi katika hili naomba tuendelee kushirikiana. Lakini naomba mnisamehe wale wote ambao sikuwataka kwa namna moja au nyengine lakini bado wanaendelea kunisaidia wakati wote. Naomba niwashukuru sana.

Lakini kama mlivyoeleza katika maelezo yenu na wengi waliochangia nimekuwa najitahidi sana mimi na Naibu Waziri wangu kila wakati kunapotokea changamoto kila pahala tunahakikisha tunafika katika eneo na kuweza kutatua kile kilichokuwepo yale wakati mwengine yanakuwa zaidi ya uwezo wetu na ndio maana tunasema jamani tunaomba mvute subra ili tutakapopata uwezo kidogo tuweze kulitatua. Lakini tumejitahidi sana, tumetatua mambo mengi nawashukuru sana na kila mmoja anaona kuna eneo nilikuwa silijui na sikutegemea hata siku moja kama ningekuwa napajua kule Dimani kwenye visima kule nilikuwa sikujui wala sikujua hata kama wanakaa watu. Lakini namshukuru Dkt. Mwinyihaji Makame ameweza kunifikisha katika eneo hilo niweze kukujua.

Lakini nimshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alinipeleka eneo sijawahi kuliona pia lakini nimekuta mji mkubwa mji uliopendeza wananchi wanaishi huko, tutajitahidi kutoa huduma, tutajitahidi sana ili tuweze wananchi wetu kupata huduma kwa mashirikiano ya pamoja tunaweza.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba sana kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar tusaidiane katika kukinga vianzio vya maji, tusaidiane kuacha kujenga nyumba kiholela, tusaidiane katika kufanya udalali wa maeneo ambayo hayahusiki tuache kabisa. Masheha nawaomba sana tusaidiane kwa sababu wakati mwengine unakuta tatizo hata Wajumbe hapa wameeleza Sheha ndio anaanza kuuza maeneo. Lakini kwa elimu aliyoipata kwa muda huu na kwa udhibiti wa Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa naamini hawataendelea na yale ambayo hoja nyingi zimetokea. (*Makofi*)

Mwisho kabisa, naomba niwashukuru Mawaziri wenzangu wote kwa kunisaidia kwa hali na mali katika kufanikisha kazi zangu za kila siku. Mimi naamini sana watu walikuwa wanasema wizara yangu ngumu. Mimi naamini sana wizara yangu si ngumu tunaiweza, tunajiamini na tunaweza kufanya kazi. Lakini ili kazi hii iweze kupata mafaniko kwa umoja wetu tushikamane ili tuweze kuhakikisha wananchi wetu tunawahudumia ipasavyo. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Toa hoja Mheshimiwa. Mheshimiwa naomba utoe hoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa wale wote wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Spika: Watendaji wa Wizara wanaweza wakashuka huku kuja kumsaidia Mhe. Waziri mnaruhusiwa. Tunaendelea.

Fungu N01 Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Jumla **10,035,127,000**

Kifungu PN0101 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi 1,959,901

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina kifungu ambacho HN 010101 Uandaaji na Uibuaji wa Sera na Tafiti za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia pamoja na Mhe. Waziri kunijibu katika suala la utafiti katika eneo la Qatar amesema kwamba mikoko inazuia maji na ndio ambayo ni sera. Lakini nataka nizungumze Mheshimiwa kabla ya mikoko pale katika eneo la Qatar kabla ya enzi hizo palikuwa hapana mikoko yalikuwa ni maji tulikuwa tukiogelea wala bahari haijapanda juu. Lakini baada ya kupandwa mkoko au baada ya kuachiwa mkoko sasa hivi kuna kilomita moja kutoka Bahari Kuu mpaka mkoko.

Nimemuomba waziri katika eneo la Qatar ambapo kuna soko linajengwa anipe nafasi kidogo tujaze wakati lile limekuwa pori na tuna kilomita moja ya kuzuia maji kutoka bahari kuu.

Kwa hivyo, waziri alinijibu kwamba nistahamili kwamba utafiti umefanywa, lakini utafiti gani ambao umefanyika kwamba tusipate eneo la kujaza kutoka upande wa Makamu wa Pili wa Rais kuja kuunganisha na soko ambalo jipya linajengwa. Kwa hivyo, hapo nilitaka ufafanuzi zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake suala lake kama lifuatayo:-

Kama nilivyomjibu swali mama kwamba mikoko hii ndio imekuwa mhimili mkubwa wa kutoa kinga dhidi ya mawimbi ya bahari na kupunguza kasi ya upepo mkali kutoka baharini. Kama mwenyewe alivyokiri hapo kwamba eneo lililobaki ni dogo mikoko ile ilipandwa kwa sababu maji yalikuwa yanapanda juu kwa hiyo mmong'onyoko umekuwa mkubwa ili ule mmong'onyoko uweze kuzuilika, kwa hiyo kupunguza kasi ya yale maji ya mawimbi. Ndio maana hata kwenye *speech* yangu Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia eneo la Mtoni kuhamasisha wananchi kwamba pale papandwe mikoko ili ile *speed* maji kuja juu kuja kwenye nyumba iweze kupungua.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa pamoja na majibu yake mazuri lakini mimi nafikiri tukikaa humu Barazani kwa kujadiliana hapa itakuwa ni kazi ndefu. Nimuombe waziri na kamati yake hiyo ya ufundi twende tukaangalie lile eneo na tuweze kuelewana kama atakubali hivyo mimi nakubaliana nae.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri muende mkafanye ziara.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tumekubali tutakwenda Pemba.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasimama kwa kifungu namba HN01010302 Kuratibu na kusimamia shughuli za kisekta wizara PBA Pemba. Nilikuwa nasimama kwa *issue* ya misitu na msitu wa Ngezi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna gazeti la serikali ya tarehe 6 linasema hivi:-

"Tunasema hivi kwa sababu tunazo taarifa za uhakika kwamba kuna muwekezaji amemegewa ardhi kwenye msitu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa usilisome gazeti nafikiri ungeenda kwenye hoja yako tu moja kwa moja kwa sababu anafahamu waziri, hoja yako tu moja kwa moja kwa sababu anafahamu waziri.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hoja yangu Mhe. Waziri amejitahidi kujibu kwamba msitu ule haujakatwa viwanda, Mhe. Mwenyekiti na jana tulikuwa tunaongea na Mhe. Waziri wa Kilimo alikiri kwamba alikwenda kule alikuta page msitu umekatwa na alitoa amri page zile zitolewe bila ya kumshauri mto yoyote. Sasa nataka kujua Mhe. Mwenyekiti, je msitu huu umekatwa viwanja na amepewa mwekezaji na kama umekatwa atavifuta lini hivyo viwanja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh mkwezi na mkulima swali lake kama ifuatavyo. Eneo la Vuma Wimbi Makangale kwenye Msitu wa Ngezi. Kwanza naomba kutoa taarifa kwamba hakukupimwa viwanja,

naomba kurejea kauli yangu lijulisha Baraza lako, lakini pia kuwajulisha wananchi kwamba eneo lile halikupimwa viwanja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ninayesimamia sekta yangu, kweli nilitoa amri ya kwenda kupimwa eneo lile baada ya mgogoro wa muda mrefu ambao unatatuliwa kwa barua haufiki mwisho, nikawaambia kapimeni na pamepigwa kambi siku tatu, kuanzia saa 2:00 mpaka saa 11:00 watu wanafanyakazi, nilizungumza katika mazungumzo yangu. Walikwenda kupima tukazungumza na tukasema baada ya kupima na kuweka *beacon* zile basi tutapata kujua eneo halisi na katika upimaji ule tuliomba sana usiathiri Msitu wa Ngezi na usiathiri eneo la JKU.

Sasa kwa vile kumepimwa mimi niko kama waziri muhusika ambaye nashughulika na *issue* za upimaji, wataniletea *layout* kesi yoyote nitaletewa. Kwa hivyo, hakuna kiwanja hata kimoja kilichopimwa, alama zile zimewekwa kwa mujibu wa utaratibu na kwa mujibu wa sheria za upimaji ambazo wizara yangu inazisimamia.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mimi nataka anihakikishie kama kipo kiwanja kilichopimwa akifute, kwa sababu ule Msitu wa Hifadhi wa Akiba kama kipo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nafikiri Kiswahili tu tunasema kupima, lakini nadhani kuna kupima halafu kuna kukata kwa ajili ya kugawa viwanja, nafikiri mngeiweka vizuri hiyo. Kwa sababu watu wengine wanahisi ukipima Mhe. Waziri maana yake ndio umekata. Naomba Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimueleweshe Mhe. mkwezi na mkulima swali lake la ziada. Nasema tena pale

hapajakatwa viwanja. Pale pamekatwa eneo ambalo warithi wa Sheha Mjaja Mpwani wamepata haki mahakamani kwamba ni eneo la kwao, ndio tukasema kupimwe kukishakupimwa ndio tutaweza kukaa kutatua mgogoro. Hakupewa mtu pamepimwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu na mimi kama waziri wa sekta bado naendelea kusimamia sekta yangu katika kuhakikisha kwamba tunamaliza kutatua migogoro. Tunaiheshimu sana serikali, Msitu wa Ngezi tunauheshimu na sote ni wazalendo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, unajua kwa vile waziri huyu tunamuamini sana. Tunawaamini wote lakini unajua *as you know* kama alivyosema Rais wa Ghana "*If you educate woman you have educate the whole family"*, tunamuamini. Lakini nataka kumwambia maneno matatu.

Jambo la kwanza ajue kwamba kuna mwekezaji inasemekana na gazeti limerikodi la serikali hili. Sasa kama kapimiwa, nataka tuendelee kwa sababu, kama kuna mwekezaji kapewa, kwa sababu yuko mwekezaji inasemekana kapewa, kama kapewa namuomba amfutie. Lakini kwa leo naomba tuendelee, kwa sababu namwamini, lakini kama yupo akamfutie. Akumbuke huu ni msitu wa hifadhi ya akiba wa kizazi cha leo na kizazi cha kesho. Tusijaribu kukiuka taratibu za serikali, tuna kila *record* hapa za Mhe. Mohammed Aboud alipokuwa Waziri wa Kilimo, Mhe. Hassan Nassor Moyo alipokuwa Waziri wa Kilimo mwaka 1968 zinasema wazi wazi na ramani hata mimi ninayo hapa hii hapa Mhe. Mwenyekiti, inaonesha ulivyopimwa ule msitu. Namwamini lakini tuendelee lakini kama yupo akamfutie.

Kifungu PN0101 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi 1,959,901,000

Kifungu PN0102

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Abdalla Ali Kombo, atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, halafu atafuatia Mhe. Hassan Khamis Hafidh Dayaspora kwanza halafu utafuatia wewe Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana nilitaja mambo mengi, lakini pia nilitaja utata wa kiwanja cha Tomondo hapa karibu ya Mombasa. Kuna kiwanja kina utata kwamba kuna wananchi au kuna mwananchi alikiendeleza, kilikuwa shimo alipewa akajaza kila kitu kimekaa sawa. Wizara imekichukua na kuna tuhuma aliyekichukua ni waziri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako nataka kumuuliza Mhe. Waziri, je hiki kiwanja amekichukua kweli, na kama amechukua anajua ni ukiukwaji wa sheria na wa katiba ya Chama cha Mapinduzi na katiba ya nchi. Hati namba ZTCRO Z651/2004. Sasa namuuliza waziri hiki kiwanja umekichukua kweli.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kusimamia kusema kwamba mimi kama Salama Aboud Talib bado nahitaji kupata kiwanja ndani ya wizara ya ardhi ambayo naiongoza, lakini kiwanja cha Tomondo sikuchukua, lakini nimefuata sheria na taratibu za ardhi kama zilivyo na kama zilivyoainishwa ndani ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Samahani ooh! Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Ulimi hauna mfupa endelea.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Samahani Mhe. Mwenyekiti, samahani sana unajua

Mhe. Mwenyekiti: Hamna tatizo endelea tu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa na huwa hapa sipendi hata kidogo kusema uongo. Nilichukua msahafu nikaapa na wewe ulikuwa karibu hapo. Ninachosema na ninachoomba, Mhe. Mwanasheria Mkuu sijui kama kuna taratibu ya kusimamisha Baraza. Lakini majibu ya kwamba simo, kachukua, hayumo kama alivyojibiwa mjumbe mwenzangu wa msitu wa hifadhi mimi siyapendi.

Kwa hivyo, naomba twende Tomondo akatuoneshe namba hii ya kiwanja hiki nani aliyechukua kama sio yeye ama jamaa zake ama ndugu zake. Mhe. Mwenyekiti, nasema tena serikali yangu naipenda sana, lakini na ubadhirifu usiokuwa na mpango umeshanitosha nadhani na wenzangu. Kiwanja hiki wenyewe wamekuja asubuhi hapa, maofisa wa ardhi wanakiri kwamba hapa pameendelezwa hili lilikuwa shimo. Alivyomaliza tayari, inasemekana, sasa kwa sababu sitaki isemekane namtaka Mhe. Waziri akanithibitishie viwanja hivi hapa. Sitaki wenyewe wengine kuwataja kwa sababu sio utaratibu. Lakini kiwanja hiki hapa wamejikatia. Kwa hivyo, sitapenda kuipitisha hii bajeti mpaka nipate ukweli.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Ali Kombo ahsante. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza naomba nikubali ombi lake la kwenda katika hiyo sehemu. Lakini kwanza nataka kumuhakikishia hiyo

sehemu anayozungumza sio jaa. Lakini kwa uhalisia wa eneo lenyewe na uharibifu wa huyo aliyefutiwa na kupewa mwanzo ndio alikuwa kasababisha pamekuwa jaa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka kumuhakikishia Mhe. Abdalla Ali Kombo kwamba watu wengine wote kupewa viwanja ni haki yao na hata mimi ni haki yangu. Lakini kwa pale ninakuhakikishia kwamba sina kiwanja ambacho ni cha kwangu kama Salama Aboud Talib. Lakini nimelipokea suala lake tutakwenda na wengine watakwenda, lakini bado natafuta eneo muafaka Mhe. Mwenyekiti, na mimi kama Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupatiwa kiwanja na nikikipata kama ni haki yangu kisheria basi nitachukua.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Mhe. Abdalla Ali Kombo amekubali Mhe. Waziri mtakwenda.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Lini tutakwenda. Ndio nijue.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Leo.

Mhe. Mwenyekiti: Leo mtakwenda. eeh.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesimamia katika hoja hiyo hiyo ya mgogoro wa ardhi. Nilichangia jana.

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kipi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha Utawala wa Ardhi SN010201 Utawala na Ugawaji wa Ardhi, halafu chini yake pana HN0102 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, jana katika kuchangia kwangu Mhe. Waziri nilimpa mpaka nakala na Mhe. Mwanasheria Mkuu alizungumza vizuri hapa, kuwa ardhi ni mali ya serikali. Nikasema wawekezaji wazalendo hawana haki nchi hii au kuna serikali ngapi. Namshukuru Mhe. Waziri kayaona makaratasi na kakiri. Lakini ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri kuwa nia yake ni safi na tunaiona lakini watendaji wake ndio wanamuangusha. Mimi nataka anieleze tu wala sitaki tufike mbali. Ameshayaona hayo maelekezo kuna wawekezaji wanapata shida wamefuata *process* zote na vibali vyote, na sio kimoja, viwili au vitatu vyote na kaviona, lakini wanabughudhiwa. Hebu utaratibu huu maelezo yake yakoje.
Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la pili vile vile kuhusu Mahakama ya Ardhi iliyokuwa Majestic, chini yake ni utatuzi wa mgogoro wa ardhi ikiwa ni mahakama

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ngoja tumalize hili moja la mwanzo. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu swali lake Mhe. Jaku Hashima Ayoub kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji wazalendo wana haki ndani ya nchi hii, lakini haki hiyo haitolewi tu kwamba mwekezaji mwananchi mzaliwa wa hapa lakini uwe na uzalendo wako, lakini sheria na taratibu za serikali lazima zifuatwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub a-*declare interest* kwa sababu jana kanipa kweli *documents* zake za eneo la

Mtoni, nilimwambia nitazipitia, nitaziangalia na halafu tutaona, kwa sababu pia jambo lenyewe ni la muda mrefu. Kama nilivyoamua kwenda kupima Vuma Wimbi nikaenda nikalifuatilia na nikaamua nilipime ili kumaliza mgogoro basi na hili nilichomuahidi jana ni kwamba nitalifanyia kazi, na ninasema Baraza lako linisikie nitalifanyia kazi na nitampa majibu kutokana na kazi ambayo nitaifanya kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi sio mgeni katika chombo hiki kuliko yeye humu ndani Mhe. Waziri. Kabla ya kuchangia nili-*declare interest*, na siko peke yangu tu kuna na mwekezaji mwengine yupo Mangapwani,

Mhe. Mwenyekiti: Na wewe upo?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu nili-*declare interest*, sio mgeni. Nimesikia mawazo yake na ninamuamini sina mashaka na yeye tuendelee. *Hansard* zipo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasimama…

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Suleiman Sarahan Said, ni Mhe. Hassan Khamis Hafidh nimemruka. Mheshimiwa huyu ni rafiki yangu halafu namsahau mara kwa mara. Mhe. Diaspora.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nasimama kwa HN01020101 Utawala na Ugawaji wa Ardhi. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba ugawaji wa ardhi ambayo imegaiwa na serikali sina tatizo nayo.

Kwa mfano, Mhe. Waziri alitangaza kwamba atafuta viwanja vya pale Tunguu, haki hiyo anayo sheria inamkubali. Lakini nikamwambia Mhe. Waziri kuna watu nchi hii wana viwanja zaidi ya 30 ukiwacha Tunguu na kwengineko, kuna watu nchi hii wana maeneo hayana mwisho. Sheria nakumbuka inasema sijui heka ngapi. Ndio eka 8 mwisho kupewa, kuna mtu ana heka karibu 20 au 30 nchi hii hii.

Sasa swali langu ni kwamba ni lini atawafutia au atavichukua hivyo viwanja vya hao manyangumi wenye maheka kama haya. Kwa sababu pale vidogo vidogo kasema atavifuta hatuna tatizo haki anayo na uwezo anao. Lakini hao wenye heka zilizokiuka sheria, sheria heka 8, lakini kuna watu wana heka 40, 30, 80, haiwezekani nchi hii ndogo atawafutia lini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri lini unafuta hivyo viwanja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh mkwezi na mkulima kuhusu swali lake la kufutiwa maeneo makubwa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema pale na bahati nzuri Mhe. Mwanasheria Mkuu alifafanua vizuri. Nchi hii inaongozwa na sheria na taratibu. Sheria namba 12 ya mwaka 1992 iko wazi na mimi nasema mbele ya Baraza lako tukufu na wananchi wananisikia, nilitoa kauli hapa walikuwa wakali, lakini bado naendelea kusimamia sheria na nitasimamia taratibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi wakati sheria hatujazibadilisha basi nitahakikisha wale wote wenye maeneo zaidi kinyume na utaratibu, basi hatua itafanyakazi yake na sheria itafanyakazi yake. Suala hili nalisema kwa kinywa kipana tena kwamba bahati nzuri mimi ni msimamiaji wa sheria, bahati nzuri nasema sana

mimi hapa nilipofika sina inachokihitaji, nahitaji kuhakikisha kwamba naiacha Zanzibar njema na naiacha Zanzibar kwa vizazi vijavyo iko salama katika mikono salama. Kwa hivyo, hilo tutalifanyia kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema miongoni mwa mawaziri ninaowaamini yeye namwamini. Lakini Mhe. Waziri akumbuke kwamba kuna watu wanahitaji ardhi na watu wana ardhi kubwa kinyume na utaratibu. Sasa aniambie bado hajaniambia, aidha bajeti hii nitawafutia au ijayo. Nataka ile kauli ya mwanamke kama Mhe. Salama Aboud atawafutia lini hilo ndio swali langu. Lini atawafutia eidha bajeti hii au mara tu baada ya kutoka hapa nitaanza kuwashughulikia na kuwafutia, kama hivyo nataka kujua.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. mkwezi na mkulima naomba bado nikuambie hivi sheria hizi zimetungwa na Baraza hili la Wawakilishi, na sheria hizi ni lazima tuziheshimu kwa mujibu wa utaratibu. Hii kazi itafanyika baada ya kuhakiki maeneo yote, na sheria tutazifuata kwa mujibu wa taratibu zilizoidhinishwa na Baraza lako hili tukufu Mhe. Mwenyekiti, sitokwenda kinyume na taratibu. Sitokwenda kinyume na sheria, sitokwenda kinyume na taratibu zilizoidhinishwa na Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, naomba niendelee kuhakiki, kama nilivyojibu swali langu na niweze kusimamia sheria na nitaendelea kusimamia sheria, kama ya kufuta nitafuta na kama ya kuongeza nitaongeza. Lakini bado nitaendelea kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu za nchi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nitamruhusu lakini mimi hoja yangu iko pamoja tu. Mpaka amalize uhakiki haya, lakini hii nchi itakwisha na hatuna pengine baada ya hapa. Hajaniambia lini, lakini nitamruhusu tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nasimama kwenye HN01020202 katika uimarishaji wa miji kiuchumi unaolenga kukuza pato la wananchi na taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sikumsikia, lakini bado naendelea kumwambia kwamba kwa makusudi ya serikali imeamua kuwa Mji wa Chake Chake kuweka Mji Mkuu. Sasa Mhe. Waziri wakati nachangia nilimwambia kwamba eneo la *opposite* na Archipelago au naweza kusema hifadhi ile *ZSSF Hotel*. Eneo lile nilimwambia kwa hali yoyote sifikirii kama panaweza kukaa nyumba kiusalama kwa sababu eneo la barabara lina mita karibu 15, eneo la bahari liko hapo, eneo lililobakia zaidi ya mita 10 mpaka 15 lakini pia ni eneo la Ikulu ambalo halitaki *disturbance* kwa sababu liko karibu na kona ya kupindia Ikulu, hauwezi msafara ukapinda kwa *speed* kubwa ni lazima upunguze *speed*.

Mhe. Mwenyekiti, nilimwambia Mhe. Waziri kwamba eneo hili atupe kwa ajili ya kuweza kufanya Forodhani ya Pemba, pale Chake Chake kwa ajili ya wananchi ana pato la wananchi na ana pato la serikali, waziri hajanijibu. Kwa hivyo, hili nalisimamia kwamba waziri anatoa kauli gani hapa, kwa sababu ile Achikilago ile kuingia ndani ya nyumba iko chini ya barabara, siku ambayo itataka kuongezwa barabara ile basi itabidi Achikilago ivunjwe. Sasa sijui serikali itakuwa pahala gani naomba anijibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimtowe hofu mheshimiwa wangu mpendwa Meya wa Jiji la Chake Chake Mhe. Suleiman Sarahan Said. Naomba nimtowe hofu sana katika miji 14 inayopangwa midogo basi mji wa pili ni mji wa Chake Chake kutoa Zanzibar Unguja. Kwa hivyo, wizara yangu sasa hivi inaendelea kuupanga mji wa Chake Chake, nafikiri kama ana mawazo mazuri ambayo anahisi yataleta imput na tija ndani ya kupanga mpango ule basi

Dk. Mohamed wa Mipango Miji yupo naomba ushauri tumeupokea, na wewe kama una ushauri wa ziada basi uje.

Nimekubaliana na *concept* yako, lakini ulinikimbia wakati nilipokuja Pemba na nilitangaza hapa tukutane kwa sababu ya kadhia hii hii. Lakini mimi binafsi nilivyokwenda Pemba lile eneo kwanza nimeliona kwa Forodhani halifai, kwa sababu Forodhani pale watu watataka kupumzika, lakini watoto pia wanahitaji kucheza eneo lao liko chini ya barabara na huku pembeni kuna mikoko. Nilikaa sana nikashauriana na Manispaa ya Chake Chake, lakini pia tukashauriana na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba Mhe. Mwanajuma Majid tukashauriana kwa bahati mbaya yeye mwakilishi alikuwa hayupo, lakini tukashauriana kwamba eneo lile halitofaa nililisikia hapa nikaona niendee nikatizame nikaliona na tukatoa ushauri *for the time be* tuongee na *ZSSF* na tuliongea nao ili tuhamie eneo la Tibirinzi la nje kama tunahitaji watoto kucheza na watu kwenda kupumzika, wakati mji wa Chake Chake unapangwa basi maeneo hayo yote kama yalivyopangwa Mjini Unguja basi na hayo yote kwenye Mji wa Chake Chake yatakuwepo na wananchi wako wataburudika na kufaidika bila ya tatizo lolote.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majbu yake Waziri ingawa alinipigia simu lakini Waziri anakuwa na tabia ananiogopa mimi maana yake nikipiga simu ananiambia uko wapi, nikimwambia niko Unguja ananiambia basi niko Pemba sasa mara hii tutaondoka ndege moja tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nipo katika Mahakama ya Ardhi kifungu HN 01020106 Utatuzi wa migogoro ya Ardhi ikiwemo Mahakama ndio inayotatua migogoro ya ardhi..

Mhe. Mwenyeki: Mbona haijatengewa kitu hii.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hebu angalia tena Mhe. Mwenyekiti utatuzi wa migogoro ya ardhi na Mahakama nayo inatatua migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti: Angalia mna 00 humo Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, HN01020106 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio hiyo ninayozunguma mie Mheshimiwa haijatengewa fedha hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sababu gani basi haikutengewa pesa.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sasa hilo suali liko wazi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti mimi naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub muwakilishi wa wananchi jimbo la Paje asome SN 010203 utatuzi wa migogoro ya ardhi jumla ya Shilingi utaziona hapo kwa Makadirio 3,019,768,000 zipo chini kabisa hapo kama utazona na kwa makusudi iliwekewa sub program yake na ndio maana hapa likawa halikupangiwa fedha na limetolewa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa darasa alilonipa ndio hapa hapa tena anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa, nipo kwenye Mahakama ya Ardhi nayo ni kutatua migogoro ya ardhi hiki chombo tulikuwa tukiwalaumu Mahakimu kwa muda mrefu haki hazipatikani, lakini chumba kimoja wanatumia maafisa watatu mpaka wanne hata vyombo vyetu vya habari vimesema choo ndani kina mtihani. Si juzi wala jana karibu miaka mitatu tunapiga kelele suala la Mahakama ya Ardhi

ipo Majestic, hata pahali pa kujificha mvua pale hapana imekuwa kama hospitali ya Mnazi Mmoja tulipopiga kelele hapa kuhusu kujega banda.

Wananchi wanatoka shamba wanakuja kufuata haki zao hebu tueleze Mhe. Waziri kweli ndio Serikali imeshindwa kutafuta utafiti wa kupata jengo jengine na pale panapatikana haki. Ukimtafuta waziri unaweza kufika miezi miwili hujamuona ndio kama nilipokusifu jana kuwa miongoni mwa Waziri wanaopokea simu haraka mmoja wapo ni wewe, hebu tueleze kweli Serikali imekosa pahali pa kupata haki zao, chumba kimoja wanakaa maafisa watatu mpaka wanne...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante imeshafahamika ngoja akujibu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli na nimesema ndani ya ufafanuzi wangu kwamba Mahakama ya Ardhi Majestic jengo lile halipo katika hali nzuri mimi binafsi nakiri hilo. Lakini baada ya kulipata mbali ya kupitia Baraza hili mimi binafsi wakati nimekwenda kulitembelea pale basi niliona ubovu wa jengo lile na jengo lile limeshafanyiwa tathmini na sasa hivi tumo katika hatua za mwisho za kutafuta fedha kwa ajili ya kulijenga jengo hilo. Mimi naomba aendelee kuvuta subira jitihada wajada tunajitahidi kuhakikisha kwamba jengo lile tunalipa hadhi yake inayofaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, maneno mazuri sadaka ni kweli nakubaliana nae kazungumza lakini huu ndio utaratibu wa Serikali yetu hili suala haliulizwa jana wala juzi karibu miaka minne mpaka mitano linapigiwa kelele, afya za wafanyakazi mle haziridhishi. Kuna jengo kule Wizara ya Biashara pale hebu walifikirie basi, wana majengo mawili pale Wizara ya Biashara kweli Serikali imeshindwa kutafuta pengine.

Haya ndio majibu ya Serikali tumo mbioni muda mfupi lakini pale ndio panapo haki za wanyonge zinapopatikana kesi zinakawia kufika kwa kuwa chumba kimoja wanatumia watu wanne na halipo juzi wala jana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ushauri wako wa kwamba waende kwenye jengo lilikuwa la Wizara ya Biashara au vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Popote watakapopata pahali pa kujistiri tu kile kijengo kipo kiza sana Mheshimiwa ni hatari kabisa, Mhe. Abdalla akiambiwa akapande ngazi hawezi kupanda mle anamtafuta mtu pia hawezi kupishana inabidi apite kwenye ngazi upande upande na si juzi wala jana karibu miaka mitano.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na *concern* ya Mhe. Muwakilishi Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu hii Mahakama ya Ardhi, kwa kweli lakini naomba nitoe taarifa tu kwamba Wizara ya Biashara haina jengo. Hapa kuna mambo mengi ambayo tumejitayarisha kuyafanya ila nina imani kabisa kabisa katika bajeti waliyopewa hii Wizara hii inayohusika na mambo ya Ardhi watawatafutia njia nzuri ya kuwaweka wafanyakazi wapate starehe na kazi zao kwa mubashara. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Unasimama mara ya tatu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya Mheshimiwa mimi sichoki kusimama anayehangaika hachoki akishaweka pale ndio atakuwa ameshachoka Mheshimiwa. Mhe. Waziri, hebu tutafutie njia nzuri ipi maana yake njia inaweza kuwa na visiki vikaondoshwa ukaweza kupita, njia ikakarabatiwa, ikajengwa, ikazibwa ukaweza kupita, hebu Mhe. Waziri tufahamishe njia nzuri ipi ili wananchi waweze kusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri tuiachie Serikali watalishughulikia hili. Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mheshimiwa kuhusu utaratibu sikusimama lakini nimesimama kuhusu habari hii ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub hoja yake ya tatu aliyosema lakini nataka twende kwenye kanuni 98, kanuni ya fasili ya 7 yenye kifungu (e) na (f). Mhe. Mwenyekiti, ukishamuuliza ikiwa mjumbe hatokubaliana na maamuzi ya Waziri, Waziri mwengine yeyote anaweza kutoa ufafanuzi ili hoja yake aweze kuridhika, au Mkuu wa Serikali katika Baraza hili Makamo wa Pili wa Rais yupo aweze basi atoe *commitment* kitu gani kifanyike kabla ya kwenda kwenye kura au jengine lolote.

Mhe. Mwenyekiti: Basi nampa Mhe. Waziri mwenyewe tena.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kusema kwamba hili suali halikunishinda lakini kwa vile alizungumza biashara ikabidi atolewe ufafanuzi katika kutumia jengo la Biashara. Ninachotaka kusema tunakiri kwamba jengo lile ni bovu lakini pia tuna mahitaji ya lazima Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa hiyo bajeti ya mwaka huu kumetengwa fedha kwa ajili ya kujenga lile jengo la Kaskazini Pemba Mahakama ya Ardhi na tulikaa tukakubaliana bajeti ya mwakani sasa hivi tumeanza kufanyia ukarabati mdogo mdogo na ndio ile tuliyofanyia tathmini. Lakini bajeti halisi itakuja baadae na fedha hii tutazitafuta, lakini pia hili si kigezo tunaweza tunawea kushindwa kulipitisha kabisa kama jengo litakuwa hali si nzuri basi tunaweza kukaa na wenzetu wakatupa *Supplementary Budget* ambayo tutaweza kulifanyia kazi hili.

Lakini *priority* kwa mwaka huu ni kujenga Mahakama ya Ardhi Mkoa wa Kaskazini Pemba ambayo fedha yake imetengwa ndani ya eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti: Asante Mheshimiwa naona unanyanyuka tena unajua ulitoa wazo yaani wewe hukupendekeza kwamba tuhamishe wapi kifungu kwa ajili ya kukava hicho ulichokuwa unataka ndio maana hatuwezi hata kulipigia kura, yaani ungesema fedha itoke pahali kadhaa kwa ababu tunapitisha vifungu hapa sasa hivi, ili tupige kura tukubaliane fedha zisiende Pemba zije zifanye hiyo shughuli ya Unguja kwanza. Labda ingekuwa inaingia akilini ingawa sidhani kama ni njia nzuri sana kwa hiviyo ningeshauri sana tuendelee Mheshimiwa tusipige kura kwenye hili kwa sababu hujapendekeza tuhamishe wapi pesa ili tuweze kukubaliana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nakufahamu sana na mawazo yako na hekima na busara za kiti chako na siwezi kusema hivyo kwa Pemba, Pemba nao wana haki vile vile ni sehemu ya Zanzibar kwa kuhamisha pesa itakuja kitu kama ubaguzi si kitu kizuri, lakini suala haliko juzi la Pemba naweza kusema liko juzi hii leo miaka saba tunapiga kelele.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa lakini nadhani Waziri kajieleza vizuri sana fedha waliyonayo sasa hivi wamelenga Pemba kwanza, hapa tayari jengo lipo halipo katika hali nzuri lakini angalau lipo kule hakuna kitu ndio wamepeleka pesa kwa ajili ya kufanya zile kazi, ndio msingi wake. Mheshimiwa unajua hoja yako ni nzuri sana tu wala haina matatizo, ni nzuri iko *valid* sasa lazima tuwape na wao nafasi kwa sababu yenyewe ndio hiyo hiyo ipo kidogo kwa hivyo tutaitumia na tutaipangilia vizuri tu. Kwa hivyo basi, ngoja tufanye kabisa huku Pemba ambako hakuna kabisa halafu baadae tutarudi tutakuja kurekebisha hapa tunaweza labda wakasema Serikali watafanya ukarabati na nini ili

kuweka katika hali nzuri. Njia inayofikia hapo kuweka vizuri, njia kwanza sehemu tele hapa ni mbovu kwa sababu ya mvua zilizopita hizi tunajua sote lakini tuje na hoja pia tuivumilie Serikali kidogo, mzigo ni mkubwa lakini ndio wetu sote mimi wewe naomba tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimekubali kuchinjwa tuendelee.

Kifungu PN0102 Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi 2,515,001,000
Kifungu PN0105

Mhe. Mwenyekiti: Nitakupa tena mwanzo Mhe. Jaku Hashim Ayoub, halafu Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Simai Mohammed Said sijamsikia, Mhe. Suleiman Makame Ali, Mhe. Omar Seif Abeid halafu nitamalizia na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Mhe. Jaku ndio wa mwanzo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana nakuja kwenye suala la maji HN01050106 Uimarishaji wa Miundombinu Maji Vijijini ikiwemo vijijini kijiji cha Michamvi. Mhe. Mwenyekiti, kanijibu sana Mhe. Waziri na nimshukuru sana kanielimisha, lakini Mheshimiwa ndio yale niliyoyarudia tokea dunia kuanza hali tete juzi baada ya kumhadithia Mhe. Waziri kapeleka gari mbili tu za maji leo Ramadhan ya kumi na moja, natumia shilingi 60,000 kwa gari moja tu kupeleka Michamvi. Juzi nimegharimika na *pump* ya Bwejuu pesa si kidogo na anajua Waziri katika mtu ninayeumia na maji ni mimi nilisema kila kitu maji hata aya ya *quran* jana nilitumia nikauliza watu wa Michanvi wamekosa nini magari mengine wanapeleka ya maji, vijijini wale mpaka leo hawajapelekewa maji mwaka jana hawakupelekewa, mwaka huu baada ya kumhadithia Waziri kafanya jitihada zimekwenda gari mbili na kuna Michamvi mbili.

Juzi nimetengeneza pampu ya Bwejuu Mamlaka ya Maji shahidi, juzi tena nyuma yake Jambiani na maji ya kule ni machungu hebu Waziri kweli Serikali imekosa kutoa milioni 250 hivyo hivyo nikashauriwa na Wizara hiyo hiyo…

Mhe. Mwenyekit: Mheshimiwa nafikiri utakuwa umeshaeleweka tumpe Waziri tu labda akujibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub tumekuwa tukiongea kila siku tulikuwa tunawasiliana na ndio maana hata nilivyosimama pale nafikiri katika watu niliowapa shukrani za pekee mmoja alikuwa ni Mhe. Jaku kwa juhudi kubwa anayoichukua kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Lakini namuomba Mhe. Jaku asisahau juhudi hizi anazozichukua pia anatafuta fadhila kwa Mwenyezi Mungu sisi tunazitaka na yeye anazihitaji, lakini pia nataka kumwambia katika kufanikisha hilo Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji *ZAWA* tumekuwa tukishirikiana nae siku hadi siku katika kutekeleza hili na ndio maana ili kuwapelekea wananchi wa Michanvi maji tumechimba visima vya Ras al Khaimah tumejenga tangi kwa ajili ya watu wa Michamvi, lakini zinahitajika bilioni 100.8 ili kukamilisha hilo. Wizara yangu tayari imeshaanza kulipatia ufumbuzi na Serikali imeanza kutoa fedha kwa baadhi ya vifaa, lakini naomba niwahakikishie kuna fedha ambazo pia tunazitarajia katika kukamilisha visima hivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwenyezi Mungu akujaalie uzidishe subra na uendelee kuhudumia wananchi wako wa Paje na sisi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakakavyotujaalia tutaweza kuwahudumia kama unavyosema mwenyewe tunaleta maji japo unasema hayatoshi. Lakini tunajitahidi na *inshaallah* Mwenyezi Mungu kwa sote mimi na wewe na wengine wote na Mhe. Rais kwa dhamira yake ya kufanya juhudi mbali mbali basi

wananchi wa Michanvi iko siku maji watapata na tutasahau hayo, ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa utulivu wake lakini nilisema humu ndani mna milango mitatu ya kuingilia Jimbo kutoka Ikulu, Jimbo kutoka Viti Maalum, Jimbo la Wananchi, hii mimi ndio ajira yangu waliyonituma na mimi si kazi yangu kupeleka maji, mimi wamenituma kule au wamenichagua kuja kuwatetea matatizo yao. Leo kama dawa hapana nitafutwe mimi, njia mbovu nitafutwe mimi, buku nitafute mimi, chaki nitafute mimi. Juzi tu kimekauka kidonda cha Bwejuu Mamlaka yake shahidi lakini bado …

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja hiyo hiyo ya maji Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja zinahitajika milioni 250 tu kwa nilivyokaa na Mkurugenzi Mkuu na mimi niko tayari kuchangia katika hizo milioni 250 wananchi wanaumia na mimi naumia na magari vibaya, ukiandika hesabu hiyo kwa mwaka shilingi ngapi, kwa hivyo mimi niko tayari tukae pahala mimi na yeye nichangie na Serikali ichangie.

Mhe. Mwenyekiti: Ngoja akujibu basi Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, narejea tena dhamira ya Serikali hii ni kupeleka maji safi na salama kwa kila mwanachi wa Zanzibar na kwa juhudi za Mhe. Rais na juhudi zetu na *inshaallah* nimerudi kwamba Mwenyezi Mungu atatusaidia katika hili. Nimesema katika utaratibu ambao sisi kama Mamlaka tumejipangia moja ni sehemu ya Michanvi ambayo maji yanapelekwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alinieleza nasema hata jana kanipigia simu ya mwisho nafikiri saa nne kasorobo tatizo kwamba magari yanayopeleka maji hayatoshi. Tunajitahidi kufanya hivyo lakini tumesema ingawa tuna kidogo tugawane kidogo kidogo, kuliko kuwa na kingi tukaanza kugombea. Sasa hivi hatuna kwa hivyo hichi kidogo tulichonacho naomba Mhe. Jaku uridhie tugawane kidogo kidogo kila mtu apate kwa namna yake, lakini kila mtu angalau apate lile tone la maji na kuweza kujikimu. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Jaku uniridhie na unifahamu katika hili, nakuomba kaka yangu ndugu yangu uniridhie katika hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, huu mzigo si mdogo na mimi kwa kupiga hesabu mamlaka wenyewe walitaka ushauri wakanambia nichimbe msingi nikauchimba kwa gharama si ndogo kwa maji ya pwani kuyazalisha yawe matamu mwaka wa pili huu, pesa si kidogo nimezitia pale na hakuna kitu. Mheshimiwa angetoka tu akenda kufanya ziara akamuuliza Sheha natumia shilingi ngapi mimi kule maana yake sio najisifu tu humu ndani ninachokitumia aende akaangalie. Juzi namwambia mimi nimetengeneza pampu ya Bwejuu, Juzi tena Jambiani, nyuma yake ilikuwa Muungoni sasa huu mzigo haliko hilo moja tu huko jimboni kuna mengi.

Sasa namuomba huu mzigo auchukue kipindi cha Ramadhan tupokezane angalau achukue yeye hizi zilizobaki mimi nipumzike kidogo nivute pumzi hilo dogo tu. Mhe. Hamza Hassan Juma ana gari hapa tunaweza kukodi gari lake Serikali mkamlipa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hebu muahidi kidogo Mhe. Jaku mpe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, wala hakuna shida mimi kwenda kufanya ziara kwake nafikiri aikuwa haja-*request* tu bahati nzuri

Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwangu kila anachokitaka vingi anavipata. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Swaumu! swaumu!

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishari na Mazingira: Ila Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana hili alikuwa hajanambia kwa hivyo sasa hivi niko tayari.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo lakini nilikuwa nataka kusema kidogo tu nusu sekunde uniruhusu kweli ukitaka kitu mtangulize mwanamke mbele utafanikiwa ahsante.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba hatuna muda mwingi tutamaliza lakini nachukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira anafanya kazi nzuri hasa kwa Jimbo la Welezo ambalo ndio jimbo lenye visima vingi kwa Zanzibar hii...

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sasa Mhe. Mwenyekiti, pampu ilikuwa haifanyi kazi tukanunua pampu. Lakini kinachonishangaza hizi pampu Mhe. Mwenyekiti, kila siku zinaharibika na wananchi wanakuwa wanapata shida, huwa tunatatua tunanunua pampu na nini na Mhe. Waziri amefanya. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuondokana na kadhia hii jimbo langu la Welezo ndio lenye visima vyote vya vinavyonywesha maji mjini hasa kuna kisima kimoja kipo tenki moja la *reserve* liko pale hospitali ya wakoma, pale zamani hospitali ya Welezo kubwa sana lilikuwa na mradi wa *JICA* linakaa pampu kubwa. Mhe. Mwenyekiti, kisima hicho hakikauki maji wala hakitokauka sasa

wananchi wangu wamenituma nije kusema watobolewe ile paipu na wao wapewe.

Kwa sababu kwa nini maji yapo kwao yanawapita wao yanakwenda mjini na pampu hiyo, kisima hicho hakiharibiki wala maji hayakauki lakini yanawapita yanakwenda mjini. Sasa ninachotaka Mhe. Waziri kwa huruma yake namjua ni mama na yeye hapendezewi kuona maji yako Welezo lakini wana Welezo hawapati maji na leo ni siku ya mwezi wa Ramadhan aniahidi atawaamuru watendaji wake wafanye utaratibu wa kutoboa lile tangi ambalo halikauki maji na wananchi wangu wa Waelezo wapate na thawabu nyingi atazipata kama anazozipata. Mhe. Mwenyekiti, naomba ahadi hii.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh ni mkwezi na mkulima Mwakilishi wa jimbo la Welezo. Kwanza ananifurahisha sana kwa sababu najua anapenda maslahi ya sisi kinamama maana yake kama maji hakuna shida kubwa tunayo sisi, kwa hiyo namshukuru sana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nimeshakwenda nae katika maeneo yake tumeshatembelea visima kuna kazi za ziada tumefanya maji kidogo kidogo anakiri kwamba yanatoka. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba vianzio vya maji karibu vyote vimo ndani ya Mkoa wa Magharibi, kwa hiyo Welezo ni sehemu kubwa maji yapo, lakini tukisema ndugu yangu Mhe. Mkwezi na Mkulima tukiacha maji yaingie Welezo tutoboe bomba, kwanza tutakuwa tumeharibu miundo mbinu lakini la pili maana yake kama tutakuwa hatuwaonei huruma watu wengine ambao maeneo yao hawana maji. Kwa hiyo, mimi bado narudi ingawaje tuna kidogo tuendelee kugawana kidogo kidogo watu wa

Mji Mkongwe, watu wa Rahaleo, watu wa Michezani waendelee kupata maji kutoka visima vya Welezo, wakati na nyinyi wenyewe mnapata lakini uhalisia naomba basi tutafuatana mimi na yeye tena tutaangalia na tutaiangalia programu ya ugawaji maji ili tuweze kulishughulikia suala hili.

Mhe. Spika: Mhe. Hassan Khamis Hassan mfuatane na Waziri ili ukamuelekeze hicho unachotaka kifanyike.

Mhe. Hassan Khamis Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nachukua kauli ya Waziri kwamba tufuatane twende kule tukaangalie jinsi gani wana Waelezo watapata maji namuamini, nampenda sana na naamini kwa umahiri wake ataweza kutekeleza hasa ukizingatia ahadi hiyo ameiweka leo siku ya mwezi wa Ramadhan naomba tuendelee.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru na mimi wakati nachangia nilichangia kwa hisia…

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu chako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nasimamia kwa kifungu cha SN010501

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ambayo ameisoma Mhe. Waziri ameongea mambo mengi juu ya masuala ya maji lakini pia alizungumzia katika umuhimu wa kuweka mji mpya Tunguu pamoja na Jumbi lakini kwa ujumla kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, suala la maji katika majumuisho yake sikupata kauli ya uhakika ambayo mimi kwa upande wangu, pamoja na wananchi wangu hasa kwa upande wa Tunguu pamoja na Dunga na Unguja Ukuu. Sasa nilitaka *commitment* yake juu ya maji ya Unguja ambayo yanakwenda mpaka kwenye kisiwa cha Uzi pamoja na maji ya Dunga na Tunguu yenyewe hasa. Muhimu

kwamba kwa hili nitakaa nae sambamba kwa kutambua kumrahisishia yeye kuna mualiko ambao nitamualika Makamu wa Pili kuja jimboni na mualiko tayari ameupokea, sasa nataka anihakikishie tu katika haya yote na yeye atapanda katika safari yetu na yale yote ambayo yaliyozungumzwa tuko nao pamoja kwa sababu tukija kuzungumza kwa hapa itakuwa ni mengi kutaja *one by one*. Kwa hiyo nilitaka uhakika wake basi kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said, Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu jibu lake kama ifuatavyo.

Ni kweli kauli aliyoizungumza katika maeneo ambayo Kikungwi, Kibele na kwengine, ambapo alilalamika kwamba maji hayapo naomba nimwambie Mheshimiwa tunajitahidi kufanya kazi lakini kwa sababu eneo lenyewe wakati tumezungumza mimi na yeye kipindi nyuma nilimuangiza Naibu Waziri wangu akaenda kutembelea na alivyorudi akaniletea mrejesho. Lakini kama tunavyojua suala la upatikanaji wa fedha na wakati mwengine mambo mengi kwa sababu kila mtu anahitaji maji ndani ya jimbo lake.

Tumejitahidi kupeleka maeneo mengine lakini mengine bado hayajafika, lakini naomba nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kujitahidi tutaendelea kufanya ziara jimbo hadi jimbo, yale ambayo yatakuwa ndani ya uwezo wetu kwa bajeti hii basi tutaweza kuyafanyia kazi, lakini yatakayokuwa nje ya uwezo wetu kwa sasa hivi tutakuwa bado hatuwezi kuyafanyia kazi.

Lakini katika maelezo yake alizungumza eneo la Tunguu, eneo la Tunguu kuna maeneo maji tayari yapo, kuna maeneo bado hayajafika, lakini umeme halikadhalika, umeme bado tunaendelea kwenda nayo na eneo kubwa tumeshafikisha umeme. Eneo ambalo umeme haujafika pia basi pia tutaufikisha lakini kwa

mujibu wa kila fedha zitakapoweza kupatikana, ningeweza kuwaahidi Baraza lako lote kwamba ningeweza hata leo kwa sababu hata mimi dhamira njema sitaki wananchi wangu wateseke. Lakini haya mambo yanakwenda kwa mipangilio kwa hiyo naomba aniamini na kwamba haya tutayafanyia kazi na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atusaidie kabla ya miaka mitano basi tuwe tumemaliza hizi changamoto ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mwenyekiti, namshukuru kwa maneno mazuri lakini moja nilichoomba ni kwamba katika ziara ambayo atakuja kuifanya Makamo wa Pili niliyomualika nimetaka na yeye mwenyewe aambatane na sisi kwa sababu kwanza huo mualiko aliosema yeye wa Naibu Waziri hakumuelekeza yeye, ndio mimi niliyemuomba Naibu Waziri kuja kukutana na sisi na tuweke *hansard* sawa. La pili, kwa vile Naibu Waziri alifanya ziara katika jimbo letu, tulikwenda pamoja mwaka mzima na sijaona maendeleo yoyote, sasa nataka Waziri mwenyewe anipe kauli yake ataambatana na sisi pamoja na Makamo wa Pili katika ziara yetu katika Jimbo la Tunguu, ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Simai Mohammed Said kwamba sina shida na mimi bahati nzuri mnajua wengi kwamba mfuatiliaji, kwa hiyo nitaambatana na wewe katika ziara yenu mara tu mtakaponiambia, niko tayari kufuatana na nyinyi.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri dada yangu na pengine huenda akawa shemeji yangu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilitarajia kwamba Mhe. Waziri atanijibu swali nililomuuliza jana kuhusu suala la umeme kule Ndagoni. Mhe. Mwenyekiti, nipo kwenye kifungu cha HN01050112 Uimarishaji na Uwendelezaji wa Miundo Mbinu ya Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba Ndagoni ndio kwenye roho ya Pemba kwenye miundo mbinu ya umeme, lakini Ndagoni hakuna barabara hadi sasa na ndio kwenye roho kuu ya Pemba kwa kupitia umeme uliotoka Tanga na kusababisha siku nyengine mpaka wale askari wanaokwenda kulinda miundo mbinu ya umeme…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda hoja yako usituhutubie unataka Waziri akusaidie vipi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ndio Mheshimiwa nataka nieleze kidogo aweze kunifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana usijenge hoja anafahamu kwa sababu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka ufafanuzi kwa sababu nilimuuliza kwamba atashirikianaje na Wizara ya Miundo Mbinu pamoja na Tawala za Mikoa ili kuhakikisha kwamba barabara ile ya Ndagoni imetengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu kuna miundo mbinu ya umeme. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Suleiman Makame Ali shemeji yangu kwa Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) swali lake kama ifuatavyo. *(Makofi)*

Kwa kuwa tumezowea kufanya kazi kwa mashirikiano makubwa na Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, lakini na Wizara ya

Ujenzi na Mawasiliano, basi nimuombe tu nilimjibu pale hakunisikia tutakaa pamoja na sisi tutahusika ili kuona barabara za kwenda kwenye miundo mbinu ile zinatengenezwa. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana, sana, sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nasimamia kifungu HN01050108 Uimarishaji na Kujengea Uwezo *ZAWA* kujiendesha kibiashara. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba wale watoto *ZAWA* kwa upande wa Pemba uwezo wao wa kujiendesha ni mdogo, kwa hiyo nilitaka nijue ile mikakati yao mara hii ya kuweza kuisaidia kwa upande wa Pemba wakaweza kujiendesha kwa sababu hawalipwi bili ya maji maeneo mengi hayapati maji. Kwa hiyo, Mhe. Waziri vipi mara hii kwenye bajeti hii *ZAWA* Pemba tutaweza kuwasaidia. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid wa Jimbo la Konde swali lake kama ifuatavyo.

Ni kweli amenipa mchango wake wa maandishi na alizungumzia swali *OC* katika Ofisi za *ZAWA* Pemba. Nataka nimhakikishie Idara yangu kule Pemba haina hata shida sasa hivi kwa sababu kila wanapohitaji basi hata kama una tatizo unajua nikate wapi lakini uhakikishe kule Mamlaka ya Maji Pemba inafanya kazi. Nataka nikwambie katika pahala ambapo maji naweza kusema kwamba yapo kwa *almost 90 percent* ni Pemba na wanafanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia hadhara hii, kupitia Baraza lako Tukufu na kupitia wananchi wanaonisikiliza naomba niwasifu sana watu wa *ZAWA* Pemba kwa kazi kubwa na juhudi wanayoifanya kuhakikisha wananchi wa Pemba wanapata maji salama. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru lakini ningeomba kama hivyo anavyosema ndivyo basi na Konde pale yeye anapajua nyumbani, lakini hata pale kwangu maji hamna basi wafanye bidii ili na mimi pale maji yanifike. Ahsante sana tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa amekusikia atalifanyia kazi. Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mimi nasimama kwenye kifungu HN01050106 Uimarishaji wa Miundo Mbinu ya Maji Mijini na Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nawasilisha kutoa maoni Mhe. Waziri nilimwambia kuhusu tenki la Chanjamjawiri ambalo nina maeneo makubwa sana pale na kwa kweli imekuwa kadhia kubwa sana hii kwa sababu mtu ambaye anatoa maji pale na pampu inaharibika siku zote. Nikamuomba Waziri kwamba aniwekee tenki ili maji yapatikane kwa muda wote sikupata maelekezo yake naomba taratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tangi la Chanjamjawiri.
Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, Meya wa Jimbo la Chake Chake swali lake ambalo karibu kila *section* ameniuliza lakini naomba nimjibu.

Kwamba mimi binafsi naona umuhimu na bahati nzuri nimekwisha kwenda katika eneo husika na nimejua kwamba ile pampu ya kufanyia kazi *through* ina shida kwa sababu mwisho inapata joto kali na kuweza kuungua kwa haraka na sasa tupo kuweka pampu mpya. Tumeona umuhimu wa kujenga tangi lakini lazima ukubali kwamba ujengaji wa tangi ni gharama tumeliweka katika mpango na mara tu tutakapoweza basi tutalijenga tangi hilo, tunatamani visima vyote viwe na matangi lakini kama nilivyosema awali wakati mwengine uwezo unatushinda. Lakini kwa sababu mji wa Chake Chake ni mji wenye hadhi na mji ambao unaendelea kupangwa basi *priority* tutaona kuiweka katika eneo hili, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niseme namsifu waziri kwa kazi zake nzuri pamoja na Afisa Mdhamini wetu wa maji wakati wote huwa anavaa *rainboot.* Mimi mwenyewe ni shahidi wa kumuona anahangaika kama haya mambo ya tenki ni mambo makubwa mpaka yamfike waziri, pamoja na majibu yake waziri lakini kwa kweli pale pahala panaendelea kujenga na kwa kweli muda umeshakuwa mkubwa sana. Mimi ningeomba waziri kwa sababu ilani ya miaka 5 tunabakisha miaka 3 hebu nieleze kidogo ilani ya mwaka huu au mwakani utanijengea tenki kwa sababu na mimi nipate angalau kujilabu kule nyumbani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake kama ifuatavyo.

Kwamba ndani ya bajeti ya mwaka huu ujenzi wa tenki la Chake Chake haupo, lakini nikasema *priority* tuliyoiweka kwa sababu tuna fedha za wafadhili ambazo tunazitegemea kuzipata ndio maana nikasema naomba *inshaallah* Mwenyezi Mungu atusaidie basi swali hilo tutaweza kulifanyia kazi katika uimarishaji wa

maji mjini na vijijini. Basi swali hilo tukaona tutalipa *priority* na ndio maana nikasema katika kikao mbele *priority* basi hilo tutaliweka.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpe pongezi tena Waziri pia kwa sababu Waziri mwenyewe amelelewa Chake Chake, tumewahi kuokota maembe yale alfajiri pamoja naomba tuendelee namfahamu vya kutosha. *(Makofi)*

Programu ya Usimamizi wa Huduma Za Maji na Nishati

	Jumla	41,438.242
SN010601	Programu kuu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi	

Mhe. Mwenyekiti: Nampa nafasi ya mwanzo Mhe. Simai Mohammed Said halafu anafuatia Mhe. Suleiman Sarahan Said, halafu Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza pia nimekuona

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati nachangia nilizungumza kuhusiana na ramani ya Zanzibar vituo vyetu ambayo inawezekana nikasema kutokana na muda wa kuwa imeshapitwa hasa kutokana na mambo mawili makuu, moja ni mabadiliko ya tabia nchi na pia masuala ya *land reclamation.* Sasa mwaka jana pia nilizungumza katika maoni yangu nazungumza kwenye mchango wangu nilirudia mwaka jana pia katika bajeti niliulizia suala hili, hasa Mhe. Waziri wakati anafanya majumuisho yake hakunipa taarifa kamili juu ya suala hili juu ya ramani ya visiwa vyetu ambayo ina umuhimu pia

kuzidi kuitambua hasa. Nilikuwa naomba maelezo ya kina ili niweze kuridhika hapa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Simai Mohammed Said, Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu, swali lake kama ifuatavyo.

Wakati tunatoa ufafanuzi nilisema sasa hivi ramani za miji kutokana na mabadiliko ya tabianchi kwanza kikawaida ramani ya miji inabadilika kila baada ya miaka 10. Kwa hiyo, ukizingatia haya mabadiliko ya tabianchi lazima tuyafanyie *refer*, sasa hivi nikasema Wizara yangu kupitia Upimaji wa Ramani wameanza kufanya zoezi la *drawing* kwa sababu ya kufanya utayarishaji wa *map* mpya na hizo ramani mpya. Suala hili sasa hivi tayari limo katika hatua za mwisho na kazi inaendelea na imeshafanywa, kwa hiyo nafikiri hakuwa ananisikiliza au alikuwa ametoka, lakini naomba niseme kwamba nilijibu vizuri na nafikiri ramani hiyo itatoka mara tu shughuli hizo zitakapomalizika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza nimthibitishie Waziri wakati anatoa hotuba yake nilikuwepo lakini maneno anapoyatoa wakati mwengine huwa kama anayatafuta sijamsikia vizuri, naomba tuendelee.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Mimi nasimama kwenye HN01060101 Utaratibu na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu fungu lililotengwa ni kama 1,440 lakini nilikuwa namwambia Waziri kwa miaka mingi sana katika Kisiwa cha Pemba hakijapata mabadiliko ya Tabia Nchi kama mvua na mabadiliko mengine. Katika ratiba yake hii

ambayo nimeiona hapa nilikuwa kitabu hichi kimetunga kabla ya mazingira haya yaliyotokea amejipanga vipi Waziri kuhusu habari ya matokeo ya baadae.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, Meya wa Jiji la Chake Chake, swali lake kama ifuatavyo.

Kuna vitu unaweza kujipanga katika madadiliko ya Tabia Nchi kwa maana ya kuweka mikakati lakini kuna mambo huwezi kuyapanga ambayo ndiyo tunaita maafa (*disaster*). Katika mikakati wizara yangu kupitia Mamlaka ya Mazingira *(ZEMA)* na Idara ya Mazingira ndiyo maana inahamasisha suala la ukataji miti, upandaji mikoko katika maeneo ya bahari, lakini kuhifadhi vyanzo vya maji, kuondoa kuchimba ovyo mchanga, vifusi, mawe bila ya utaratibu. Ndio maana wizara sasa hivi ilikuwa inasimamia lakini inaendelea kusimamia kikamilifu kwa sababu ya kuondosha haya matatizo ambayo tunaona yanatokea.

Mhe. Mwenyekiti, mengine niseme ni majaala ya Mwenyezi Mungu ambayo kwa kweli hatuwezi kusema kwamba tutayawekea mikakati na hatujui saa ngapi wala lini yatatokea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nakubali maelekezo ya Mhe. Waziri kwa maneno yake. Lakini mimi nilikuwa nazungumzia kwamba katika mvua za mara hii hasa naweza kusema maeneo ya mjini ambayo tayari yana maeneo yamejengwa ambayo yalikuwa yana *land slide* yale ambayo ya *town* kama tukisema Michakaeni ndiyo kwenye mnara mkubwa wa *TTCL* na mambo mengine. Mlima ule unateremka na labda Manispaa waliona kama kuna watu walijenga vibanda kwa ajili ya labda mlima utazuilika lakini mlima una miti mikubwa pamoja na ule mlima wenyewe. Nazungumzia eneo kama lile umejipangaje

kuinusuru ile mitambo pamoja na nyumba zilizopo juu katika kona ile ya Michakaeni.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu tena Mheshimiwa swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli utamaduni wa watu wetu hasa kwa maeneo yenye milima ukiangalia Chake Chake yenyewe au kwa maeneo ya Pemba kwa ujumla watu hawaja- *experience* shida iliyotokea mwaka huu kwamba juu watu wanajenga, chini watu wanajenga kwa sababu haijawahi kutokea kwa Zanzibar kwa miaka yetu hata siku za nyuma, lakini kwa miaka yetu ya uhai ambayo tupo haijawahi kutokea. Kwa hivyo watu wamezoea kupanga katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili naomba nilibebe nikae na Kamati ya Maafa tuliangalie kwa kina suala hili tunalifanyaje, kama tunaweza kuhamisha vijiji vyote vilivyokuwa mabondeni au kama kuna utaratibu mwengine basi mimi naomba nilichukue kwa ushauri na tuweze kulifanyia kazi kwa pamoja kama serikali. Hili linahitaji upeo mkubwa, linahitaji umakini mkubwa na linahitaji kufanyiwa kazi kwa busara zaidi. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, Waziri suala alilosema ni kubwa pamoja na serikali kwamba tutalifanyia kazi. Naomba tuendelee.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kuuliza swali kidogo. Mimi nasimamia kwenye fungu HN01060102 Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya kadhia nzima ya bahari inavyokula ardhi katika eneo la Msuka na nilishawahi kuzungumza na Waziri wa Tawala za Mikoa kuhusiana na kadhia ya pale kwa sababu hapo mbele kuna kituo cha KMKM ambacho nacho pia kimeshaathirika kutokana na huo mmong'onyoko mkubwa wa ardhi uliosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mimi nilitaka kumuomba Waziri aniambie ni lini tutakwenda pale pamoja na timu yake ya wataalamu waende wakaone jinsi ya mabadiliko na maharibiko yaliyotokewa pale ili watalamu wale waweze kupendekeza njia nzuri ambayo tutaweza kulihifadhi eneo lile lisiweze kuendelea kuathirika na kile kituo cha KMKM kikaendelea kuwepo na wananchi wakaweza kuwa salama na maji ya bahari. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Ardhi je, utaweza kwenda nae Mheshimiwa na wataalam wako?

Mhe Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo.

Ameniuliza ni lini? Mimi tukishakupanga ile safari yetu na Mhe. Suleiman Sarahan Said, Meya wa Jiji la Chake Chake, basi naomba na yeye tuipange kwa pamoja ili tukenda kule niweze kuyatazama maeneo yote mawili.

Lakini pia katika hili Mhe. Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba Wizara yangu Mazingira sasa hivi inafanya kazi ya kupitia maeneo ya fukwe ili kunusuru hali kama hizo ambazo zitaweza kujitokeza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Omar Seif Abeid nafikiri umeshapata majibu. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kupata ufafanuzi kidogo kwa hii hoja ambayo niliizungumza kwa niaba ya Kamati lakini na mimi pia ni sehemu ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kukubali lile ombi langu la kumtaka Mkurugenzi wa Mazingira kwenda kufuatana na mimi na kwa bahati nzuri pia na Mhe. Waziri wa Habari na yeye vile vile ile Skuli ya Faraja ni Skuli yetu kwa pamoja. Tunashukuru kwa kuwa umetuagiza kwamba tufuatane na Mhe. Waziri wa Elimu nadhani itakuwa ni jambo la faraja zaidi, kwa kweli hilo tunakushukuru. Sasa kabla ya hizo ziara za Pemba nafikiri tungeanza na hii ya Unguja kwenye Skuli ya Faraja ili kwenda kuiokoa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaja kwenye hoja yangu nataka nitoe masikitiko kwa serikali na zaidi Afisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, hoja aliyoizungumza Mhe. Omar Seif Abeid kuhusu suala la Visiwa vya Msuka na sehemu nyengine kuingiliwa na maji, masuala haya kwa Zanzibar peke yetu kuweza kuyakabili kwa kweli ni matatizo makubwa sana. Masuala kama haya tunatakiwa tushirikiane kusaidiana na mashirika ya Kimataifa.

Mimi ni mwanachana wa *NGO's* hapa Zanzibar ambayo inayohusiana na mazingira. Safari hii nilipata mualiko wa kwenda Mexico, lakini kwa bahati mbaya sana sikumuona Afisa yeyote kutoka Zanzibar. Masuala kama haya tunapokuwepo kama kule kuna mashirika kuna taasisi tungeliweza kutengeneza hoja zetu

zikaingizwa katika programu za kimataifa tukaweza kupata misaada mbali mbali. Hili nilikuwa naomba kwa kweli mikutano inaendelea 10 naomba sana Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais basi katika mikutano ile tusiikose na wataalamu wetu hawa watakapokwenda kumsaidia.

Nakuja katika hoja Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nililekeza katika kadhia iliyojitokeza katika jimbo la Mtoni juu ya athari iliyojitokeza kwenye mradi wa *Mtoni Marine.* Kadhia ile ni kubwa ni kadhia ya kitaifa na iko haja sisi kama Baraza la Wawakilishi serikali kutuletea ripoti kamili kuhusu nini kitaweza kufanyika pale. Kadhia yenyewe ninayoikusudia zile nyumba za wananchi wa mtoni karibu nyumba 80 ambazo sasa hivi maji yakijaa zinaingia maji. Tuliomba kwenye ripoti ya Kamati serikali ilete taarifa Barazani ili tuweze kuijadili. Hili Mhe. Waziri alilielezea lakini hakuji-*commit* kwamba labda baadaye itakuja taarifa ya serikali ili kuwasemea wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri *commitment* ya serikali kuhusiana na suala hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Hamza Hassan Juma Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano, Mwenyekiti mahiri, ametoa ushauri, ushauri nimeupokea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sisi tumesema tufanye kazi ya awali basi ushauri tunaupokea nitakaa na serikali tutaufanyia kazi na hatimaye tutafikia lengo. Mimi nimuombe tu kwamba kama alitaka kuona kwamba uhalisia wa eneo lile labda niseme, naomba Mhe. Mwenyekiti nipe dakika moja niseme uhalisia wa eneo lile. Maana ukiangalia hapa unachozungumzia ni *project* iliyokuwepo, lakini uhalisia sio *project* tu ni matumizi ya wananchi pia yamechangia kwa asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri mimi mwenyewe nimesoma Kilimo na Mazingira kwa hivyo najua *environmental impact* inavyotokea katika maeneo ya fukwe. Pamoja na mawimbi ya maji kusukumwa na zile *rider,* lakini mikoko pale ukiangalia kwa asilimia kubwa imetoweka lakini matumizi ya wananchi kwenye bahari fukwe ile imekuwa kubwa, kwa hivyo mambo yale yote yanasababisha maji kujaa na mawimbi kuja makubwa. Lakini kwa kuwa Kamati inaendelea kufanya kazi mimi naomba Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla pamoja na Mwenyekiti wangu mpenzi wa Kamati ambaye saa zote tunafanya kazi kwa pamoja, aniamini kwamba hii kazi tutaifanya na yeye kwa sababu muda wote tunafanya kazi kwa pamoja basi tutamshirikisha humu ndani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana sana na Mhe. Waziri, lakini suala la Kamati kushirikiana tunashirikiana vizuri sana. Lakini hili suala kama nilivyosema ni kubwa na ni funzo. Mradi kama ule kwa Zanzibar, sio ule tu yapo maombi mengine ya kufanywa miradi kama ile hapa Zanzibar. Ndio maana nikasema serikali, hatulazimishi kesho au keshokutwa wakae wafanye tathmini halafu baadaye watuletee Barazani, ili tunapokuja kuidhinisha hiyo miradi mengine humu. Ingawa miradi inaidhinisha *ZIPA* lakini katika zile *policy* zetu, katika sheria zetu tujaribu kuangalia ni mambo gani ambayo tumekosea na mambo gani ambayo tuweze kurekebisha ili huko baadae twende vizuri zaidi.

Kamati hatuna tatizo tutakwenda lakini baadae lazima serikali ituletee ripoti ili tuweze kujua halafu tunakuja kutenga sheria zetu huko baadae tujue maeneo gani tunakosea na nini tuweze kufanya. Ni hivyo tu Mheshimiwa lakini tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu siku zote ni sikivu hususan kwenye mambo ya msingi yanahusu mazingira. Kiukweli tunao utaratibu kabla ya kupitisha kwa miradi tathmini ya mazingira hufanywa. Lakini panapojitokeza tatizo zaidi ni wajibu wetu kama serikali kuliangalia tatizo hilo kwa kina ili tupate ufumbuzi. Hasa tukilia maanani umuhimu wa miradi mikubwa inayoendelea ambayo inaleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu ndiyo inayoimarisha uchumi wetu na kuleta haiba na kuvutia katika dunia.

Miradi kama hiyo ni muhimu kuungwa mkono ili miradi hiyo iendelee, lakini wakati huo huo kulinda na kuhakikisha wananchi wetu wanakuwa salama. Ushauri tunaupokea na tutakwenda kuufanyia kazi ili kuona kwa namna gani wananchi wetu wanaathirika ili waishi kwa salama na miradi iendelee ili ilete tija kwa watu wetu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, tunaendelea Waheshimiwa.

Fungu N0.1 Mazingira na	Jumla ya Program ya Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabia Nchi	1,595,431,000
	Jumla Kuu	**47,508,574,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

*(Baraza lilirudia***)**

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa hoja imetolewa naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mimi napenda sana nitoe shukrani zangu za dhati sana, kwanza kwako Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya mpaka tumeweza kupitisha vizuri sana hili fungu. Lakini pia nitoe shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu madhubuti sana na mizito ambayo mmeitoa imefanikisha mwisho tumeweza kupitisha fungu la hii Wizara.

Pia nitoe pongezi zangu kwa serikali kwa mashirikiano ambayo mmeyaonesha katika kulisimamia na kufanikisha upitaji wa hii bajeti. Baada ya hayo machache Waheshimiwa sasa namuomba Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2017/18

Utangulizi

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Baraza lako tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016-2017 na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka 2017-2018.

Mhe. Spika, sina budi kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Subhana Wataala, kwa kutujaalia kuwa na Afya njema, Utulivu na Amani katika nchi yetu vilivyotuwezesha kwa mara nyengine tena kukutana katika kikao chengine maalum cha Bajeti cha Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, na kwa heshima kubwa, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kukamilisha kwa mafanikio makubwa ya mwaka mmoja tangu alipochaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuiongoza nchi yetu kwa kipindi cha pili cha miaka mitano. Sambamba nae, nampongeza sana Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, kwa mashirikiano yake na umahiri wa hali ya juu wa kumsaidia Mheshimiwa Rais anaoutumia pia katika kuongoza shughuli za Serikali hapa Barazani la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu, kuwapa pole wananchi wote waliofikwa na maafa yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha hivi karibuni. Aidha, nachukua fursa hii kuwakumbusha wananchi wenzangu tuendelee kuchukua tahadhari za kujikinga na maradhi ya kipindupindu ambayo yanaweza kujitokeza kutokana na mvua zilizonyesha.

Mhe. Spika,baada ya pongezi na shukrani nilizozitowa naomba nikumbushie kwamba, Uwasilishaji wa hotuba hii utatuwezesha kukidhi matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu 88 (b). Kinachoeleza kuwa moja ya kazi ya Baraza lako tukufu ni "... kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi..." pamoja na kutekeleza masharti ya kanuni 96 (2)-(3) za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012.

Mhe. Spika, **k**uwepo kwangu katika Baraza hili kunatokana na kukubaliwa na Chama changu cha Mapinduzi kuwa miongoni mwa waliopewa fursa ya kusimama kukiwakilisha katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015, uliorudiwa tarehe 20 Machi 2016 kwa majimbo yote ya Unguja na Pemba lakini mimi nilisimama kwa jimbo la Donge. Aidha, nipo hapa kufuatia imani inayoendelea kuoneshwa na wananchi wa Jimbo la Donge kwa Chama cha Mapinduzi na kwangu binafsi, kwa kunipa ridhaa ya kuwa Muwakilishi wao katika chombo hichi muhimu kwa nchi yetu. Nachukua tena fursa hii kukishukuru sana Chama cha Mapinduzi lakini kwa namna maalum, wananchi wote wa jimbo la Donge kwa kuendelea kunipa heshima na imani kubwa na kunistahamilia sana pale ninapotumia muda mwingi shughuli za Kitaifa na wananchi wote wa Zanzibar, nawashukuru sana.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niendelee na uwasilishaji wa Hotuba ambao nitaanza kwa kuwasilisha kwa ufupi, Muundo wa Wizara na Majukumu yake.

Muundo na Majukumu ya Wizara

Mhe. Spika, Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kuundwa na Idara kumi (10), Tume ya Mipango yenye Idara nne (4), Taasisi kumi (10) zinazojitegemea na taasisi nne (4) za Muungano

zinazofanyakazi hapa Zanzibar. Idara na taasisi hizo zinaonekana katika Jadweli nam.1

Mhe. Spika**,** Idara na Taasisi hizo zinatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kwanza kukusanya mapato ya Serikali kutokana na vyanzo vya ndani, kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka nje ya nchi na kusimamia matumizi yake;

ii. Kusimamia rasilimali za Serikali;

iii. Kusimamia mwenendo wa Deni la Taifa;

iv. Kutoa huduma za Uhasibu Serikalini;

v. Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha;

vi. Kuandaa na kusimamia Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye Mipango ya kipindi cha kati kwa maana (miaka mitano) Mipango mahsusi ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini;

vii. Kushajiisha, uwekezaji wa sekta binafsi hasusan kwa wawekezaji kutoka nje ya nchi; n.k.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

Upande wa Mapato

Mhe.Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ilipangiwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya ya jumla ya TZS 824.35 bilioni ikijumuisha TZS 447.23 bilioni za mapato yatokanayo na kodi, TZS 18.02 bilioni ikiwa ni mapato yasiyokua ya kodi...

Mhe. Spika: Samahani Waziri wa Fedha naomba nimpishe Mwenyekiti achukuwe kiti ili nikafanye shughuli nyengine. Mheshimiwa Mwenyekiti karibu.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango ilipangiwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya ya jumla ya TZS 824.35 bilioni ikijumuisha TZS 447.23 bilioni za mapato yatokanayo na kodi, TZS 18.02 bilioni ikiwa ni mapato yasiyokua ya kodi TZS 326.10 bilioni zilipangwa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 33.00 bilioni ni mikopo ya ndani kwa ajili ya kuziba nakisi ya Bajeti.

Matumizi ya Wizara

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Fedha na Mipango ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 157.69 bilioni. Matumizi hayo yanajumuisha matumizi ya Wizara ya Fedha (F01) ya TZS 68.25 bilioni, matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali (F02) ya TZS 83.53 bilioni na TZS 5.91 bilioni ni matumizi ya Tume ya Mipango (F03).

Utekelezaji halisi kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017

Upande wa ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/17, Mapato yaliyokusanywa na Wizara na

kuingizwa katika hesabu za Serikali ni TZS 448.15 bilioni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yaliyokusanywa yanajumuisha mapato ya kodi za ndani ya TZS 365.94 bilioni, mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya TZS 58.6 bilioni, mikopo ya ndani ni TZS 8.1 bilioni na Mapato yasiyokua ya kodi ni TZS 10.44 bilioni. Jadweli nam.2 linaonyesha uchambuzi wa mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017.

Mhe. Mwenyekiti, mapato ya kodi ya TZS 365.94 yaliyokusanywa katika kipindi hichi yamefikia asilimia 108.6 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 82 ya makadirio ya mwaka 2016/2017. Mapato ya kodi yaliyokusanywa yanaonyesha ukuaji wa asilimia 27 ikilinganishwa na mapato ya kodi yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai-Machi 2015/2016 ya TZS 288.56 bilioni. Mchanganuo wa mapato hayo kwa Taasisi ni kama ifuatavyo:

i. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) imekusanya TZS 197.53 bilioni sawa na asilimia 109 ya lengo la Julai 2016-Machi 2017 sawa na asilimia 83 ya makadirio ya ukusanyaji wa mwaka yaliyokisiwa kuwa ni TZS 237.44 bilioni;

ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Tawi la Zanzibar imekusanya TZS 152.7 bilioni ikiwa ni sawa na asilimia 109 ya kipindi cha miezi tisa na asilimia 81 ya makadirio ya mwaka ya TZS 188.80 bilioni;

iii. Fedha zilizopokelewa kutokana na kodi ya mapato ya wafanyakazi (PAYE) wa Taasisi za Muungano waliopo Zanzibar ni TZS 15.75 bilioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya TZS 21.0 bilioni zilizopangwa kukusanywa kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mapato ya nje jumla ya TZS 58.61 bilioni zimekusanywa sawa na asilimia 18 ya makadirio ya mwaka ya TZS 326.1 bilioni. Ukusanyaji wa mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo umeathiriwa na kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya Miradi mikubwa ya Maendeleo iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2016/2017. Maelezo zaidi ya suala hili nitayatoa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Matumizi ya Wizara

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Julai-Machi 2016/17, Wizara ya Fedha na Mipango imetumia jumla ya TZS 104.8 bilioni sawa na asilimia 66.5 ya TZS 157.69 bilioni zilizokadiriwa kutumika kwa mwaka 2016/2017. Mgao wa matumizi kimafungu ni kama ifuatavyo:

i. Wizara ya Fedha (F01) imetumia TZS 29.59 bilioni sawa na asilimia 43 ya makadirio ya TZS 68.25 bilioni makadirio ya mwaka;

ii. Matumizi kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali (F02) ni TZS 72.11 bilioni sawa na asilimia 86.5 ya makadirio ya TZS 83.35 bilioni ya mwaka;

iii. Tume ya Mipango (F03) imetumia jumla ya TZS 3.10 bilioni sawa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka ya TZS 5.91 bilioni. Jadweli Nam.3 linaonyesha uchambuzi wa Matumizi kwa Programu.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA PROGRAMU

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, majukumu niliyoyaeleza yalipangwa kutekelezwa kupitia programu kuu saba

(7) na programu ndogo 16 zinazosimamiwa na Wizara. Kwa heshima naomba kuwasilisha utekelezaji wa programu hizo kama ifuatavyo:

Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Programu hii ni kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na Usimamizi wa fedha za Umma. Programu inahusisha utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kutokana na vyanzo vya ndani na nje ya nchi, matayarisho na usimamizi wa Bajeti ya Serikali, usimamizi wa Hazina, ukaguzi wa ndani na utoaji wa huduma zote za Uhasibu Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, program hii ilitekelezwa kupitia program ndogo tatu (3) ambazo zilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 54.20 bilioni kwa mwaka 2016/2017. Hadi kufikia Machi 2017 prorgamu hii ilitumia jumla ya TZS 18.15 bilioni sawa na asilimia 33.5 ya makadirio ya mwaka. Miongoni mwa Shughuli mahsusi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

i. Kukamilisha kwa wakati utayarishaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018;

ii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ya TZS 389.55 bilioni kama nilivyoeleza awali;

iii. Kusimamia ukusanyaji wa TZS 58.6 bilioni kutokana na Ruzuku na Mikopo kutoka nje;

iv. Kusimamia matumizi ya Serikali ya TZS 410.45 bilioni sawa na asilimia 99 ya makadirio ya TZS 415.02 bilioni zilizohitajika kwa matumizi ya Julai 2016-Machi 2017;

v. Kushirikiana na Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukamilisha zoezi la matayarisho ya ulipaji wa mishahara mipya ili kutimiza ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo hatimae mishahara mipya imeanza kulipwa katika mwezi wa Aprili, 2017;

vi. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika kada mbali mbali za kihasibu ikiwemo mafunzo ya *CPA*, *IPSAS* na *IFRS;* na

vii. Kuunganisha *votes* kumi na mbili katika Kituo Kikuu cha Mfumo wa Mtandao wa Kihasibu *(IFMS)* Serikalini uliopo Wizara ya Fedha na Mipango.

Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la programu hii ni kusimamia mali za Umma na kuhakikisha kunakuwa na tija katika uwekezaji wa mitaji ya Umma. Programu hii inasimamia utekelezaji wa jukumu la usimamizi wa mali za Serikali ambalo huhusisha masuala ya Ununuzi, Utunzaji na Uondoaji wa mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Mashirika yake na Kampuni binafsi. Programu ilitekelezwa kupitia programu ndogo mbili.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla programu hii ilipatiwa TZS 4.66 bilioni sawa na asilimia 70.4 ya TZS 6.61 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa 2016/2017. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha miezi tisa ni:

i. Kusimamia ukusanyaji wa TZS 86.38 milioni ikiwa ni mapato yanayotokana na kodi ya majengo ya Serikali;

ii. Kukusanya gawio la faida *(dividend)* la TZS 1.23 bilioni kutoka katika mashirika ya Serikali;

iii. Kuifanyia mapitio mikataba 12 ya ukodishwaji wa majengo ya Serikali na kupelekea kuongezeka mapato yanayotokana na mikataba hiyo kwa asilimia 51;

iv. Kusimamia ujenzi unaoendelea wa jengo jipya la Ofisi -Pemba litakalokidhi matumizi ya shughuli za kiofisi kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na

v. Kuanza mchakato wa kutafuta Mkandarasi wa Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa upande wa Unguja.

Programu ya Uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo kwa Sekta nyengine, Wizara ina jukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha ikiwemo Usimamizi wa Sekta kwa ujumla, utayarishaji wa Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha pamoja na kutoa huduma za Uendeshaji na kiutumishi kwa Sekta ya Fedha. Lengo kuu la progamu ya Mipango na Uendeshaji wa Sekta ya Fedha ni kuimarisha sekta ya Fedha inayoendana na mageuzi ya kiuchumi. Programu hii ilitekelezwa kupitia program ndogo tatu.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2017 Programu imepatiwa jumla ya TZS 6.78 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya mwaka ya TZS 7.28 bilioni kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kukamilisha mapitio ya Sheria na uandaaji wa Sheria mpya ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(Public Finance Management Act)* nam.5 ya mwaka 2016;

ii. Kukamilisha mapitio na uandaaji wa Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam.12 ya mwaka 2016;

iii. Kukamilisha utayarishaji wa Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa *(Excise Duty Bill)* na Huduma;

iv. Kukamilisha utayarishaji wa Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Stempu itakayoshika nafasi ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam.6 ya mwaka 1996;

v. Kukamilisha utafiti wa kuchunguza sababu inayowapelekea Wananchi wa Zanzibar kutotumia huduma zinazotolewa na Taasisi za kifedha zilizopo Zanzibar;

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kazi nyengine zilizotekelezwa ni:

vi. Kuandaa dhana *(Concept note)* ya Ujenzi wa Ofisi mpya ya Wizara ya Fedha na Mipango itakayojengwa Mazizini Unguja;

vii. Kulipia gharama za ununuzi wa vifaa na huduma za kiofisi ikiwemo; huduma za mawasiliano pamoja na usafi wa maeneo na mazingira ya nje na ndani ya majengo ya Wizara;

viii. Kulipia gharama za safari za kazi kwa Uongozi na watendaji mbali mbali wa Wizara wanaoiwakilisha Serikali na Wizara katika kazi mbali mbali ndani na nje ya nchi;

ix. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi kumi (3 Shahada ya Pili na 7 Shahada ya Kwanza) katika fani zinazoendana na usimamizi wa Fedha na Mali za Serikali;

x. Kulipa madeni kwa vyuo vinavyochukua wanafunzi wa Wizara;

xi. Kuratibu shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba.

Programu ya Usimamizi wa huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inahusisha usimamizi wa matumizi ya huduma zinazotolewa na Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwemo ulipaji wa Kiinua mgongo na Pencheni kwa Wastaafu wa SMZ. Katika kipindi cha miezi tisa, fedha zilizotumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali zimefikia TZS 72.11 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi cha Julai-Machi 2016/2017 na asilimia 86.5 ya makadirio ya mwaka ya TZS 83.35 bilioni. Fedha zilizotumika kwa ajili ya matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu zilitumika kama ifuatavyo**;**

i. Kulipa TZS 13.64 bilioni mafao ya kiinua mgongo kwa wastaafu 1,015 wa SMZ;

ii. Kulipa TZS 9.94 bilioni pencheni ya wastaafu za kipindi cha miezi tisa;

iii. Malipo ya Madai ya Wazabuni wa Serikali ni TZS 8.83 bilioni; na

iv. Malipo kwa marejesho ya Mikopo ya ndani iliyochukuliwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali za Maendeleo ni TZS 11.3 bilioni.

Ufafanuzi wa matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali unaonekana katika Jadweli Nam 4.

Usimamizi wa Deni la Taifa

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya fedha na Mipango inajukumu la kuratibu na kusimamia mwenendo wa Deni la Taifa. Hadi kufikia Machi 2017, deni la Taifa la Zanzibar lilifikia jumla ya TZS 377.10 bilioni ikiwa ni pungufu kwa TZS 21.3 bilioni ikilinganishwa na deni la mwezi wa Julai, 2016 ambalo lilikuwa TZS 398.4 bilioni. Deni la nje ni TZS 270.20 bilioni sawa na asilimia 72 ya deni wakati deni la ndani ni TZS 106.8 bilioni sawa na asilimia 28. Sababu kubwa ya kupungua kwa deni hili ni kulipwa kwa madai ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa SMZ. Aidha, uimara wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola za Marekani imepelekea kutoengezeka kwa kasi kwa Deni la Taifa. Jadweli Nam.5 linaonyesha uchambuzi wa Deni la Taifa hadi Machi 2017.

Usimamizi wa Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango inajukumu la kusimamia upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya matumizi ya Mfuko wa Miundombinu. Kwa mwaka wa Fedha 2016/2017, Mfuko ulikadiriwa kupokea jumla ya TZS 26.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2017, Fedha zilizokusanywa zimefikia TZS 20.95 bilioni ikiwa sawa na asilimia 79 ya lengo la mwaka

2016/2017 na asilimia 105 ya lengo la miezi tisa. Fedha hizo zimegaiwa ili kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi TZS 14.89 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya TZS 18.0 bilioni;

ii. Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Pemba (Chake-Wete na Ole-Kengeja) umepatiwa TZS 360.00 milioni sawa na asilimia 21 ya makadirio ya TZS 1.7 bilioni;

iii. Usambazaji wa Umeme Vijijini (Kisiwa cha Fundo) umepatiwa TZS 1.80 bilioni sawa na asilimia 90 ya makadirio ya TZS 2.0 bilioni;

iv. Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, Elimu Mbadala na Amali umepatiwa TZS 650.00 bilioni sawa na asilimia 41 ya makadirio ya TZS 1.6 bilioni;

v. Mradi wa kilimo cha Mpunga wa umwagiliaji maji umepatiwa TZS 10.00 milioni sawa na asilimia 3 ya makadirio ya TZS 400.00 milioni;

vi. Mradi wa kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji na Mazao ya Baharini umepatiwa TZS 19.00 milioni sawa na asilima 14 ya makadirio ya TZS 140.00 milioni; na

vii. Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umepatiwa TZS 200.00 milioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya TZS 500.00 milioni.

Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi ina lengo la kuimarisha Uratibu wa Mipango ya Maendeleo na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya kitaifa. Programu hii ina programu ndogo tatu. Kwa kipindi cha Julai-Machi 2016/2017 programu hii imetumia jumla ya TZS 949.56 milioni ambayo ni sawa na asilimia 53.09 ya makadirio ya mwaka ya TZS 1.79 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuanza matayarisho ya Mpango wa Maendeleo kwa ukusanyaji wa taarifa za mwelekeo wa hali ya uchumi, vipaumbele vya kitaifa na programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18;

Pamoja na hilo shughuli nyengine zilizotekelezwa ni:

ii. Kukamilisha maadhimisho ya wiki ya Umasikini yaliyofanyika Micheweni mwezi Novemba 2016 ambayo yaliweza kutoa fursa ya kubadilishana mawazo kwa sekta za umma, sekta binafsi na asasi za kiraia kwa kuelewa umuhimu wa ushirikishwaji katika kukabiliana na masuala ya umasikini katika maeneo yao;

iii. Kukamilisha MKUZA III na kuidhinishwa rasmi na Serikali. Aidha, kazi ya uandaaji wa muongozo wa utayarishaji wa Mipango mikakati ya sekta inaendelea;

iv. Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za msingi zinazohusu idadi ya watu kwa wilaya 2 za Pemba ni Wilaya ya Chake chake na Wilaya ya Micheweni;

v. Kufanya tafiti za Tuongee na Watoto na matokeo ya tafiti ya mwanzo yametolewa na kusambazwa;

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine zilizotekelezwa kwa maana ni:

vi. Kuwajengea uwezo maafisa mipango juu ya kuandaa mipango na bajeti za wilaya;

vii. Kukamilisha ripoti ya Idadi ya Watu ya mwaka 2016 juu ya athari za kibinadamu katika rasilimali za bahari na fukwe ;

viii. Kukamilisha Zoezi la uhamasishaji wa ujazaji wa madaftari ya shehia katika shehia 51 za Unguja na Pemba;

ix. Kutayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa MKUZA III na Muongozo wake;

x. Kuandaa na kuchapisha kitabu cha Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2016/17;

xi. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa saba wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini; na

xii. Kutoa mafunzo juu ya dhana ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa maafisa wa Ufuatiliaji na Tathmini na Maafisa Mipango kwa ngazi za Mikoa, Wilaya na halmashauri kwa Unguja na Pemba.

Usimamizi wa Uchumi Mkuu

Mhe. Mwenyekiti, lengo la programu hii ni kuandaa sera madhubuti za kiuchumi. Programu hii ilitekelezwa kupitia programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu na Uratibu wa Mashirikiano Baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya TZS 1.63 bilioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya TZS 2.37 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi hicho shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kufanya mapitio ya moduli ya kifedha *(Financial Programming)* pamoja na kuanzisha moduli mpya ya utabiri wa Faharisi za bei za Bidhaa na Huduma ambayo husaidia kufanya makadirio ya mwenendo wa uchumi;

ii. Kuanza kwa ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali huko Mazizini.

iii. Kukamilisha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya 2014/15 *(Household Budget Survey 2014/15);*

iv. Kutoa mafunzo kwa wadau wa PPP katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shehia za Unguja na Pemba;

v. Kujenga uwezo kwa Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na Maafisa wa PPP katika kuibua, kuendesha na kusimamia miradi inayotekelezwa kwa mfumo wa PPP.

Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango

Mhe. Mwenyekiti, programu hii lengo lake ni kuhakikisha kuwa shughuli za Tume ya Mipango zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Kwa mwaka 2016/2017 ilitengewa jumla ya TZS 777.83 milioni kwa kazi za kawaida na hadi kufika mwezi wa Machi, 2017, programu imetumia jumla ya TZS 578.05 milioni sawa na asilimia 74.3% ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Kazi zilizofanywa

i. Shughuli za uendeshaji wa Ofisi Unguja na Pemba zimeratibiwa kwa kutoa huduma za kiutawala na kuimarisha upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya kiutendaji.

ii. Vikao vitano vimeratibiwa vikiwemo Tume ya Mipango, Kamati ya Wataalam, Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani;

iii. Mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa fani za uchumi, Sera za Umma, Ufuatiliaji na Tathimini pamoja na fani ya ununuzi na ugavi katika vyuo mbali mbali yametolewa kwa maofisa kumi na nne.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/17 KATIKA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZILIZOPO CHINI YA WIZARA.

Mhe. Mwenyekiti, naazia na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la Bodi ni kukusanya mapato ya ndani ya Serikali. Kwa kipindi cha Julai-Machi 2016/2017,Bodi imekusanya TZS 197.53 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya mwaka ya TZS 237.44 bilioni. Mapato haya ni sawa na ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na TZS 150.94 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi cha Julai-Machi 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, hadi Machi 2017, Bodi imepokea ruzuku ya TZS 8.3 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Bodi ikiwa ni asilimia 69 ya makadirio ya mwaka ya TZS 12.00 bilioni. Miongoni mwa Shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kuanza hatua za ujenzi wa Jengo la Ofisi ya ZRB Pemba;

ii. Kuanzisha mfumo wa kuwagawa na kuwatambua walipakodi kimaeneo kwa kutumia vitalu *(Block Management System);*

iii. Kuanza maandalizi ya kuanzisha mfumo wa usimamiaji utozaji wa kodi katika hoteli kwa kutumia mashine za kielektroniki *(E-Tax);*

iv. Kuanzisha mfumo wa usimamiaji shughuli zisizo za ukusanyaji wa mapato;

v. Kuandaa Mpango wa mahitaji ya Mifumo ya Kielektroniki ya ZRB *(ZRB System Mapping);*

vi. Kuandaa na kurusha vipindi 26 katika radio ya ZBC, Chuchu FM, Swahiba FM na Hits FM vya kujenga uwelewa wa kodi kwa jamii na walipakodi; na

vii. Kuandaa vipindi mubashara 12 vya Televisheni katika ZCTV na ZBC.

Hadi Machi, 2016 mamlaka imeweza kukusanya TZS 659.01 milioni na imepokea ruzuku ya TZS 187.50 milioni kutoka serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi halisi kwa kipindi hicho yalifikia TZS 1.25 bilioni ikiwa sawa na asilimia 30.59 ya makadirio ya mwaka. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo:

i. Kushiriki ziara za uhamasishaji ndani na nje ya nchi;
ii. Kuandaa makongamano ya uwekezaji na "*Diaspora*", katika nchi ya Comoro na Uturuki;

iii. Kuhamasisha uwekezaji kupitia maonyesho ya biashara ndani ya Zanzibar na Afrika Kusini kwa kuandaa mkutano na wawekezaji kwa lengo la kufanikisha uwekezaji nchini;

iv. Kukamilisha uwekezaji wa miradi 13 yenye thamani ya dola za ki-Marekani 132.38 milioni zilizowekezwa katika sekta tofauti. Miradi hiyo inakadiriwa kutoa ajira kwa wananchi wapatao 625. Kiwango kikubwa cha mitaji imeonekana kuwekezwa katika sekta ya Utalii eneo la Hoteli na Mikahawa;

v. Kuendeleza uwekaji wa miundombinu kwa mujibu wa mpango wa matumizi ya ardhi katika eneo la Fumba. Aidha, kwa mashirikiano na "*Master Developer'* (*Bakhressa Group of Companies*), Mamlaka imeweza kulipa fidia kwa watu 107 katika maeneo yatakayopitishwa miundombinu ya barabara; na

vi. Kujenga barabara zenye ukubwa wa kilomita saba kwa kiwango cha lami pamoja na kusimamia ujenzi wa nyumba 150 za makaazi katika mji wa hadhi ya juu (*Up Town Living*) unaojengwa Fumba.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*)

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) ni kutoa hifadhi kwa wanachama wake pale wanapostaafu au wanapopatwa na majanga ambayo yatapelekea kutoweza kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko ulikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 71.37 bilioni ikijumuisha TZS 49.17 bilioni ikiwa ni michango kutoka kwa wanachama, TZS1.78 bilioni mapato ya uwekezaji wa majengo na TZS 20.28 bilioni mapato kutoka masoko ya fedha na

mitaji. Hadi mwezi Machi, 2017 Mfuko ulikusanya jumla TZS 54.03 bilioni ikiwemo 37.025 bilioni kutoka kwa wanachama wake, TZS 1.65 bilioni ikiwa ni mapato ya uwekezaji wa majengo na TZS 15.35 bilioni ikiwa ni mapato kutoka masoko ya fedha na mitaji.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya mfuko kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 yalikadiriwa kufikia TZS 71.37 bilioni kati ya hizo TZS 15.72 bilioni kwa ajili ya kulipa mafao, TZS 50.72 uwekezaji katika masoko ya fedha na mitaji na TZS 4.93 bilioni kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Mfuko. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 matumizi ya Mfuko yalifikia TZS 54.03 bilioni ikiwemo TZS14.17 bilioni ikiwa ni mafao yaliyolipwa kwa wanachama, TZS 23.81 bilioni ikiwa ni uwekezaji wa muda mrefu na muda mfupi katika masoko ya fedha na mitaji, TZS 11.85 bilioni ikiwa ni uwekezaji katika majengo na TZS 4.2 bilioni zilitumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa Mfuko.

Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo yenye dhamana ya kusimamia Benki ya Watu wa Zanzibar. Hadi kufikia Disemba, 2016 mapato yatokanayo na utoaji wa huduma mbali mbali za kifedha yamefikia TZS 57.08 bilioni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya TZS 54.61 bilioni. Mapato hayo yanaonyesha ukuaji wa asilimia 20 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa kwa mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, kiujumla Benki ya Watu wa Zanzibar, imeweza kutengeneza faida ya TZS 18.74 bilioni. Aidha, *PBZ* hadi kufikia Disemba 2016 imepokea Amana za wateja zenye thamani ya TZS 20.95 bilioni na kupelekea Amana za wateja kiujumla kufikia TZS 423.43 bilioni. Aidha, benki imetoa mikopo ya TZS 92.64 bilioni kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbali

mbali za kiuchumi na kijamii. Sambamba na hilo, rasilimali za benki ziliongezeka kwa TZS 37.64 bilioni na kupelekea rasilimali hizo kuongezeka na kufikia TZS 503.63 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, benki imeendelea kuimarisha huduma ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi ikiwemo:

i. Huduma ya "*mobile*" na "*Internet Banking*" kwa upande wa Benki ya Kiislamu;
ii. Uwekaji wa mashine 3 za kutolea fedha (*ATM*) katika maeneo ya BLW Mbweni, Makao Makuu ya KMKM Kibweni na Tawi la Huduma ya Benki ya Kiislamu Mpirani;
iii. Benki imefunguwa matawi manne mapya ikiwemo: Matawi mawili katika mtaa wa Tazara-Dar es Salaam; Matawi mawili Mkoa wa Mtwara pamoja na ufunguzi wa Kituo cha Huduma za Kibenki katika eneo la Kiwengwa-Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Shirika la Bima Zanzibar (*ZIC*)

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la Shirika la Bima Zanzibar ni kutoa huduma za Bima mbali mbali ikiwemo vyombo vya moto, Bima ya moto, Bima za vyomba vya baharini na nyenginezo. Kwa mwaka ulioishia Disemba, 2016 Shirika limesajili jumla ya wateja wapya 30,000 na kupelekea wateja (*customer*) wote kufikia 120,000. Katika kipindi hicho, Shirika limekusanya TZS 20.03 bilioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya TZS 21.90 bilioni ya mwaka 2016. Aidha, Shirika limepokea madai ya TZS 7.0 bilioni na baada kukamilisha taratibu za kufuatilia madai hayo, Shirika limetumia TZS 5.05 bilioni kwa ajili ya malipo ya madai hayo. Jumla ya TZS 4.90 bilioni zimetumika kwa kuendeshea shughuli mbali mbali za kiofisi ikiwemo uimarishaji wa Tawi la Mtwara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki Shirika limekamilisha taratibu za umiliki wa eneo linalotarajiwa kujengwa jengo jipya la Ofisi ya Shirika kwa upande wa Pemba.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2016 HADI MACHI 2017

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu kuwasilisha utekelezaji wa miradi iliyosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2016/2017 kama ifuatavyo:

Mradi wa Kuimarisha Huduma za Jamii Mijini (*ZUSP*)

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umelenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za wanachi mijini ambapo inahudumia Manispaa na Mabaraza ya miji ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mradi huu ulikadiriwa kupokea jumla ya TZS 14.8 bilioni kutoka Benki ya Dunia (*World Bank*). Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 9.38 bilioni sawa na asilimia 63.4 ya makadirio ya mwaka, miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kukamilisha Upembuzi yakinifu (*feasibility study*) pamoja na utayarishaji wa michoro kwa ujenzi wa jaa la Kibele;
ii. Kukamilisha Usanifu wa kina (*detailed engineering design*) ya jaa pamoja na barabara ya kuelekea kwenye eneo hilo;
iii. Kujenga ukuta wa Forodhani na barabara yenye urefu wa mita 320 kutoka Bustani ya Forodhani hadi Mkahawa wa "*Mercury*" ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Julai, 2017.
iv. Kukamilisha ujenzi wa Mitaro ya maji taka eneo la Mtopepo na Karakana (*System F*).

Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora Awamu ya Tatu

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu umelenga kuimarisha uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma na kuimarisha misingi ya utawala bora. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 mradi ulipangiwa jumla ya TZS 792.65 milioni ambapo hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 478.56 milioni sawa na asilimia 60.4 ya makadirio ya mwaka na kutekeleza yafuatayo:

i. Ununuzi wa vifaa na gari kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
ii. Kuwajenga uwezo wafanyakazi wa taasisi za serikali katika maeneo ya Ukaguzi wa thamani ya Fedha;
iii. Kuwajenga uwezo wafanyakazi wa Kitengo cha *IT* cha *IFMS* katika *Window Saver, V-MWARE* na *V-SPHERE kwenye EPICOR 10*.

Programu ya Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma (*PFMRP*)

Mhe. Mwenyekiti, programu hii ina jukumu la kuimarisha Usimamizi wa Fedha za Umma ambapo unahusisha Idara na taasisi tofauti zenye majukumu ya kusimamia Fedha za Umma. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 programu ilipangiwa jumla ya TZS 2.72 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kutoa mafunzo kwa Wakaguzi wa ndani 60, wajumbe 80 wa kamati za ukaguzi kwa Mawizara na Taasisi za Serikali juu ya *IPSA's*;
ii. Kutoa mafunzo ya bajeti inayotumia programu (*PBB*) kwa Wizara zote za SMZ. Mafunzo hayo yalijumuisha Wakurugenzi wa Idara zote za Wizara;

iii. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara juu Uchambuzi na ukadiriaji wa kodi;
iv. Kuhudhuria mafunzo ya vitendo katika Usimamizi wa Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa;
v. Kupitia na kurekebisha miongozo ya Ukaguzi wa Hesabu;na
vi. Kununua Vifaa mbali mbali vya ofisi vinayotumika katika usimamizi wa mapato na matumizi ya serikali.

Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 5.57 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa programu mbali mbali za ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali. Hadi kufikia Machi, 2017 fedha iliyotumika ni TZS 3.27 bilioni sawa na asilimia 58.7 ya makadirio ya mwaka. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kulipa gharama za Ujenzi wa Jengo la Wizara tatu Pemba (Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee,Vijana,Wanawake na Watoto, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Katiba Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora);
ii. Kulipa gharama za Ujenzi wa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
iii. Kulipa gharama za Ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti (*SUZA*); na
iv. Kulipa gharama za Ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari.

Mradi wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo

Mhe. Mwenyekiti, mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 677.00 milioni kwa utekelezaji wa shughuli za mwaka 2016/2017. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya 148.0 milioni zimepatikana

sawa na asilimia 22 ya makadirio ya mwaka. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kutoa mafunzo ya Muongozo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya MKUZA III kwa Wakurugenzi 65, Maafisa 26 kutoka sekta na 55 kutoka *LGAs*;
ii. Kutoa mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Maafisa Mipango wanne wa Mikoa, ishirini na mbili kwa Wilaya na arubaini na nne kwa Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa kwa Unguja na Pemba; na
iii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Maofisa saba, wakiwemo Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mradi wa Kuendeleza Tafiti na Ubunifu

Mhe. Mwenyekiti, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 500 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mwaka 2016/2017. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya TZS 288 milioni sawa na asilimia 58 ya makadirio ya mwaka zimeshatumika. Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ni:

i. Kufanyika kwa tafiti mbalimbali zitakazotoa taarifa zinazohitajika katika kubadilisha kianzio kipya cha mwaka 2015 kwa Pato la Taifa; na
ii. Kukamilika kwa Kizio kipya cha faharisi za bei cha Januari 2017 kwa kutumia taarifa zilizopatikana katika Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya ya 2014/15.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilipatiwa jumla ya TZS 282.00 milioni ili kutekeleza mradi wa kujenga uwezo Taasisi za Serikali, Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu katika Afya ya Uzazi na Jinsia, Mradi wa Kuwawezesha Wanyonge Kujikwamua na

Umasikini pamoja na Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa kupitia miradi hiyo ni:

i. Kuendesha vikao vya kamati za wataalamu;
ii. Kutekeleza kazi ya ufuatiliaji na kuanza matayarisho ya uzinduzi wa Kituo cha Urasimishaji wa Ardhi Kiungoni;
iii. Kuwapatia Mafunzo Masheha 30 na wasaidizi wao kwa Shehia 18 za Wilaya ya Mkoani Pemba;
iv. Kuchapishwa Madaftari 450 ya kujaza taarifa za Shehia na kusambazwa kwenye Shehia ambazo zimepatiwa mafunzo katika Wilaya za Kusini na Kaskazini.
v. Kukamilisha Rasimu ya Awali ya Sera ya Idadi ya Watu Zanzibar kwa kuwasilishwa kwa wadau

MIONGOZO INAYOTUMIWA NA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango katika kuandaa shughuli zake inazingatia malengo ya Dira ya 2020, mikakati iliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015–2020, Malengo ya maendeleo endelevu ya Dunia (*SDGs*), Mpango Mkakati wa Wizara ya Fedha wa 2015/16-2017/18 na Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara itaendelea kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na serikali kuu ikiwemo maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein katika hotuba ya uzinduzi wa kikao cha tisa (9) cha Baraza la Wawakilishi-Zanzibar.

VIPAUMBELE VYA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2017-2018.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017-2018 imedhamiria kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

i. Kufanya mageuzi katika Mfumo wa kodi (*Tax Reform*), ili kuwa na mfumo imara utakaoshajiisha ulipaji kodi kwa hiari na kupunguza gharama za uendeshaji kwa Serikali pamoja na kwa Mlipa kodi;
ii. Kushajiisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali ya TZS 1.09 trilioni ili kukidhi mahitaji ya matumizi ya serikali;
iii. Kusimamia ulipaji wa madeni ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa serikali;
iv. Kuandaa "*Fiscal and Revenue Policy*" ili kuimarisha usimamizi wa mapato na kudhibiti misamaha isiyokuwa na tija kwa nchi yetu ili kukuza pato letu na kupunguza utegemezi;
v. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuhakikisha makusanyo hayo yanakusanywa moja kwa moja katika mabenki na hatimae kuhamishiwa katika Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya serikali;
vi. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Mkakati wa maendeleo Zanzibar;
vii. Kukamilisha uanzishaji wa Sheria mpya ya Ushajiishaji na Kulinda Uwekezaji (*Zanzibar Investment Promotion and Protection Act*) ambayo itatoa sura mpya ya Uwekezaji utakaongeza tija na kukuza Pato la Taifa na Ustawi wa Jamii kwa ujumla; na

viii. Kuanza ujenzi wa Ofisi mpya ya Makao Makuu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa upande wa Unguja.

MWELEKEO WA BAJETI ZA TAASISI ZA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2017/2018.

Bodi ya Mapato-Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato Zanzibar imekadiriwa kukusanya TZS 347.29 bilioni kutoka katika vyanzo vya mapato ya kodi za ndani. Aidha, kwa mwaka 2017/2018, Bodi inatarajiwa kupokea ruzuku ya TZS 18.6 bilioni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bodi. Miongoni mwa shughuli zitakazotekelezwa ni:

i. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi;
ii. Kuanzisha matumizi ya mashine maalum za kielektroniki za kufuatilia mwenendo wa watalii wanapoingia nchini hadi wanapoondoka kwa lengo la udhibiti wa mapato yatokanayo na Sekta ya Hoteli;
iii. Kuanzisha matumizi ya Leseni maalum za kielektroniki za udereva (*Smart Driving Licence*) kwa lengo la kupambana na matumizi ya leseni bandia;
iv. Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya *ZRB* Pemba.

Shirika la Bima - Zanzibar (*ZIC*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2017, Shirika linatarajia kukusanya TZS 23.78 bilioni kutoka katika huduma za bima ya vyombo vya moto, bima ya moto, bima za vyombo vya baharini na nyenginezo. Kwa upande wa Matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya TZS 9.50 bilioni ikijumuisha matumizi ya

shughuli za Uendeshaji ya TZS 5.84 bilioni, TZS 3.65 bilioni kwa uwekezaji wa ndani.

Mfuko wa Barabara (*ZRF*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha wa 2017/18 Mfuko unatarajia kupokea jumla ya TZS 12.06 bilioni ambapo TZS 10.55 bilioni zitatokana na chanzo cha kodi ya mafuta *"Road Development Levy"* na TZS. 1.50 bilioni zitakazotokana na kodi ya uingizwaji wa magari *"Motor Vehicle Levy"* na TZS 73.00 milioni kutokana na ukodishwaji wa jengo.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Barabara unakadiriwa kutumia jumla ya TZS. 12.06 bilioni, ambapo TZS 9.10 bilioni zimepangwa kutumika kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara kuu, TZS 1.61 bilioni kwa matengenezo ya barabara za ndani na TZS 1.36 bilioni kwa kazi za uendeshaji mfuko.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko umepanga kukusanya jumla ya TZS 93.6 bilioni, kati ya hizo TZS 52.04 bilioni kutoka kwa wanachama wa Serikalini, Mashirika ya umma, Taasisi binafsi na waliojiajiri wenyewe. TZS 4.99 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na uwekezaji wa majengo na TZS 36.57 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na uwekezaji wa masoko ya fedha na mitaji ya muda mrefu na mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko unatarajia kutumia TZS 93.6 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo; Kulipa mafao kwa wanachama 6,650 kwa jumla ya TZS 20.9 bilioni; Kuwekeza TZS 67.5 bilioni kwenye majengo na masoko ya fedha; na TZS 5.2 bilioni kwa shughuli za uendeshaji.

Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*)

Mhe. Mwenyekiti, benki inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 64.70 bilioni kutoka vyanzo vya mapato. Aidha, benki imepanga kutumia jumla ya TZS 46.06 bilioni kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: Kufungua tawi katika Mkoa wa Dodoma pamoja na kuongeza vituo vya huduma katika maeneo ya Kigamboni na Tandika jijini Dar es Salaam; Kuweka mashine za kutolea fedha *ATM* katika maeneo ya Kivunge, JKU Saateni, Paje, Chwaka na Mahkamani-Vuga kwa upande wa Unguja. Aidha, kwa upande wa Pemba mashine zitawekwa katika eneo la Micheweni, Machomanne na Konde.

Mhe. Mwenyekiti, benki pia imekusudia kuimarisha utendaji wa shughuli za benki kwa kuendelea na utaratibu wa kubadilisha mtandao mama wa benki *Core Banking* System na pia kujiunga na mitandao ya "*Mastercard*" na "*Union Pay"* itakayowawezesha wateja wa Benki ya Watu wa Zanzibar kutumia huduma za benki popote pale Duniani. Aidha, Benki imekusudia kuanzisha vituo vya "*Point of Sale*ili kuweza kutoa huduma kwa wageni wanaokuja Zanzibar .

Mamlaka ya Uwekezaji na Uendelezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2017/2018, Mamlaka inatarajia kukusanya TZS 3.96 bilioni ambapo kiasi cha TZS 1.81 bilioni zinatarajiwa kukusanya kutoka vyanzo vya ndani, TZS 1.71bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo (*ADB* na *FOCAC*)na TZS 450.00 milioni ikiwa ni ruzuku kutoka mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka kwa mwaka wa fedha 2017/18, inatarajia kutumia TZS 5.43 bilioni kwa utekelezaji wa shughuli zifuatazo:

i. Kushiriki katika ziara za uhamasishaji ndani ya nchi, kikanda na kimataifa;
ii. Kuandaa kongamano la uwekezaji;
iii. Kulipia gharama za uanachama wa taasisi za kikanda na kimataifa;
iv. Kuandaaa mikutano na wadau wanaotoa huduma kwa wawekezaji *Investors' dialogue*;
v. Kufanya ukaguzi wa maeneo ya miradi inayotarajiwa kuekezwa;
vi. Kuendeleza utafiti juu ya Mwenendo wa Mitaji Binafsi *PCF*;
vii. Kufanya utafiti juu ya fursa mpya za uwekezaji Zanzibar (Mshauri wa Nje);
viii. Kujenga uzio *Amani Industrial Park*;
ix. Kutengeneza maghala matatu yaliopo Amani na Maruhubi;na
x. Kujenga uzio wa Micheweni pamoja na shughuli nyengine za uendeshaji wa Mamlaka.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali *(OCGS)*

Mhe. Mwenyekiti, **k**wa mwaka 2017/2018, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inatarajiwa kupokea jumla ya TZS 5.85 bilioni ikijumuisha ruzuku ya TZS 2.22 bilioni kutoka Serikalini na TZS 3.63 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ofisi inatarajia kutumia TZS 2.22 bilioni kwa kazi za kawaida na TZS 3.63 bilioni kwa kazi za maendeleo. Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:

i. Kukamilisha kazi za Kufanya Mapitio na Kuimarisha Takwimu za Pato la Taifa;
ii. Kufanya Utafiti wa Hali ya Kiuchumi na Kijamii kwa mwaka 2017;
iii. Kutoa takwimu za Faharisi ya Bei ya Mlaji kwa kila mwezi;
iv. Kutoa ripoti za kila robo mwaka na mwaka za takwimu za Pato la Taifa;na
v. Kuendeleza na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtwakimu-Mazizini.

MAKADIRIO YA MAPATO KWA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango imepangiwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya TZS 1,060.90 bilioni ikijumuisha TZS 627.01 bilioni za mapato yatokanayo na kodi na TZS 22.4 bilioni ikiwa ni mapato yasiyokua ya kodi. Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ni TZS 381.48 bilioni na TZS 30.0 bilioni ni mikopo ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka 2017/2018 Mapato ya kodi za ndani yaliyopangwa kukusanywa yanajumuisha mapato yatakayosanywa na :

(i) Bodi ya Mapato Zanzibar imepangiwa kukusanya TZS 347.29 bilioni sawa na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka 2017/2018 ya TZS 1.09 trilioni; na
(ii) Mamlaka ya Mapato imepangiwa kukusanya TZS 258.72 bilioni sawa na asilimia 24 ya makadirio ya mwaka 2017/2018 ya TZS 1.09 trilioni.

Jadweli Nam.6, 7 na mchoro Nam.1 yanaonyesha uwiano wa makadirio ya mapato kwa mwaka 2017-2018.

MAOMBI YA FEDHA KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO -2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara ya Fedha na Mipango iweze kutekeleza ipasavyo malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha ya TZS 219.41 bilioni kwa mwaka 2017/18 ambapo uchambuzi wa Matumizi hayo kama ifuatavyo:

Fungu F01: Wizara ya Fedha

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS 108.87 bilioni ikiwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Kazi za Maendeleo kwa Fungu hilo. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara TZS 31.31 bilioni, Ruzuku kwa Taasisi za Serikali zilizopo chini ya Wizara TZS 29.26 bilioni, fedha za Matumizi Mengineyo TZS 10.23 bilioni na TZS 38.06 bilioni zimepangwa kutumiwa kwa Kazi za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Matumizi ya Fedha kwa programu za F01 yamegawika kama ifuatavyo:

i. Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha Za Umma inakadiriwa kutumia TZS 64.76 bilioni;
ii. Programu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma inakadiriwa kutumia TZS 9.51 bilioni;
iii. Programu ya Uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Fedha inakadiriwa kutumia TZS 34.59 bilioni;

Fungu F02: Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS 101.11 bilioni kwa ajili ya matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu

wa Serikali. Matumizi hayo yanajumuisha mishahara ya TZS 1.11 bilioni na TZS 11.48 bilioni kwa malipo ya kiinua mgongo, TZS 18.0 bilioni kwa malipo ya Pencheni na TZS 70.53 bilioni kwa malipo ya gharama nyenginezo zinazopaswa kuhudumiwa na Mfuko.

Fungu F03-Tume ya Mipango

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaomba jumla ya TZS 9.43 bilioni kwa ajili ya matumizi ya Tume ya Mipango ikijumuisha TZS 1.18 bilioni kwa ajili ya ulipaji wa Mishahara, TZS 2.22 bilioni kwa ajili ya ruzuku ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, TZS 1.30 bilioni kwa matumizi mengineyo ya Tume ya Mipango na TZS 4.73 bilioni kwa Kazi za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya Fedha kwa programu za F03 yamegawika kama ifuatavyo:

i. Programu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda kazi imekadiriwa kutumia TZS 1.52 bilioni;
ii. Usimamizi wa Uchumi Mkuu unakadiriwa kutumia TZS 6.20 bilioni;na
iii. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango unakadiriwa kutumia TZS 1.72 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka 2017/2018 yanapatikana katika kitabu cha tatu cha Bajeti ukurasa F01-1 hadi F03-15.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii ya pekee, kuwashukuru wote waliotupa mashirikiano ili kufanikisha

utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Baadhi ya nchi zinazotoa ushirikiano mkubwa katika kusaidia ufanikishaji wa shughuli za Wizara na Serikali kwa ujumla. Nchi hizo ikiwemo: Norway, Korea, Japan, China, Italia, India na Singapore. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mashirika na taasisi mbali mbali za Kimataifa ikiwemo; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Benki ya Dunia *(World Bank),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB), DFID, UNICEF,* Shirika la Fedha la Dunia *(IMF)* kupitia kanda ya Afrika Mashariki, na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za dhati kwa Taasisi na Asasi za Kiraia pamoja na Sekta Binafsi kwa mashirikiano yao ya karibu wanayotupa wakati wa matayarisho ya Bajeti. Napenda kuwaomba washirika wote wa maendeleo kiujumla kuendelea kushirikiana nasi kwani mashirikiano yao yatatusaidia sana kufikia malengo tuliyoyaweka kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika wako na Wenyeviti wote wa Baraza hili kwa uongozi wenu imara mnaoutumia katika kuongoza vikao vya Baraza hili. Shukrani zangu pia ziende kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na miongozo waliyoitoa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yangu na hatimae kuridhia mapendekezo haya yawasilishwe katika Baraza hili.Tunathamini sana mashirikiano tunayoyapata kwako, Baraza zima na hususan kwa kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, pia natoa shukrani zangu za dhati kwa Wafanyakazi, Wakuu wa Vitengo, Idara na Taasisi za Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Khamis

Mussa Omar, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Ndg. Juma Hassan Reli, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ali Khamis Juma na Mhasibu Mkuu wa Serikali Ndg. Mwanahija Almas Ali. Nawashukuru sana kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara yanatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru sana Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali chini ya Wizara kwa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, mara hii sehemu kubwa ya kikao chetu hiki cha Bajeti kimefanyika ndani ya mwezi wetu mtukufu wa Ramadhani. Naomba nichukue fursa hii kuwatakia swaumu njema, sala na dua zenye kukubaliwa kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba pamoja na waumini wote wakiislamu ulimwenguni kwa kutekeleza ibada hiyo, ikiwa ni moja kati ya nguzo tano za uislamu. Pia namuomba Mwenyezi Mungu kwa fadhila za mwezi huu wa Ramadhan, atujaalie kuwa ni jamii yenye kupendana na kushikamana zaidi, atuondolee kila fitna na hasada miongoni mwetu na baina ya makundi mbali mbali ya jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

JADWELI NAM.1

JADWELI NAM.1	
FUNGU	**RA ZA WIZARA YA FEDHA NA MIPAN**
F01:WIZARA YA FEDHA	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
	Idara ya Bajeti
	Idara ya Fedha za Nje
	Idara ya Uhakikimali
	Idara ya Mitaji ya Umma
	Idara ya Mipango Sera na utafiti
	Idara ya Hesabu za Ndani
	Idara ya Utawala na Uendeshaji
	Idara ya Fedha na Kodi
	Ofisi Kuu Pemba
	Mfuko Mkuu wa Serikali
F01: MFUKO MKUU WA	Mfuko wa Miundombinu
F03: TUME YA MIPANGO	Idara ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini
	Idara ya Maendeleo ya Watenda Kazi
	Idara ya Ukuzaji Uchumi
	Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini
TAASISI ZA MUUNGANO	
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)-Tawi la Zanzibar	
Mamlaka ya Bima(TIRA)- Tawi la Zanzibar	
Benki kuu ya Tanzania(BOT)-Tawi la Zanzibar	
Tume ya pamoja ya Fedha- Tawi la Zanzibar	

VIAMBATANISHO VYA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA MWAKA 2016-2017

JADWELI NAM.2

Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Fe	
Vianzio:	2
Mapato ya Kodi	
ZRB	
TRA	
PAYE	
Jumla ya Mapato ya Kodi	
Mikopo ya ndani	
Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo	
Mapato yasiyokua ya Kodi:	
Gawio kutoka BOT	
Gawio kutoka katika Mashirika	
Mapato ya Uhamiaji	
Usajili wa Wazabuni na uuzaji wa nyaraka za za	
Uuzaji wa vifaa chakavu	
Kodi za nyumba za Serikali	
Kodi ya Bohari	
Jumla ya Mapato yasiyo ya kodi	
Jumla kuu	
Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango	

JADWELI NAM.3

Matumizi ya F01 & F02 na F03 (Julai-Machi) kwa mv		
S/N	**Programu kuu**	**Programu ndogo**
1	Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	Mfumo wa Udhibiti wa Ulipaji
		Usimamizi wa hesabu za ndani
		Usimamizi wa Bajeti ya Serikali
		Uratibu wa Rasilimali za Nje
		Jumla ndogo
2	Usimamizi na uwekezaji wa Mali za Umma	**Usimamizi wa Mitaji ya Umma**
		Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali S
		Jumla ndogo
3	Mipango na Uendeshaji wa sekta za Fedha	Utawala na Uendeshaji wa Wizara
		Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha
		Sekta ya Fedha na Mapato ya Kodi
		Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wiza Pemba
		Jumla Ndogo
		Jumla F01
4	Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali	Usimamizi wa mfuko Mkuu wa Serikali
		Jumla F02
5	Kuratibu Mipango ya kitaifa na maendeleo ya Watenda Kazi	Uratibu wa Maendeleo ya kisekta na Kupunguza umaskini
		Maendeleo ya Watendakazi na masuala ya Idadi ya Watu
		Tathmini na ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo
		Jumla ndogo
6	Usimamizi wa uchumi Mkuu	Usimamizi wa Uchumi Mkuu
		Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Binafsi
		Jumla ndogo
7	Utawala na Uendeshaji wa tume ya Mipango	Utawala na uendeshaji wa Tume ya Mipang
		Jumla ndogo
		Jumla F03
		Jumla F01+F02+F03

JADWELI NAM.4

Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali hadi Ma	
Vianzo	Makadirio 2016/201
Hati Fungani	8,485.0
Mikopo ya ndani	4,672.0
Kiinua Mgongo	14,705.0
Pencheni	12,504.0
Wazabuni wa Serikali	7,256.0
Malipo Mengineyo	35,907.0
JUMLA	83,529.0
Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar	

JADWELI NAM.5

Deni la Serikali hadi kufikia tarehe 30 M
Maelezo
Deni la Ndani:
Mikopo ya Ndani
Hati Fungani za muda mrefu
Kiinua mgango
Wazabuni wa Serikali
Jumla Ndogo
Deni la Nje
Jumla ya Deni la Taifa
Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango-Z

VIAMBATANISHO VYA MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2017-2018

JADWELI NAM.6

	Mapato ya Wizara ya Fedha kwa r
Vianzio	**Makadi**
Mapato ya Kodi	
ZRB	
TRA	
PAYE	
Jumla	
Mikopo ya ndani	
Mapato kutoka kwa washirika wa Maendeleo	
Mapato yasiyo kuwa ya kodi	
Gawio kutoka BOT	
Gawio kutoka katika Mashirika	
Mapato ya Uhamiaji	
Usaji wa Wazabuni na Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni	
Uuzaji wa vifaa chakavu	
Kodi za Nyumba za Serikali	
Kodi ya Bohari	
Jumla	
Jumla kuu	
Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango	

JADWELI NAM.7

Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Fedha	
Vianzio	M
Mapato ya Kodi	
ZRB	
TRA	
PAYE	
Mikopo ya ndani	
Mapato kutoka kwa washirika wa Maendeleo	
Mapato yasiyo kuwa ya kodi	
Jumla kuu	

MCHORO NAM.1



JADWELI NAM.8

Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 20			
S/N	**Programu kuu**	**Program ndogo**	**Fedha zin**
1	Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma	Usimamizi wa hazina	
		Usimamizi wa hesabu za ndani	
		Usimamizi wa bajeti za Serikali	
		Kusimamia sekta ya Fedha na Mapato yatokanayo na kodi	
		Uratibu wa Rasilimali za nje	
		Jumla ndogo	
2	Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma	Usimamizi wa Mitaji ya Umma	
		Usimamizi na Uhakiki wa Mali za Serikali	
		Jumla ndogo	
3	Mipango na Uendeshaji wa Sekta za Fedha	Utawala na uendeshaji wa Wizara	
		Mipango, Sera na Tafiti za sekta ya Fedha	
		Uratibu na utekelezaji wa shughuli za wizara Pemba	
		Jumla Ndogo	
		Jumla F01	
4	Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali	**Jumla F02**	
5	Kuratibu Mipango ya kitaifa na Maendeleo ya Watenda kazi	Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini	
		Maendeleo ya Watendakazi na masuala ya Idadi ya watu	
		Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo	
		Jumla ndogo	
6	Usimamizi wa uchumi Mkuu	Usimamizi wa uchumi Mkuu	
		Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Binafsi	
		Jumla ndogo	
7	Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	
		Jumla ndogo	
		Jumla F03	
		Jumla kuu	

JADWELI NAM.9

Miradi/Program zitakazotekelezwa na Wizara ya Fedha na

S/NO	Jina la Mradi/Program		
		Jumla	**SMZ**
1	Mipango Ufuatiliaji na Tathmini yenye kuleta matokeo ya Mkuza III		
2	Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali		
3	Kuwawezesha wanyonge kujikwamua na Umaskini	**105.00**	
4	Kuoanisha masuala ya Idadi ya watu katika afya ya uzazi, jinsia na kupunguza umaskini	**269.00**	
5	Mpango wa Kurasimisha rasilimali na biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)	**632.24**	
6	Kuendeleza Tafiti na Ubunifu	**225.00**	
7	Uimarishaji wa takwimu	**3,500.00**	
8	Ujenzi wa Ofisi za Serikali	**8,300.00**	8
9	Upatikanaji wa rasilimali fedha	**1,000.00**	1
10	Mradi wa maendeleo endelevu	**495.52**	
11	Mradi wa huduma za jamii mijini	**18,732.74**	
12	Usimamizi wa Mageuzi ya Fedha za Umma	**2,600.00**	
13	Kuimarisha Utawala bora III	**4,266.40**	
14	Uimarishaji wa rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili	**2,668.85**	
	JUMLA	**42,794.75**	**11**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ussi Yahya Haji (Kny: Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti wa Kamati Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe.

Mwenyekiti**,** kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi naomba kutoa taarifa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kueleza chochote, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* mwingi wa rehma kwa uwezo na mapenzi yake ya kutukutanisha hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie uzima na akipe heri na baraka kikao chetu hiki hasa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan tukiwa katika kumi la pili la Maghfira. Aidha, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa, wewe Mhe. Spika kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake wa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu wa hali ya juu unaopelekea wananchi kuzidi kujenga imani kwake. Tunawaomba wananchi wetu waendelee kumuamini pamoja na kumpatia mashirikiano ya hali na mali hususan katika kudumisha amani na utulivu ili tuweze kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Aidha, tunazidi kumpongeza Mhe. Rais kwa kutekeleza ahadi zake alizozitoa katika Kampeni za Uchaguzi za mwaka 2015 alipokuwa akitetea nafasi yake ya Urais katika nchi yetu kwa kuwapatia Wafanyakazi wa Zanzibar nyongeza ya mshahara wa kiwango cha chini kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, salamu za pekee zimuendee Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa busara na uwezo wake mkubwa aliojaaliwa kuwa nao hususan katika usimamizi wa shughuli za Serikali ndani ya Baraza hili muhimu la

kuwawakilisha wananchi. Kwa kweli ni kiongozi wa kupigiwa mfano ambapo nasi Waheshimiwa Wajumbe tunatakiwa tuchote busara na hekima kutoka kwake ili tuweze kuwaongoza vyema wananchi wetu huko majimboni mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, **n**itumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Viongozi na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zake hususan Waziri Dkt. Khalid Salum Mohammed; Katibu Mkuu Khamis Mussa Omar; Naibu Katibu Mkuu Ali Khamis Juma; Mhasibu Mkuu wa Serikali Mwanahija Almas Ali na Afisa Mdhamini Ibrahim Saleh Juma kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao uliopelekea kutekeleza kwa asilimia kubwa malengo yao waliyojipangia katika mwaka wa fedha 2016/2017. Vile vile, Kamati inawashukuru sana kwa mashirikiano yao chanya waliyotupatia yaliyoiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake pasi na kuwepo kikwazo cha aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, kwa kuthamini na kutambua michango na ushauri uliotolewa na Kamati yangu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ya Fedha na Mipango. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Makatibu ambao wametusaidia ipasavyo katika kutekeleza majukumu ya Kamati kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti;
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamo Mwenyekiti;
3.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe;

4.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Mjumbe;
5.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe;
6.	Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
7.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe.
8.	Ndugu Ramadhan Khamis Masoud	-	Katibu
9.	Ndugu Said Khamis Ramadhan	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango imeundwa na baadhi ya Taasisi zinazojitegemea kimafungu. Hivyo, Bajeti ya Wizara hii inatekelezwa kupitia mafungu makuu matatu (3) yanayojumuisha Fungu FO1 linalokusanya Programu zote za Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu F02 la Mfuko Mkuu wa Serikali na Fungu F03 linaloelezea Programu za Tume ya Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa Programu za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea ushauri na maelekezo kama ifuatavyo:

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma inakusudia kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali na ufuatiliaji wa upatikanaji misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Programu kuu hii kwa pamoja

inatekelezwa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mfuko wa Barabara, Idara ya Bajeti, Idara ya Fedha za Nje, Idara ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani na Idara ya Fedha na Kodi.

PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, Programu hii ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali lengo lake ni kusimamia na kutayarisha Bajeti ya Serikali na matokeo ya Programu hii ni kuhakikisha kunakuwepo mgawanyo mzuri wa rasilimali unaozingatia vipaumbele vya taifa kwa sekta mbali mbali za serikali. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango isimamie vizuri mgawanyo wa rasilimali kwa sekta ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja, ikiwemo Sekta ya Afya, Elimu, Maji safi na salama na Sekta ya Kilimo. Aidha, inaipongeza wizara kwa kujiwekea vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ikiwemo kipaumbele cha kushajihisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali ya Tzs. 1,087.4 Bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukusanyaji mapato sio la Wizara ya Fedha na Mipango peke yake, bali hata sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi tuna jukumu kubwa la kuhakikisha mapato ya serikali yanaongezeka maradufu kwa kuwahamasisha Wananchi wetu kwenye Majimbo yetu kudai risiti kila wanapofanya manunuzi. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha mchakato wa ununuzi wa mashine za *EFD* ili serikali iongeze wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA RASILIMALI ZA NJE

Mhe. Mwenyekiti, programu ndogo hii inakusudia kufuatilia na kuratibu misaada na mikopo kutoka kwa Wahisani wa maendeleo, hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya Tzs. 49.86 Bilioni zimekusanywa zikijumuisha Tzs. 25.42 Bilioni ni ruzuku na Tzs. 24.44 za mikopo. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango isikate tamaa katika kuwahamasisha Washirika mbali mbali wa Maendeleo wanaoitakia mema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili Tzs. 381.41 Bilioni zipatikane kutoka kwa Washirika wa Maendeleo hao kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango iongeze kasi ya ufuatiliaji wa taratibu za kisheria na kifedha ili Mradi wa '*Terminal II'* uweze kukwamuka katika mwaka wa fedha 2017/2018.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma inakusudia kusimamia Mitaji ya Umma ili kuhakikisha inakwenda sambamba na mabadiliko ya uchumi pamoja na kuwepo kwa uwazi na usawa wa tathmini ya bidhaa zinazonunuliwa katika taratibu za manunuzi. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mitaji ya Umma na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*).

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) inaendelea kufanya kazi nzuri ambayo kamati yangu inaipongeza, lakini kuna maeneo ambayo yametolewa kwa Wawekezaji ili wayaendeleze kwa kufanya Miradi ya Kimaendeleo ambayo hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuyafanyia kazi maeneo hayo. Kamati yangu inashauri maeneo yote waliyopewa wawekezaji kwa muda mrefu ambayo hadi sasa bado hayajaendelezwa ni busara yarejeshwe serikalini. Aidha, kamati inaishauri tena Wizara ya Fedha wakamilishe taratibu zilizobakia baina ya Serikali na Muwekezaji

wa Hoteli ya Bwawani ili hatua za kuimarisha hoteli hiyo ikamilike na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana kwa serikali kujiongezea mapato na vijana wetu wapate ajira.

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Fedha na Mipango imekusudia kuweka mazingira bora na rafiki kwa Wafanyakazi ili matokeo ya ufanisi wa kazi za Wizara na Taasisi zake yaonekane na kuwa endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inathamini sana juhudi zinazofanywa na Wizara hii hususan za kuimarisha maslahi ya Wafanyakazi wake. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango iwafikiriwe kuwapatia posho la mazingira magumu watendaji wa kada ya Uhasibu wa '*Vote'* za wizara kwa kazi zao kubwa, ngumu na nyeti ili wafanyekazi zao kwa ari kubwa na kasi zaidi. Watendaji wenyewe ni:-

1) Wasaidizi Wahasibu Wakuu wa *Vote*;
2) Wakaguzi Wakuu wa Ndani wa *Vote*; na
3) Washika Fedha wa *Vote*.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango iweke utaratibu maalum wa kuwapandisha Madaraja Wahasibu, Washika Fedha na Wakaguzi wa ndani kwa mujibu wa sifa na uzoefu wao ili kupunguza malalamiko yaliyopo kwa Watendaji hao.

PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali ina lengo la kusimamia na kufanya malipo maalum ya serikali. Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia malipo maalum ya serikali yanajumuisha malipo ya viinua mgongo, pencheni, madeni na matumizi mengineyo ya serikali. Hadi kufikia Machi, 2017 Mfuko Mkuu wa Serikali umetumia Tzs. 15.14 bilioni kwa ajili ya kulipa mafao ya kiinua mgongo kwa wastaafu 1,015 wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na 9.94 Bilioni zimetumika kwa kulipia pencheni za wastaafu. Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua inazozichukua za kuwalipa Wastaafu wetu kwa kipindi kifupi baada ya kustaafu, hatua hizi ziwe endelevu ili wastaafu wafaidi mafao yao kabla ya jasho lao kukauka. Aidha, kamati inaiomba serikali kupitia Wizara hii iongeze kiwango cha pencheni kwa Wazee Wastaafu kama ilivyofanya kwa Wafanyakazi wa Serikali, Wazee wetu hawa wamefanya kazi kubwa sana kuitumikia Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar, hivyo ipo haja kwa Serikali kuwaongezea mafao ya pencheni ili waweze kumudu gharama za maisha ambazo huwa zinapanda kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea Programu hizo za Wizara ya Fedha na Mipango, kutokana na umuhimu wa taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii, sasa naomba nizielezee baadhi ya taasisi hizo kama ifuatavyo:

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII (*ZSSF*)

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaupongeza Uongozi na Watendaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kwa ubunifu wao katika kuwekeza fedha za mfuko kwenye Miradi mbali mbali ya Maendeleo ikiwemo uwekezaji wa kiwango cha umiliki wa

asilimia 45 ya Hisa katika Kampuni mpya ya Uvuvi ya Zanzibar (*ZAFICO*). Kamati inaitaka *ZSSF* iisimamie vizuri Kampuni hii ya *ZAFICO* ili fedha zilizowekezwa ziweze kuleta tija na faida kuwa kubwa badala ya hasara kama tunavyoona kwenye baadhi ya mashirika yaliopo. Aidha, Kamati inaitaka *ZSSF* kukamilisha kwa wakati miradi ya nyumba za makaazi ziliopo Mbweni - Unguja na ukarabati wa Jumba la Treni (*Chawel building*) sambamba na kuharakisha ujenzi wa '*Shopping Mall'* katika eneo la Michenzani Makontena.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR *(ZRB)* NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA - ZANZIBAR *(TRA)*

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Mapato ya Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zina jukumu la kukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia Machi, 2017 *ZRB* imepindukia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 110 na *TRA* imepindukia lengo kwa kukusanya asilimia 109. Kwa kuwa *"Mcheza Kwao Hutunzwa"* Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Watendaji wa Taasisi mbili hizo kwa ubunifu wao wa kufuatilia na kuwahamasisha walipa kodi walipe kwa hiari bila ya kushurutishwa pamoja na kutafuta njia mbadala za kuongeza mapato kupitia vyanzo vya mapato viliopo bila ya ongezeko lolote la kodi. Kamati yangu inazisisitiza taasisi hizo kwamba wasibweteke na mafanikio hayo badala yake waongeze bidii zaidi ili mwaka wa fedha 2017/2018 waweze kuvuka lengo la ukusanyaji wa mapato ya Tzs. 347.3 Bilioni kwa *ZRB* na Tzs. 258.7 Bilioni kwa *TRA*.

BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (*PBZ*)

Mhe. Mwenyekiti, tunaupongeza Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kwa jitihada na mabadiliko makubwa ya kiutendaji wa Benki hiyo hususan kwa kufungua Matawi mapya katika Mtaa wa

Tazara - Dar es Salaam, Mtwara pamoja na kufungua kituo cha huduma za kibenki katika eneo la Kiwengwa Mkoa wa Kaskazini - Unguja. Licha ya mafanikio hayo yaliyopatikana, kamati yangu inashauri yafuatayo:

1) *PBZ* iharakishe kufunga mtandao mpya wa *CORE BANKING SYSTEM* utakaokidhi kuwahudumia wateja wengi zaidi;

2) *PBZ* iongeze madirisha ya utoaji huduma (*tellers*) katika Matawi yake ili kupunguza msongamano wa Wateja hasa mwisho wa mwezi;

3) *PBZ* iharakishe inafunga mashine mpya za *ATM* za kuweka na kutoa fedha ili kupunguza msongamano kwenye Matawi ya Benki hizo;

4) *PBZ* iendelee kuwahimiza na kuwaelimisha wananchi kuhusu utumiaji huduma za Kibenki kupitia mitandao mbali mbali ya simu za mkononi yaani *INTERNET BANKING*; na

5) Kamati inawaomba Wateja wa *PBZ* na Wananchi wote watumie huduma za *ATM* ambazo zipo katika maeneo mbali mbali. Huduma hizo ni rahisi, salama na bora zaidi hususan katika kupunguza msongamano kama sio kuumaliza kabisa hasa kila ifikapo mwisho wa mwezi.

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Shirika letu la Bima la Zanzibar ni shirika ambalo linafanya vizuri kila uchao, licha ya ushindani mkubwa uliopo kutoka katika Makampuni mengine yanayotoa huduma hii ya bima hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hivyo, Kamati inaushauri Uongozi wa Shirika la Bima uongeze bidii na juhudi zaidi ili shirika letu lizidi kupata mafanikio zaidi. Aidha, Kamati

inaishauri serikali kwamba miradi mikubwa kama '*Terminal II'* na Ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri pamoja na hoteli zote zikate bima zao kupitia Shirika letu la Bima. Vile vile, kamati inazishauri Taasisi za Serikali na Mashirika ya Serikali ambazo zimekata bima kupitia Mawakala, wabadilike na wakate bima zao moja kwa moja kwenye Shirika letu la Bima Zanzibar.

MFUKO WA BARABARA

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko huu wa Barabara upo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ambao una lengo la kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya Barabara pamoja na kufuatilia na kukagua matumizi ya fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu na imara itakayosaidia harakati za kiuchumi. Kamati inaushauri Mfuko wa Barabara kuwa makini na fedha wanazotoa kwa ajili ya matengenezo ya Barabara kwani baadhi ya barabara zinaonekana hazina viwango wala hazilingani na fedha zilizotumika "*Value for Money*". Aidha Kamati inaitaka Mfuko wa Barabara, watoe fedha za matengenezo ya barabara kwani tumeshuhudia barabara nyingi za mjini na za Mashamba zimeharibika kwa mvua za Masika zilizonyesha hivi karibuni. Tunawaomba watendaji wa Mfuko wa Barabara wachukue hatua za haraka ili kuzinusuru barabara hizo zisiendelee kuchimbuka na kuweza kupitika kwa uzuri zaidi kwa muda wote.

MRADI WA KUIMARISHA HUDUMA ZA JAMII MJINI (*ZUSP*)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu wa *ZUSP* una lengo la kuweka mazingira bora ya Miji yetu Unguja na Pemba, kamati inaishauri wizara kusimamia vyema mikataba mbali mbali ambayo inasaini na Wakandarasi ihakikishe inatekelezwa mikataba hiyo kwa wakati, kwani baadhi ya Miradi inachukuwa muda mrefu zaidi ya ule uliosainiwa kwenye Mkataba hatimae Miradi hiyo hupelekea

gharama za ziada kwa Serikali. Kamati inaitaka wizara isimamie kwa karibu zaidi Mradi wa Ukuta (*Sea wall*) kwani Mradi huo umechukua muda mrefu bila ya kumalizika. Aidha, Kamati inaiomba Wizara kupitia Mradi huu wa *ZUSP* kuyaondoa maji ya mvua yanayotuwama eneo la Mwanakwerekwe, Fuoni Kibondemzungu na maji yanayotuama kwenye barabara ya Kiembesamaki - Uwanja wa Ndege ili kuweka haiba nzuri ya maeneo hayo.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kwa vile Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muiunge mkono bajeti hii, ili mumuwezeshe Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha ujao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Mwenyekiti wangu pamoja na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ussi Yahya kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa

mchango wako na uwasilishaji wako makini nakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa mwanzo kwa leo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali, na kama muda utatosha nitampisha Mhe. Ali Salum Haji - Mnadhimu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii muhimu ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, katika bajeti yake ya mwaka 2017/2018.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi mbali mbali kwa kazi zao nzuri wanazozifanya hadi kukaa hapa na kuhakikisha kwamba mambo yote katika nchi yetu yanakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kuyashukuru mashirika yote yaliyokuwa chini ya Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri zinazofanywa na kuongezeka pato la nchi katika nchi yetu. Aidha nawapongeza wafanyakazi wote wa wizara hii pamoja na mashirika yote kwa kazi hizo wanazofanya na kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumzia baadhi ya sehemu au mashirika na yale yote niliyokuwa sikuyagusa nayaunga mkono kwa asilimia mia moja katika kazi zao. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, tumo katika ushindani wa kibiashara na tunaona mabenki mbali mbali, makampuni mbali mbali yapo kwa wingi katika nchi yetu, ili kuhakikisha kwamba ushindani unaendelea na mwenye uwezo ndio anakwenda vizuri. Kwa hivyo, mimi nachukua fursa hii kwanza kuipongeza benki ya watu wa Zanzibar kwa kazi nzuri wanazofanya. Pia kusema tu kwamba kiwango chao cha mahitaji ya wananchi wetu kimekuwa kikubwa na

mahitaji yameongezeka. Lakini ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri umefika wakati sasa hivi Benki ya Watu wa Zanzibar ikazidi kuelekezwa katika maeneo mbali mbali katika mkusanyiko wa watu kwenye jamii yetu tunayoishi.

Mhe. Mwenyekiti, utashuhudia siku za mwisho wa mwezi, wananchi wetu wengi wafanyakazi wanakwenda katika mabenki yetu kupokea mishahara yao huwa kama kuna maandamano, kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri tuna Wilaya zetu tuna Mikoa yetu kwa hivyo kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja vingetafutwa Vituo viwili kila Wilaya kikaweko karibu na watu wetu ili kupokea pesa kule kuondokana na msongomano wanaoupata mjini.

Kwa mfano kama Mkwajuni zamani ilikuwepo benki tukenda zetu kwa sasa labda tuchukulie tu *centre* yetu Mahonda au Kiwengwa mote mnafaa humo, lakini ukienda Mkoa wa Kusini Makunduchi, ukija zako kwengine kwa Wilaya ya Kati tuchukulie mkusanyiko wa watu sasa upo Chwaka au kwengineko Uroa humo mnafaa kuweka uwiano mzuri kwa wananchi wetu wasisumbuke.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Pemba nako vile vile tuna sehemu za mkusanyiko wa watu wengi katika hali ya biashara zetu, ukenda Wete nashukuru benki ipo lakini ukenda Tumbe sasa hivi kuna mkusanyiko mkubwa, lakini unaweza kwenda Micheweni na kwengineko kila pahala ambapo pataonyesha pana haja ya kupunguza msongamano siku za mwisho wa mwezi wananchi wetu wanapata shida sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na shida hiyo nawapongeza wafanyakai wa benki wanafanya kazi katika mazingira mazuri ingawa magumu wakati mwengine, lakini wastahamilivu sana hujapata shida ya manung'uniko ya wateja wake wanaokwenda

pale kama leo tunasumbuliwa hakuna. Mimi nawapongeza ni watu ambao karibu sana wanafanya kazi kwa uadilifu na ile ndio sera ya Serikali yetu, tufanye kazi katika mazingira mazuri ili wananchi wetu waridhike na huduma.

Mhe. Mwenyekiti, hata mikopo mingi wafanyakazi wetu na badhi ya nafasi nyengine na wafanyabiashara wanapata mikopo kwa uwezo wao naipongeza benki kwa kuongezeka kwa asilimia kubwa kwa wajarisiriamali wetu kupitia benki yetu hii wanapata mikopo mbali mbali kuendesha maisha yao. Kwa hivyo, nawaomba tu *PBZ* au Benki ya Watu wa Zanzibar waongeze nguvu waongeze maarifa ili biashara itanuke zaidi na kupatikana pato la nchi katika mambo mbali mbali.

Lakini jengine Mheshimiwa kwa upande mwengine nitawapongeza wenzetu wa Shirika la Bima la Taifa la Zanzibar hivi sasa hivi tumeona mafanikio makubwa mapato yameongezeka. Lakini hali kadhalika wigo wa kuendeleza sehemu mbali mbali Tanzania Bara wameelekeza nguvu zao huko kuongeza pato letu la nchi na wao kupata pato na kuingiza Mfuko Mkuu wa Hazina katika pato hili la Serikali. Kwa hivyo nawapongeza Bima sina matatizo nao.

Mhe. Mwenyekiti, *ZRB* ni chombo ambacho kimeundwa kisheria kinakusanya mapato na mapato hayo ndio yanaelekezwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kujua tu kwamba kimepatikana hiki kigawiwe kiendeleze katika sehemu zetu za Wizara mbali mbali au taasisi mbali mbali za Serikali. Lakini niseme tu kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar wamefanya juhudi kubwa sana na katika juhudi yao hiyo tumeona changamoto yao wanayoendelea nayo, pamoja na mazingira mengi wanayofanya katika kazi zao lakini bado natoa wito wafuatilie baadhi ya taasisi ambazo bado ziko nyuma au zinachelewa kupeleka mapato yao katika chombo hiki cha *ZRB*.

Lakini kuna mfumo mwengine nimeuona Mheshimiwa hayo pia katika kukusanya mapato kuna wafanyabiashara, madereva, au nani, mara nyingi wanapata shida siku za kulipa leseni zao, leseni ukalipe *ZRB* unaambiwa ondoka hapa nenda *PBZ* kwanza kalipe huko urudi tena hapa inakuwa usumbufu. Ningeomba Mheshimiwa hapo hapo *ZRB* pawe na chombo cha kulipia kama *PBZ* pale wawepo tuondoe urasimu wa kuhangaishwa watu wetu kutoka Karakana siku nyengine urudi hapa halafu urudie tena kule.

Namuomba Mhe.Waziri hili tuliangalie kwa sababu malalamiko ya wafanya biashara wengi au wenye leseni za magari huwa wanapata shida na wanalalamika muda wao mwingi unapotea pale kwenye msongamano. Ndio nikasema tu pana haja sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, tutanue wigo wa maeneo kupunguza huu msongamano na kurahisisha kazi ili anapokwenda pale mtu yeyote mwenye kuhitaji leseni na mambo mengine inakuwa rahisi kulipa na kuondoka. Huo ndio utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mapato yanapatikana vizuri na yanapatikana kwa wakati bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kwa jumla nitazungumzia kidogo huduma za jamii kwa wananchi wetu. Ningemuomba Mhe. Waziri Serikali yetu kupitia kauli ya Mhe. Rais iliongeza mshahara kwa wafanyakazi na hilo limepokelewa mikono miwili. Lakini mimi nitamuuliza tu Mhe. Waziri kama itakuja taarifa ile baadae au sikusikia vyema wastaafu wetu wa sehemu mbali mbali wanaulizia kima cha chini kimeongezeka lakini wao vipi wamesahauliwa au vipi. Kama sikusikia Mheshimiwa Waziri akija atanihakiki tu kwamba lilisemwa au kama halijasemwa ndio nauliza je, wastaafu wetu wanaelekea wapi katika faida hii iliyopatikana ya kuongezwa mshahara kwa kima cha chini.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, sina mengi sana katika Wizara hii nampongeza tena Mhe. Waziri na watendaji wake wote na naomba Waheshimiwa Wajumbe sisi sote wa Baraza la Wawakilishi kila panapo nyanja ya kupata mapato tumuelekeze tumfahamishe ili ahakikishe kwamba tunakwenda vizuri katika mambo yetu mbali mbali na serikali kupata fedha nyingi ndio kuongeza ufanisi wa utendaji wake. Kwa sababu tunajua Wizara hii ndio mama ukenda kwenye Baraza la Wawakilishi tunaitegemea Wizara ya Fedha, ukenda kwenye kilimo, ukenda kwenye afya, maji, umeme ukenda pahala popote inategemewa hii. Kwa hivyo, niseme tu naipongeza Wizara, nampongeza Waziri na watendaji wake na sina tatizo nayo nimeridhika nayo. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele naunga mkono kwa asilimia mia moja sina tatizo nayo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali wa Jimbo la Kijitoupele kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Kwahani.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Mimi sina mchango mkubwa kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na michango mikubwa nimeshaiwasilisha kwa Kaimu Mwenyekiti wangu aliyewasilisha hapa, michango yangu yote ilikuwa nimetia mle isipokuwa nina mawili matatu tu niliona ni vyema basi tukumbushane zaidi kwa Mhe. Waziri.

Kabla sijaanza na mchango wowote Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa namna ya utendaji bora wa kazi ambao umetoa matumaini kwa wananchi wa Zanzibar wote. Lakini pia ningependa nivipongeze vitengo vya

Wizara hii kwa wenzetu wa *ZRB, ZSSF* na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, michango yangu ipo katika maeneo kama mawili, la kwanza nataka nchangia katika suala zima la risiti za *electronic* ambalo limeanza kuonesha dalili na matumaini yameanza kuonekana. Lakini nilitaka nimuombe Mhe. Waziri tu namna ya kurudisha bidii na uharakishaji katika suala zima la kutumia risiti za *electronic*. Wakati wajumbe wengi wanapozungumzia suala hili na hapa Serikali mara nyingi inatushajihisha sisi Waheshimiwa, hata taarifa ya kamati yetu pia tumejaribu kuwahamasisha Waheshimiwa kuwahamasisha wananchi katika kudai risiti.

Lakini suala zima la kudai risiti limekuwa lina ukwasi ndani yake kwa sababu wananchi mara nyingi wanaponunua bidhaa wao wanakuwa wanakimbilia katika suala zima la unafuu wa bei na wafanyabiashara wamekuwa wana ghilba. Hata Mhe. Waziri alikiri kwamba wafanyabiashara wetu wengi wana ghilba na Wazanzibari wanahisi kwamba usipofanya ghilba katika biashara wao wanahisi faida hupati, kwa sababu katika eneo moja la ghilba ambalo tunalipigia kelele ni eneo la msamaha wa kodi katika bidhaa muhimu wakati wa Ramadhan wafanyabiashara wanakuwa wanapunguziwa kodi lakini bidhaa hatuzioni kupunguzwa bei.

Sasa na hili katika suala zima la risiti wafanyabiashara wengi wananchi wanapokwenda kununua bidhaa wanakuwa wanawapa bei mbili tofauti wanawaambia ukitaka risiti nitakupa bei hii, kama hutaki risiti nitakupa bei hii. Sasa mwanadam kwa unyonge wake au kwa kutaka unafuu anaona bora yeye asipate risiti ili kile kitu apate apunguziwe bei. Sasa nimuombe Mhe. Waziri namna au haja ya kuharakisha ili kupata *electronic* risiti. Mhe. Mwenyekiti, karibuni sisi tulikwenda Arusha lakini nilipata mshangao mkubwa sana kwamba tulipofika kwenda kupata

mahitaji ya mlo wa asubuhi tuliagizishia chakula cha kawaida, lakini wakati tunaomba bili basi tuliletewa risiti za *electronic* nikasema hii ni hatua kubwa ambayo wenzetu wamefikia kwamba sio kwenye maduka tu mpaka kwenye mikahawa ya kawaida sasa hivi hulipi malipo katika hali ya kawaida, sasa wenzetu wameshapiga hatua kubwa iliyokuwepo na hili lina faraja kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tumelikuta Arusha lakini pia niliwahi kulikuta nchi za nje kwamba unapolipa bidhaa uliyonunua hata zile bidhaa zenyewe yale malipo unayakuta yameshatawanywa, yaani unalipa lakini risiti inakwambia kwamba asilimia tano Serikali Kuu, asilimia mbili Serikali za Mitaa, asilimia tatu unalipia *VAT*. Sasa ukilipa moja kwa moja kila sehemu unakuta ule mgawanyo umeshafanyika kwa uwazi pasipo na kuanza kugawa tu labda halmashauri ngapi na huyu ngapi. Najua Mhe. Waziri juzi alihudhuria kikao kile cha uzinduzi wa kulipa kwa mtandao katika malipo ya kisasa yana mambo mengi. Sasa nilikuwa hapa nimsisitize tu kufanya uharakishaji ili na sisi hilo suala tuweze kulifanyia kazi kwa haraka.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri kwa namna ya jitihada aliyoifanya na umahiri wake na kuweza kufikia pahala kuweza kuwabaini wajanja wasioitakia mema Serikali yetu kwa kufanya ubadhirifu katika Wizara yake. Nimuombe Mhe. Waziri, pamoja na jitihada alizozichukua Wizara imejisafisha imeweza kujenga matumaini lakini bado aendeleze jitihada hizi kwa wale ambao wamebakia hawaitakii mema nchi yetu kwa kufanya udokozi, basi nao asiache kuwachukulia hatua kama hatua za awali ambazo ameanza kuzichukua. Busara zake, hekima zake na utendaji wake umeanza kutupa nguvu sisi wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo nataka nimtanabahishe Mhe. Waziri kwamba pamoja na kubaini katika watu ambao

wamemzunguka katika eneo lake lakini bado tuna eneo ambalo sasa hivi limekuwa linatupa tabu katika Serikali yetu katika Mawizara tofauti Kitengo cha *PMU*. Mhe. Mwenyekiti, vitengo vya manunuzi katika Wizara tofauti kidogo vimekuwa vinatupa tabu na vinaitia hasara Serikali kwa sababu unaweza ukauona wizi wa haraka haraka, yaani wizi wa moja kwa moja ukajua tu kwamba huyu mtu labda ameiba milioni 20 au 10 lakini kuna wizi unauiba mtu hauoni lakini unaitia hasara Serikali. Vitendo hivi Mhe. Mwenyekiti, vinafika pahala kwamba watu wanafanya *negotiation* na watu wanaochukua tenda matokeo yake tenda nyingi, bidhaa nyingi au kazi nyingi zinakuwa hazifanyiki kwa umakini kwa vile ambavyo tunahitaji vifanyike, mtu akishapewa tenda akishapewa chochote anayefanya kazi maana yake anataka afidie alichokitoa hatima yake kazi zinakuwa hazina ubora. Kazi zikiwa hazina ubora maana yake hatuchukui muda mrefu tunahitaji kuja kufanya matengenezo kwa zile kazi au yale mambo ambayo yamefanyika, vifaa vingi vinakuwa havina ubora kwa muda mfupi kwa sababu tayari yeye mwenyewe mtu aliyepata ile kazi ameshatoa chochote kwenye taasisi hizi za watu wa manunuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri kuangalia hivi vitendo kuna baadhi ya maeneo watu wanakaa kwa muda mrefu hususan katika vitengo hivi, lakini mbali ya vitengo hivi pia washika fedha wetu wanakaa katika maeneo yao kwa muda mrefu tumejenga mazingira na sheria ndio inavyotutaka kwamba wahasibu kila baada ya muda wao huwa wana-*rotate* kutoka Wizara fulani kwenda Wizara nyengine. Lakini baadhi ya vitengo vya fedha kama hawa washika fedha na watu wa manunuzi wao wanakaa katika Mawizara kwa muda mrefu, basi ili kuja kuondosha hili suala la kukaa watu kwa muda mrefu na kujenga mazingira au mazoea baina ya wao na wananchi katika kutoa huduma zao, ni vyema na maeneo haya mengine Mhe. Waziri akayaona na akajaribu kufanya mabadiliko ya mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, yangu mimi kama nilivyosema michango mikubwa iko katika kamati yangu na imewasilishwa hapa na Mhe. Ussi Yahya Haji haya yalikuwa ni vibwagizo tu na pongezi kwa Mhe. Waziri kwa jitihada zake. Sote tumeridhika namna Serikali yetu inavyoongeza mapato katika suala zima la kukusanya mapato, lakini katika masuala mazima ya usimamizi wa hayo mapato katika Wizara zetu tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani asilimia mia. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Kwahani, sasa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na kuwa ni mchangiaji wa mwisho. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu aliyetufikisha hapa tukiwa katika hali ya furaha na amani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu na ushauri utakwenda katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 31 kinachohusu ujenzi wa Afisi za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, Wizara naipongeza kwa juhudi kubwa za ujenzi wa afisi mpya za kisasa niliwahi kumsikiliza mtu mmoja akanambia katika nchi mbali mbali duniani zenye kuendelea nchi inapokuwa na majengo moja kwa moja inakuwa na thamani, na si nchi tu hata mtu mmoja mmoja. Kwa hivyo0, kasi hii ya Serikali yetu ya kuongeza majengo ya afisi za kisasa iende hivi hivi mpaka tuhakikishe tunaondokana na majengo ya zamani yaliyooza. Wanapokuja wataalii hapa wanaanza kuona mabadiliko kuanzia Uwanja wa Ndege wakipita kidogo *Airport* wanakuta Afisi ya *ZRB*, wakizungumza kidogo wanakuta jengo lililokuwa Wizara ya Habari, wakienda kidogo

wanakuta Afisi ya Takwimu mpya, Afisi ya Mwanasheria Mkuu mpya. Sasa kasi hii hii nakushauri Mhe. Waziri tuendelee ili nchi iwe na thamani ya majengo yake.

Mhe. Mwenyekiti, tunayo ardhi njia namba 7 ambako kuna uwekezaji mzuri unaofanyika. Sasa nakushauri miongoni mwa afisi ambazo zitajengwa basi moja ielekee njia namba 7 kusudi tuweze kutanua wigo wa ofisi ziwe katika sehemu mbali mbali.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi naunga mkono sana bajeti hii kwa sababu watendaji wake wote nawajua na nawaamini na ni watu mahiri kabisa, namfahamu Katibu Mkuu, Makamishna wote nawajua ni watu wachapakazi tena wachapakazi hasa. Wewe tena Dkt. Ali Mohamed Shein hakukosea aliona kwamba hapa Mhe. Khalid Salum Mohamed ni *fit* kwa hivyo hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kutokana na muda wetu uliobaki hatuwezi kuendelea na michango mingine. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na mahiri na pia niwashukuru Kamati ya Fedha ikiwemo Mwenyekiti, Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, lakini pia kwa uwasilishaji mzuri wa Mhe. Ussi Yahya Haji na niwapongeze wachangiaji wote waliochangia kwa siku ya leo.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe niakhirishe kikao mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 8:43 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 8/6/2017 saa 3:00 asubuhi)